
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI

## TUME YA MIPANGO

# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25




NOVEMBA, 2023

[illegible]

[illegible]

[illegible]

[illegible]
[illegible]

[illegible]

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ASA | Agricultural Seed Agency |
| ASDP II | Agriculture Sector Development Programme II |
| ATC | Arusha Technical College |
| ATCL | Air Tanzania Company Limited |
| ATMIS | Agriculture Trade Management Information System |
| BRELA | Business Registrations and Licensing Agency |
| BTI | Beekeeping Training Institute |
| BTIP II | Backbone Transmission Investment Project - II |
| CAMARTEC | Centre For Agriculture Mechanization and Rural Technology |
| COASCO | Co-operative Audit and Supervision Corporation |
| COSTECH | Tanzania Commission for Science and Technology |
| CPB | Cereals and Other Produce Board |
| DCF | Development Cooperation Framework |
| DIT | Dar es Salaam Institute of Technology |
| DITF | Dar es Salaam International Trade Fair |
| DMDP | Dar es Salaam Metropolitan Development Project |
| DMI | Dar es Salaam Maritime Institute |
| DUCE | Dar es Salaam University College of Education |
| EAC | East Africa Community |
| EACOP | East Africa Crude Oil Project |
| e-GA | Electronic Government Authority |
| e-HRP | Electronic Human Resource Planning |
| EIA | Environment Impact Assessment |
| e-OPRAS | Electronic Open Performance Review and Appraisal System |
| EP4R | Education Program 4 Result |
| ESIA | Environment and Social Impact Assessment |
| ETH | Engineering Technology Hubs |
| FETA | Fisheries Education Training Agency |
| FORVAC | Forestry and Value Chain Development Programme |
| GePG | Government Electronic Payment Gateway |
| GST | Geological Survey of Tanzania |
| HCMIS | Human Capital Management Information System |
| HESLB | Higher Education Students' Loans Board |
| HGA | Host Government Agreement |
| IDRAS | Integrated Domestic Revenue Administration System |
| IJA | Institute of Judicial Administration |
| IMF | International Monetary Fund |
| ISTA | International Seed Testing Agency |
| JNIA | Julius Nyerere International Airport |
| KIA | Kilimanjaro International Airport |
| LITA | Livestock Training Agency |

| | |
|---|---|
| LNG | Liquefied Natural Gas |
| LSP II | Legislative Support Project II |
| MMEM | Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi |
| MSD | Medical Stores Department |
| MSM | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| MTAKUWWA | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto |
| MTDS | Medium Term Debt Strategy |
| MUCE | Mkwawa University College of Education |
| MUSE | Mfumo wa Ulipaji Serikalini |
| MUST | Mbeya University of Science and Technology |
| NEEC | National Economic Empowerment Council |
| NFRA | National Food Reserve Agency |
| NIDC | National Internet Data Centre |
| NIT | National Institute of Transport |
| NPMIS | National Project Management Information System |
| OECD | Organization for Economic Co-operation and Development |
| OSC | One Stop Centre |
| PFMRP | Public Financial Management Reform Programme |
| PPP | Public-Private Partnership |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund |
| REA | Rural Energy Agency |
| REGROW | Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth |
| SELF | Small Entrepreneurs Loan Facility |
| SEZ/EPZ | Special Economic Zone/Export Processing Zone |
| SGR | Standard Gauge Railway |
| SIDO | Small Industries Development Organization |
| SMMRP | Sustainable Management of Mineral Resources Project |
| STAMICO | State Mining Company |
| SUA | Sokoine University of Agriculture |
| SWIOFish | South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth |
| TADB | Tanzania Agricultural Development Bank |
| TAEC | Tanzania Atomic Energy Commission |
| TAFICO | Tanzania Fisheries Corporation |
| TAFIRI | Tanzania Fisheries Research Institute |
| TALIRI | Tanzania Livestock Research Institute |
| TAMCO | Tanzania Automobiles Manufacturing Company |
| TANESCO | Tanzania Electrical Supply Company |
| TARI | Tanzania Agricultural Research Institute |
| TATC | Tanzania Automotive Technology Centre |
| TBC | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| TBS | Tanzania Bureau of Standard |

| | |
|---|---|
| TCRA | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| TDCs | Technology Development Centres |
| TEA | Tanzania Education Authority |
| TEMDO | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization |
| TESP | Teacher Education Support Project |
| TGC | Tanzania Gemmological Centre |
| TIRDO | Tanzania Industrial Research and Development Organization |
| TOSCI | Tanzania Official Seed Certification |
| TPSF | Tanzania Private Sector Foundation |
| TTCL | Tanzania Telecommunications Corporation, |
| UTT - AMIS | Unit Trust of Tanzania- Asset Management and Investor Services |
| UVIKO-19 | Ugonjwa wa Virusi vya Korona - 19 |

**YALIYOMO**


ORODHA YA VIFUPISHO ..... iv

YALIYOMO ..... iv

MUHTASARI ..... 1

SURA YA KWANZA ..... 5
HALI YA UCHUMI ..... 5
1.1. Utangulizi ..... 5
1.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi Kikanda na Kimataifa ..... 5
1.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia ..... 5
1.2.2. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea ..... 5
1.2.3. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi ..... 6
1.2.4. Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ..... 6
1.2.5. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ..... 7
1.3. Hali ya Uchumi wa Taifa ..... 8
1.3.1. Ukuaji wa Uchumi ..... 8
1.3.2. Mfumuko wa Bei ..... 9
1.3.3. Sekta ya Nje ..... 12
1.3.4. Sekta ya Fedha ..... 13
1.3.5. Deni la Serikali ..... 18
1.3.5.1. Mwenendo wa Deni la Serikali ..... 18
1.4. Maendeleo ya Watu ..... 18
1.4.1. Ongezeko la Idadi ya Watu mwaka 2022 ..... 18
1.4.2. Viashiria vya Maendeleo ya Watu ..... 19
1.4.2.1. Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ..... 19
1.4.2.2. Upatikanaji wa Chakula ..... 19

SURA YA PILI ..... 21
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO ..... 21
2.1. Utangulizi ..... 21
2.2. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2023/24 ..... 21
2.2.1. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2022/23 ..... 21
2.2.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2023/24 ..... 21
2.3. Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ..... 22
2.3.1. Miradi ya Kielelezo ..... 22
2.3.2. Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi ..... 29
2.3.2.1. Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma ..... 29
2.3.2.2. Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi ..... 44

2.3.2.3. Mapinduzi ya TEHAMA ........ 51
2.3.3. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma ........ 54
2.3.3.1. Uzalishaji Viwandani ........ 54
2.3.3.2. Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia ASDP II ........ 59
2.3.3.3. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia ........ 69
2.3.3.4. Huduma ........ 70
2.3.4. Kukuza Biashara na Uwekezaji ........ 77
2.3.4.1. Huduma za Biashara na Masoko ........ 77
2.3.4.2. Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji ........ 80
2.3.5. Kuchochea Maendeleo ya Watu ........ 81
2.3.5.1. Afya ........ 81
2.3.5.2. Ustawi na Maendeleo ya Jamii ........ 89
2.3.5.3. Elimu ........ 91
2.3.5.4. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ........ 100
2.3.5.5. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ........ 101
2.3.5.6. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ........ 104
2.3.5.7. Usimamizi wa Maafa Nchini ........ 106
2.3.6. Kuendeleza Rasilimali Watu ........ 107
2.3.6.1. Ujuzi na Uwezeshaji ........ 107
2.3.7. Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma ........ 108
2.3.8. Uwekezaji Kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania ........ 108
2.3.9. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ........ 109
2.3.10. Ufuatiliaji wa Miradi katika kipindi cha Mwaka 2022/23 ........ 109
2.3.11. Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23 ........ 110
2.3.12. Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto ........ 111

SURA YA TATU ........ 114
MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2024/25 ........ 114
3.1. Utangulizi ........ 114
3.2. Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ........ 115
3.2.1. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ........ 115
3.2.2. Misingi *(Assumptions)* ya Mpango kwa Mwaka 2024/25 ........ 115
3.3. Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2024/25 ........ 116
3.3.1. Miradi ya Kielelezo ........ 116
3.3.2. Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi ........ 116
3.3.2.1. Kuimarisha Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji ........ 116
3.3.2.2. Mapinduzi ya TEHAMA ........ 117
3.3.2.3. Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi ........ 118

3.3.3. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma .......... 119
3.3.3.1. Uzalishaji Viwandani .......... 119
3.3.3.2. Kilimo, Mifugo na Uvuvi .......... 119
3.3.3.3. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia .......... 120
3.3.3.4. Huduma .......... 121
3.3.4. Kukuza Biashara na Uwekezaji .......... 121
3.3.4.1. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji .......... 121
3.3.4.2. Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi .......... 121
3.3.4.3. Kukuza Sekta Binafsi .......... 122
3.3.4.4. Huduma za Biashara na Masoko .......... 122
3.3.4.5. Ushirikiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia .......... 122
3.3.5. Kuchochea Maendeleo ya Watu .......... 122
3.3.5.1. Afya .......... 122
3.3.5.2. Ustawi na Maendeleo ya Jamii .......... 123
3.3.5.3. Elimu .......... 123
3.3.5.4. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi .......... 123
3.3.5.5. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira .......... 123
3.3.5.6. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi .......... 124
3.3.6. Kuendeleza Rasilimali Watu .......... 124
3.3.7. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi .......... 124

SURA YA NNE .......... 125
UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2024/25 .......... 125
4.1. Utangulizi .......... 125
4.2. Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2024/25 .......... 125
4.3. Vyanzo vya Mapato ya Kugharamia Mpango kwa Mwaka 2024/25 .......... 125
4.4. Mapato ya Ndani .......... 125
4.4.1. Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi .......... 125
4.5. Mikopo na Misaada .......... 127
4.5.1. Mikopo ya Nje .......... 127
4.5.2. Mikopo ya Ndani .......... 127
4.5.3. Misaada ya Nje .......... 127
4.6. Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Kugharamia Miradi ya Maendeleo .......... 128

SURA YA TANO .......... 129
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA .......... 129
5.1. Utangulizi .......... 129
5.2. Misingi na Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini .......... 129
5.3. Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini .......... 130
5.4. Muundo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini .......... 130

5.5. Mgawanyo wa Majukumu ........................................ 130

SURA YA SITA ........................................ 131
VIHATARISHI NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO ........................................ 131
6.1. Utangulizi ........................................ 131
6.2. Vihatarishi vya Ndani na Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo ........................................ 131

## MUHTASARI

Mipango ya maendeleo katika Taifa letu imekuwa ikiongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Dira hii ya Taifa ya Maendeleo 2025 ina azma ya kuiwezesha Tanzania kuwa nchi yenye maisha bora na mazuri; amani, utulivu na umoja; utawala na uongozi bora; jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi na uchumi imara wenye kuhimili ushindani. Ili kufanikisha malengo hayo ya Dira tulijiwekea lengo la kukuza uchumi hadi kufikia kiwango uchumi wenye hadhi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Dira hii imekuwa ikitekelezwa kupitia Programu mbalimbali na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Miaka 15 wa mwaka 2011/12 – 2025/26 ambao umegawanyika katika vipindi vitatu (3) vya utekelezaji (2011/12 – 2015/16, 2016/17 – 2020/21 na 2021/22 – 2025/26), kila kipindi kikiwa na dhima mahsusi kwa ajili ya kufikia azma ya Dira 2025. Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2011/12 - 2015/16 ulikuwa na dhima ya Kufungulia Fursa Fiche za Ukuaji wa Uchumi. Aidha, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 ulikuwa na dhima ya Kujenga Uchumi wa Viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 una dhima ya kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu na umelenga kuongeza ufanisi na tija katika viwanda kwa kutumia rasilimali zinazopatikana kwa wingi nchini. Mpango huu wa Tatu wa Maendeleo ambao ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na unashabihiana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Matokeo ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 kwa kipindi cha miaka 22 iliyopita yamechochea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa kiwango cha wastani wa asilimia 6. Ukuaji huu imara na thabiti umetokana na misingi na sera madhubuti za uchumi jumla zilizotekelezwa na Serikali katika kipindi chote cha zaidi ya miongo miwili. Jitihada na ushirikiano wa Serikali na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo nchini zimechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji huu wa uchumi kwa kiwango hiki ambacho ni cha juu ukilinganisha na nchi nyingi katika ukanda wetu na hata zile zenye hadhi ya kipato cha kati. Kutokana na ukuaji huo, mnamo mwezi Julai, 2020, Pato la Mtu nchini lilifikia Dola za Marekani 1,080 na kuiwezesha nchi yetu kufuzu kuingia katika kundi la nchi zenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati cha chini kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na Benki ya Dunia.

Aidha, katika kipindi hicho cha miaka 22 (2000 - 2022), viashiria mbalimbali vya ustawi na maendeleo ya jamii vimeendelea kuimarika ikiwemo kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kwa watanzania kutoka miaka 65.5 mwaka 2019 hadi miaka 66.2 mwaka 2021 ikiwa ni jitihada za kufikia lengo la miaka 68 mwaka 2025, kuimarika kwa upatikanaji na ubora wa huduma za afya, elimu, maji na umeme nchini kote. Mathalan, kwa upande wa umeme, asilimia 89.19 ya vijiji vyote nchini vimeunganishwa na huduma hiyo, katika sekta ya elimu, kwa kiwango cha uandikishaji wa jumla (*Gross Enrollment Rate*) wa wanafunzi wa elimu ya msingi

kimeongezeka kutoka asilimia 94.6 mwaka 2012 hadi asilimia 113.2 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.6; kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari (kidato I - IV) kimeongezeka kutoka asilimia 47.4 mwaka 2021 hadi asilimia 48.2 mwaka 2022 kiwango ambacho pia ni zaidi ya lengo la asilimia 48 tulilojiwekea ifikapo mwaka 2025; kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari ya upili (kidato V - VI) kimeongezeka kutoka asilimia 6.7 mwaka 2021 hadi asilimia 7.6 mwaka 2022 ikiwa ni jitihada za kufikia lengo la asilimia 10 tulilojiwekea mwaka 2025. Katika sekta ya afya, vifo vya watoto umri chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36 kutoka vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022 sambamba na kupungua Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2014/15 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022. Katika sekta ya maji miradi 630 yenye vituo 6,553 vya kuchotea maji vinavyonufaisha wananchi wapatao 4,393,274 kwenye vijiji 1,390 imekamilika. Takwimu hizi zinaashiria kwamba nchi yetu inapiga hatua kuelekea malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, ilibainika kuwa asilimia 65.6 ya wananchi Tanzania Bara wanaishi maeneo ya vijijini ambapo shughuli kubwa ya kiuchumi ya wananchi ni kilimo (kilimo mazao, uvuvi na ufugaji) na inachangia zaidi ya ya asilimia 25 ya Pato la Taifa. Kwa muktadha huo, Mipango ya Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2022/23 na 2023/24 kwa kiasi kikubwa ililenga kuongeza tija katika sekta za uzalishaji hususan kilimo, kuimarisha huduma za maendeleo ya jamii vijijini kwa kupanga na kutekeleza programu na miradi mbalimbali itakayoongeza upatikanaji wa huduma za jamii kama elimu, afya, maji, umeme, miundombinu ya usafiri na kupanga na kupima ardhi. Miradi iliyotekelezwa inajumuisha: miradi ya usambazaji umeme vijijini; mradi wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini; ujenzi wa barabara na madaraja; elimumsingi na sekondari bila ada; na miradi ya ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka 2022/23 na robo ya kwanza ya mwaka 2023/24 ulifanikisha pamoja na mambo mengine: Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 630 yenye vituo 6,553 vya kuchotea maji vinavyonufaisha wananchi wapatao 4,393,274 kwenye vijiji 1,390; kuendelea na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika zahanati (5,892) na vituo vya afya (759) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 54; kutatuliwa kwa migogoro ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 975; kuandaliwa hatimiliki ya Kimila 7,438; kupimwa kwa mipaka ya vijiji 80; kukamilika kwa matengenezo ya mtandao wa barabara za mijini na vijijini wenye urefu wa km 22,873.47; na kukamilika kwa ununuzi wa vifaa tiba vya afya ya kinywa na macho kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri 71, vifaa tiba vya zahanati 300 na vifaa tiba katika vituo vya Afya 159.

Mafanikio haya ni matokeo ya maamuzi sahihi ya Serikali ya kupanga kwa muda mrefu, misingi thabiti ya uchumi na utekelezaji wa sera madhubuti za uchumi jumla, jitihada za makusudi za serikali kujenga mazingira wezeshi na rafiki ili kuchochea shughuli za kiuchumi na maendeleo nchini pamoja na ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo katika utekelezaji wa agenda ya maendeleo. Aidha, hadi Juni 2023 Pato la Mtu liliongezeka hadi Dola za Marekani 1,200 ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za Serikali kuiwezesha Tanzania kufikia Pato la Mtu la Dola za Marekani 3,000 kama ilivyoainishwa katika *Composite Goal*.

Katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea kuwekeza katika miradi ya maendeleo vijijini na kuongeza tija katika shughuli za uzalishaji hususan kilimo ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuwa na ukuaji jumuishi. Maeneo yatakayopewa msukumo mkubwa ni pamoja na: Kuendelea kuboresha miundombinu ya usafirishaji kwa kukamilisha miradi ya mtandao wa barabara kwa kujenga na kukarabati barabara; kujenga na kukarabati miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme vijijini na kwenye vitongoji;kuongeza uwekezaji katika miundo mbinu ya mawasiliano na teknolojia ya habari kupitia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda; kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo ikiwemo kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo; kuratibu na kusimamia shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, lishe na ustawi wa jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ya msingi kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri; kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimumsingi na sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuratibu utolewaji wa elimumsingi na sekondari bila ada; na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za elimumsingi na sekondari. Aidha, msisitizo wa pekee utawekwa katika kukamilisha programu na miradi ya maendeleo inayoendelea kabla ya kuanza kusajili na kuijumuisha miradi mipya katika Bajeti ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2024/25 ili kuepuka kuwa na miradi mingi inayochukua muda mrefu kukamilika na kuanza kuwaletea wananchi faida iliyokusudiwa katika miradi. Hatua hii pia itaiwezesha serikali kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mipango ya Maendeleo ya kila mwaka ni nyenzo muhimu ya matumizi bora ya rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Aidha, Mipango hii huhakikisha malengo ya Dira 2025 yanafuatiliwa na kusimamiwa kila mwaka ili kuweza kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini. Hivyo, Mapendekezo haya yanajenga msingi wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Aidha, Mapendekezo ya Mpango yameainisha maeneo mahsusi ya kipaumbele yatakayozingatiwa katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/25 kwa kuzingatia rasilimali chache zilizopo. Kwa ujumla katika mwaka 2024/25 msisitizo utawekwa katika kuchochea shughuli mbalimbali za kiuchumi; kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na maendeleo; na kuimarisha

ushiriki wa sekta binafsi katika maandalizi na utekelezaji wa mipango, uwekezaji na uzalishaji nchini.

Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 yamezingatia miongozo na mikakati ya maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Aidha, kitabu hiki kimegawanyika katika sura sita (6): Sura ya kwanza (1) ni mapitio ya hali ya uchumi; Sura ya pili (2) ni mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/23 na robo ya kwanza ya mwaka 2023/24; Sura ya tatu (3) inaelezea maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2024/25; Sura ya nne (4) ni ugharamiaji wa Mpango; Sura ya tano (5) inaainisha utaratibu wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango; na sura ya sita (6) inaainisha vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na namna ya kukabiliana navyo.




# 1. HALI YA UCHUMI

# SURA YA KWANZA

# HALI YA UCHUMI

## 1.1. Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa kifupi mwenendo wa uchumi na uchambuzi wa viashiria vya uchumi jumla nchini, kikanda na dunia kwa mwaka 2022 pamoja na mwelekeo kwa mwaka 2023 na 2024. Uchambuzi wa viashiria vya uchumi na mwenendo wake ni muhimu katika kupanga maendeleo kwa kuwa inawezesha kujua hali ya uchumi nchini na dunia kwa jumla hatua ambayo inawezesha kupendekeza sera sahihi za kiuchumi. Aidha, uchambuzi wa viashiria vya uchumi jumla vilivyokwisha kutokea (lag macro economic indicators) na viashiria vya uchumi jumla vinavyotokea sasa (lead macro economic indicators) unajenga msingi imara wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Kwa ujumla, kasi ya ukuaji wa uchumi duniani katika kipindi cha mwaka 2022 imepungua hadi asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2021. Hali hii pia ilijitokeza kwa upande wa Tanzania, ambapo kasi ya ukuaji uchumi wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2022 ilipungua hadi asilimia 4.7 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2021. Aidha, katika kipindi cha kipindi cha Januari hadi Juni 2023, kasi ya ukuaji wa uchumi nchini imeongezeka kufikia asilimia 5.3 ikilinganishwa na asilimia 5.1 kipindi kama hicho mwaka 2022.

## 1.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi Kikanda na Kimataifa

### 1.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba 2023 kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kutoka asilimia 6.3 mwaka 2021 hadi asilimia 3.5 mwaka 2022. Upungufu huo unatokana na sababu mbalimbali ikiwemo kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa China na India, athari za UVIKO-19, vita kati ya Urusi na Ukraine na utekelezaji wa sera za fedha kukabiliana na mfumuko wa bei katika mataifa makubwa hususan Marekani na Ulaya. Aidha, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2023 na asilimia 2.9 mwaka 2024 kutokana na kuendelea kwa vita kati ya Urusi na Ukraine, mabadiliko ya tabianchi na Sera ya Marekani ya kuongeza riba.

### 1.2.2. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Kulingana na taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba 2023 (Jedwali Na. 1), kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea imepungua kutoka asilimia 5.6 mwaka 2021 na kufikia asilimia 2.6 mwaka 2022. Upungufu huo wa kasi ya ukuaji wa uchumi umesababishwa na maamuzi ya kupandisha riba za benki kuu katika nchi zilizoendelea hususan Marekani na baadhi ya nchi za Ulaya, madhara ya vita kati ya Urusi na Ukraine inayoendelea kuyumbisha uchumi wa dunia hususan kuongezeka kwa gharama za maisha kulikosababishwa na mfumuko wa bei za

nishati barani Ulaya na nchi ya Marekani pamoja na kuongezeka kwa bei za vyakula katika soko la dunia. Aidha, uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kupungua na kufikia ukuaji wa asilimia 1.5 mwaka 2023 na asilimia 1.4 mwaka 2024.

### 1.2.3. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba 2023 (*Jedwali Na. 1)* inaonesha kuwa, kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi umepungua kutoka asilimia 6.8 mwaka 2021 kufikia asilimia 4.1 mwaka 2022. Upungufu huo wa kasi ya ukuaji wa uchumi unatokana na madhara ya vita kati ya Urusi na Ukraine ambayo yameendelea kuathiri uchumi wa nchi hizi, madhara ya UVIKO – 19, mabadiliko ya Tabia ya Nchi na Sera za Fedha za Marekani za kukabiliana na mfumuko wa bei ambazo pamoja na mambo mengine zimesababisha kuendelea kuongezeka kwa riba katika masoko ya fedha ya kimataifa. Aidha, kiwango cha ukuaji wa uchumi wa China umepungua kutoka asilimia 8.4 mwaka 2021 hadi asilimia 3.0 mwaka 2022. Upungufu huo unatokana na kudorora kwa kiwango cha uwekezaji hususan katika sekta ya mali zisizohamishika (real estate). Vile vile, kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi za Bara la Asia kinatarajiwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2023 na mwaka 2024. Kadhalika, uchumi wa China unatarajiwa kukua kwa kiwango cha asilimia 5.2 kwa mwaka wa 2023 na asilimia 4.5 kwa mwaka wa 2024. Matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa nchi hizo yanatokana na ukuaji wa haraka wa uchumi katika nchi nyingi za ukanda huo, kukua kwa mauzo nje kuliko ilivyotarajiwa katika bara la Asia pamoja na ukuaji wa uchumi wa Brazil kwa nukta ya asilimia 1.2 na kufikia ukuaji wa nukta ya asilimia 2.1 baada ya kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo katika robo ya kwanza ya mwaka 2023.

### 1.2.4. Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara umepungua kutoka asilimia 4.7 mwaka 2021 hadi asilimia 4.0 mwaka 2022. Upungufu huo unatokana na madhara ya vita kati ya Urusi na Ukraine iliyosababisha mfumuko wa bei za nishati ya mafuta na vyakula pamoja na uhaba wa fedha uliombatana na mabadiliko hasi katika masharti ya biashara. Aidha, ukuaji wa uchumi katika nchi hizo unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2023 kutokana na matarajio ya kupungua kwa uchumi wa Nigeria kutokana na masuala ya kiusalama katika sekta ya mafuta pamoja na changamoto za upatikanaji wa huduma ya umeme nchini Afrika Kusini inayoathiri shughuli za uzalishaji. Hata hivyo, uchumi katika ukanda huo unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 4.0 mwaka 2024 kutokana na kuimarika kwa shughuli za huduma katika robo ya kwanza ya mwaka 2023. ***Jedwali Na. 1 linaonesha mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia.***

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia (Asilimia)**

| Kundi/Mwaka | Ukuaji Halisi | | | | | Matarajio | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Dunia | 3.6 | 2.8 | -2.8 | 6.3 | 3.5 | 3.0 | 2.9 |
| Nchi Zilizoendelea | 2.3 | 1.7 | -4.2 | 5.6 | 2.6 | 1.5 | 1.4 |
| Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia | 4.7 | 3.6 | -1.8 | 6.8 | 4.1 | 4.0 | 4.0 |
| Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi za Bara la Asia | 6.4 | 5.2 | -0.5 | 7.5 | 4.4 | 5.3 | 5.0 |
| Nchi za Afrika Kusini mwaJangwa la Sahara | 3.2 | 3.3 | -1.7 | 4.7 | 4.0 | 3.3 | 4.0 |

***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO), Oktoba 2023*

**1.2.5. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Oktoba 2023, uchumi wa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ulikua kwa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2021. Aidha, Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa nchi hizo kinatarajiwa kushuka kufikia asilimia 3.5 mwaka 2023.

Kwa upande mwingine, uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ulikua kwa wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2021 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2**. Aidha, uchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2023.

**Jedwali Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

| Nchi | Ukuaji Halisi | | Matarajio |
|---|---|---|---|
| | 2021 | 2022 | 2023 |
| **SADC** | | | |
| Angola | 1.1 | 2.8 | 3.5 |
| Botswana | 11.8 | 6.4 | 3.7 |
| Tanzania | 4.9 | 4.7 | 5.2 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| DRC | 6.2 | 6.6 | 6.3 |
| Eswatin | 7.9 | 0.5 | 2.8 |
| Lesotho | 2.1 | 2.1 | 2.2 |
| Madagascar | 5.7 | 4.2 | 4.2 |
| Malawi | 4.6 | 0.8 | 2.4 |
| Mauritius | 3.5 | 8.3 | 4.6 |
| Msumbiji | 2.3 | 4.1 | 5 |
| Namibia | 2.7 | 3.8 | 2.8 |
| Seychelles | 7.9 | 8.8 | 3.9 |
| Zambia | 4.6 | 3.4 | 4 |
| Zimbabwe | 8.5 | 3 | 2.5 |
| Afrika ya Kusini | 4.9 | 2 | 0.1 |
| **Wastani** | **5.3** | **4.1** | **3.5** |
| **EAC** | | | |
| Burundi | 3.1 | 1.8 | 3.3 |
| Kenya | 7.5 | 5.4 | 5.3 |
| Rwanda | 10.9 | 6.8 | 6.2 |
| DRC | 6.2 | 6.6 | 6.3 |
| Sudani Kusini | 5.3 | 6.6 | 5.6 |
| Tanzania | 4.9 | 4.7 | 5.2 |
| Uganda | 6 | 4.9 | 5.7 |
| **Wastani** | **6.3** | **5.3** | **5.4** |

***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO) toleo la Aprili 2023*

## 1.3. Hali ya Uchumi wa Taifa


### 1.3.1. Ukuaji wa Uchumi

Mwaka 2022, thamani halisi ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 ilikuwa shilingi trilioni 141.9 ikilinganishwa na shilingi trilioni 135.5 mwaka 2021. Aidha, kiwango halisi cha ukuaji wa Pato la Taifa kilifikia asilimia 4.7 mwaka 2022. Kiwango hicho cha ukuaji kilitokana na: mikakati iliyochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari za vita inayoendelea nchini Ukraine; na madhara yaliyotokana na UVIKO - 19; uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan makaa ya mawe; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi; na kuongezeka kwa shughuli za utalii. Aidha, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.2 mwaka 2023 na asilimia 5.8 mwaka 2024.

Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika (current prices) liliongezeka hadi shilingi trilioni 94.2 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023. kutoka shilingi trilioni 84.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 liliongezeka hadi shilingi trilioni 73.5 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023 kutoka shilingi trilioni 69.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa

na ongezeko la  Pato halisi la asilimia 5.3. Ukuaji huo ulitokana na jitihada za Serikali za kuweka mazingira wezeshi ya ukuaji wa kiuchumi na sera madhubuti za uchumi jumla ikiwa ni pamoja na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei. Shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa zilikuwa: kilimo (asilimia 14.6), ujenzi (asilimia 10.3), biashara na matengenezo (asilimia 9.8), fedha na bima (asilimia 9.7), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 9.1) na uzalishaji viwandani (asilimia 9.0).

**Kielelezo Na. 1: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Nusu ya Kwanza Mwaka 2019 –2023**




**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023**

### 1.3.2. Mfumuko wa Bei

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO) ya Aprili 2023, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka kwa kiwango kikubwa na kufikia wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2021. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2021. Vile vile, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.2 mwaka 2021. Mwaka 2022, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulifikia wastani wa asilimia 14.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 11.0 mwaka 2021. Kwa ujumla, kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulitokana na kupanda kwa bei za nishati na vyakula kulikosababishwa na kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji (disruption of supply chain) kutokana na vita inayoendelea nchini Ukraine pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la

Fedha la Kimataifa (IMF - WEO) ya Oktoba 2023, mfumuko wa bei wa dunia unatarajiwa kupungua hadi asilimia 6.9 mwaka 2023 na asilimia 5.8 mwaka 2024.


**(a) Mfumuko wa Bei Nchini**

Mwaka 2022, Mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2021. Katika kipindi kilichoishia Septemba 2023, mfumuko wa bei ulipungua na kufikia asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3 hadi 7. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma, kuongezeka kwa upatikanaji wa mazao ya chakula nchini na utekelezaji wa sera za fedha.

Katika kipindi kilichoishia Septemba 2023, mfumuko wa bei wa vyakula na vinywaji baridi ulipungua na kufikia asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 8.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya upandaji bei ya bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kulitokana na kupungua kwa bei za vyakula kama vile mchele, mtama, uwele, unga wa mahindi, mafuta ya kula, mihogo, viazi, matunda na mafuta ya kupikia. Sambamba na hilo, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula na nishati (Core Inflation) ulifikia wastani wa asilimia 2.3 katika kipindi cha mwaka kilichoishia mwezi Septemba 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya upandaji bei ya bidhaa zisizo za vyakula na nishati kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa nchini ikiwemo saruji (Kielelezo Na. 2a).


Kwa upande mwingine mfumuko wa bei wa nishati, mafuta na ankara za maji ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 0.9 kwa mwaka unaoishia Septemba 2023 ikilinganishwa na asilimia 7.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Hali hii ilitokana na kupungua kwa bei ya nishati ya mafuta katika soko la dunia.

**Kielelezo Na. 2a: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini (Mwaka Unaoishia Septemba 2021 hadi Septemba 2023)**




***Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

**Kielelezo Na. 3b: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Septemba 2022 hadi Septemba, 2023 (2020=100)**




***Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Kielelezo Namba 2b kinaonesha kuwa, Fahirisi za bei zimekuwa na mwenendo imara kutoka Septemba, 2022 hadi Septemba, 2023 ambazo zimekuwa kati ya 108.73 na 112.35 mtawalia. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei pia umekuwa na mwenendo imara ambao uko kati ya asilimia 3.3 na asilimia 4.9.

**(b) Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Afrika Mashariki**

Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifikia wastani wa asilimia 11.2 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.6 mwaka 2021 na unatarajiwa kuongezeka na kufika asilimia 11.9 mwaka 2023. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulitokana na: kupungua kwa uzalishaji wa chakula kwa baadhi ya nchi wanachama na kuongezeka kwa gharama na mahitaji ya mafuta katika nchi hizo; na vita za mara kwa mara katika nchi za Sudani Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, viwango vya mfumuko wa bei kwa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda pekee viliendelea kuwa ndani ya lengo la Jumuiya la mfumuko wa bei usiozidi asilimia 8. Kwa upande mwingine, nchi za Burundi na Rwanda zilikuwa na viwango vikubwa vya mfumuko wa bei mwaka 2022 uliofikia asilimia 18.9 na 13.9 mtawalia. **Jedwali Na. 3** linaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei na matarajio.

**Jedwali Na. 3: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki Mwaka 2021 2022 na Matarajio ya Mwaka 2023 (Asilimia)**

| | Mfumuko wa Bei | | Matarajio |
|---|---|---|---|
| **Nchi** | **2021** | **2022** | **2023** |
| Tanzania | 3.7 | 4.3 | 4.9 |
| Uganda | 2.2 | 6.8 | 7.6 |
| Kenya | 6.1 | 7.6 | 7.8 |
| Rwanda | 0.8 | 13.9 | 8.2 |
| Burundi | 8.3 | 18.9 | 16 |
| Sudani ya Kusini | 30.2 | 17.6 | 27.8 |
| DRC | 9 | 9 | 10.8 |
| Wastani kwa Afrika Mashariki | **8.6** | **11.2** | **11.9** |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) toleo la Julai 2023 na Takwimu za nchi husika.

**1.3.3. Sekta ya Nje**

Sekta ya nje imeendelea kukabiliwa na athari za mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia uliosababishwa na vita nchini Ukraine, masalia ya UVIKO-19 nchini China na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii imesababisha kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa na huduma duniani na hivyo kupekelea kupanda kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali katika soko la dunia.

**(a) Urari wa Malipo ya Kawaida**

Urari wa malipo yote ya nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,860.1 mwaka 2022/23. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kutokana na athari hasi kwenye mnyororo wa uzalishaji na ugavi wa bidhaa duniani na malipo ya Serikali nje ya nchi. Kuongezeka kwa nakisi hiyo katika urari wa malipo ya kawaida kumepelekea kupungua kwa ukwasi wa fedha za kigeni (foreign currency liquidity) nchini hasa dola za Marekani ambazo

hutumika zaidi katika kulipia bidhaa na huduma mbalimbali kutoka nje ya nchi.

**(b) Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa na Huduma**

**Urari wa Biashara ya Bidhaa**

Urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 7,100.3 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,616.0 mwaka 2021/22. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama za uagizaji bidhaa kutoka nje, hususan mafuta ya petroli, mashine, vyombo vya usafirishaji na mbolea. Hali hii kwa kiwango kikubwa ilichangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa kutokana na kuvurugika kwa mnyonyoro wa uzalishaji na ugavi duniani.

**Urari wa Biashara ya Huduma**

Urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,889.1 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,904.4 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 51.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii na usafirishaji kufuatia juhudi za Serikali katika kuvutia watalii kutoka nchi mbalimbali na kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii kutokana na kupungua kwa athari za UVIKO-19.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma**

Urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,211.2 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,711.6 mwaka 2021/22. Hii ilichangiwa zaidi na ongezeko la gharama za uagizaji wa bidhaa. Kuongezeka kwa nakisi hii katika urari wa biashara na huduma, imesababisha upungufu wa upatikanaji wa fedha za kigeni kwenye mzunguko wa uchumi na kusababisha kuongezeka kwa viwango vya kubadilishia fedha za kigeni dhidi ya shilingi ya Tanzania.

**(c) Akiba ya Fedha za Kigeni**

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi Juni 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 5.45, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.9. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**1.3.4. Sekta ya Fedha**

**(a) Ujazi wa Fedha na Karadha**

Katika mwaka 2022/23, Serikali kupitia Benki Kuu ilitekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwenye uchumi ili kukabiliana na shinikizo la ongezeko la mfumuko wa bei linalotokana na mitikisiko ya kiuchumi duniani lililosababishwa na vita nchini Ukraine na mwendelezo wa athari za UVIKO-

19 bila kuathiri kasi ya ukuaji wa kiuchumi. Utekelezaji huo ulilenga kuhakikisha uwepo wa kiwango cha ukwasi kwenye mfumo wa kibenki kinachoendana na mahitaji halisi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kufuatia utekelezai huo, ukuaji wa ujazi wa fedha ulikuwa sambamba na malengo ukichangiwa na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na UVIKO - 19 na hivyo kuchochea ongezeko la mahitaji ya mikopo kutoka sekta binafsi. Katika kipindi hicho, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa wastani wa asilimia 13.7 na kufikia shilingi bilioni 42,185 kutoka shilingi bilioni 35,500.1 mwishoni mwa mwaka 2021/22. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa wastani wa asilimia 13.6 hadi kufikia shilingi bilioni 32,593.7 mwezi Juni 2023 kutoka shilingi bilioni 27,621.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) uliongezeka kwa wastani wa asilimia 10.1 na kufikia shilingi bilioni 20,429.2 Juni 2023 kutoka shilingi bilioni 17,030.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

**(b) Mikopo kwa Sekta Binafsi**

Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 22.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Ukuaji huu unaakisi ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya kwa sekta binafsi kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na janga la UVIKO – 19, jitihada zinaoendelea kufanywa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, pamoja na sera wezeshi za fedha na bajeti.

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, mikopo kwa sekta binafsi iliyoelekezwa kwenye shughuli za kilimo ilikua kwa kasi zaidi, hadi kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 44.5 kutoka asilimia 0.3 kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Ukuaji huu unatokana hatua za ziada za kisera zilizochukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu kwa lengo la kuongeza chachu ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi hususan katika shughuli za kilimo kwa riba nafuu, ikiwemo mkopo maalum wa shilingi trilioni moja kwa benki na taasisi za fedha ili kutoa mikopo kwenye sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10. Aidha, sehemu kubwa ya mikopo imeendelea kuelekezwa katika shughuli binafsi (biashara ndogondogo na biashara za kati) kwa asilimia 38.4, ikifuatiwa na biashara (asilimia 16.1), uzalishaji viwandani (asilimia 10.1) na kilimo kwa asilimia 8.7.

**(c) Viwango vya Riba**

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki iliendelea kuwa tulivu sawa na wastani wa asilimia 3.55 ukilinganisha na wastani wa asilimia 3.22 kwa mwaka 2021/22. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za muda mfupi za Serikali zilifikia wastani wa asilimia 5.73. Viwango vya riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi vimeendelea kupungua kufikia wastani wa asilimia 16.04 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.41 mwaka 2021/22. Mwenendo huu ulichagizwa zaidi na hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu katika kupunguza riba za mikopo. Aidha, wastani wa viwango vya jumla vya riba za amana haukuwa na mabadiliko makubwa kufikia asilimia 8.01 ukilinganisha na

wastani wa asilimia 8.18 mwaka 2021/22.

**(d) Viwango vya Ubadilishaji Fedha**

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kwenye uchumi kufuatia ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia na kupungua kwa fedha za kigeni zinazoingia nchini kutokana na kupanda kwa riba ya sera ya fedha katika nchi zilizoendelea. Hivyo, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,321.69 ikilinganishwa na shilingi 2,309.50 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

**(e) Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki za Biashara**

Sekta ya kibenki imeendelea kuimarika na kutengeneza faida ikiwa na viwango vya kutosha vya mitaji na ukwasi. Viwango vya amana na rasilimali vimeendelea kuongezeka na hivyo kusaidia sekta ya kibenki kubaki imara dhidi ya misukosuko kutoka ndani na nje ya nchi. Uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali zote ulifikia asilimia 18.3 mwezi Juni 2023, ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika kisheria cha asilimia 10. Aidha, uwiano wa ukwasi (*Liquid Assets to Demand Liabilities*) ulikuwa asilimia 25.1 mwezi Juni 2023 juu ya kiwango kinachokubalika kisheria cha angalau asilimia 20 na hivyo kuendelea kuwa toshelevu kwa mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Sekta ya benki imeendelea kutengeneza faida ambapo faida baada ya kodi (kabla ya ukaguzi wa mahesabu) kwa miezi sita ya kwanza ya mwaka 2023 iliongezeka kufikia shilingi bilioni 744.8 kutoka shilingi bilioni 562.8 katika miezi sita ya kwanza ya mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 32.3.

**(f) Mikopo Chechefu**

Ubora wa rasilimali za benki umeendelea kuimarika kutokana na kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu kufikia wastani wa asilimia 5.3 mwezi Juni 2023 kutoka asilimia 7.8 Juni 2022. Hali hii ilichangiwa zaidi na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kwa kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kusimamia ukwasi katika uchumi, hali iliyowezesha wateja kulipa mikopo kwa wakati. Aidha, hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Benki Kuu ikiwemo kuhimiza benki za biashara kuongeza umakini katika kuchakata maombi ya mikopo; kuwaondoa katika sekta ya benki wafanyakazi wa benki wasio waaminifu; kuamuru benki kutumia taarifa za mikopo kutoka katika kanzidata ya taarifa za wakopaji; utekelezaji wa kanuni za kuwalinda watumiaji wa huduma za kibenki kwa kuhakikisha utunzaji wa haki na usawa kwa wateja; na kuhakikisha kunakuwa na uwazi wa taarifa za kifedha kwa kutoa elimu ya fedha kwa watumiaji wa huduma za kifedha, kumesaidia kupunguza viwango vya mikopo chechefu. Vilevile, Benki Kuu ilielekeza benki na taasisi za fedha kuwa na mifumo ya udhibiti na utawala bora kwa kupitia upya mifumo iliyopo ili kukidhi mabadiliko na maendeleo katika sekta ya benki.

### (g) Soko la Upili la Hatifungani

**Mauzo ya Hatifungani za Serikali (Government Bonds Turnover)**
Mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Juni 2023 yaliongezeka kwa asilimia 2.4 na kufikia shilingi trilioni 3.30, ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.22 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Juni 2022. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Serikali kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

**Mauzo ya Hatifungani za Kampuni (Corporate Bonds Turnover)**
Mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Juni 2023 yaliongezeka kwa asilimia 19.6 na kufikia shilingi milioni 981.93, ikilinganishwa na shilingi milioni 821.04 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Juni 2022. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Kampuni kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

**Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (Collective Investment Schemes)**
Mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja katika kipindi kilichoishia Juni 2023 ulikuwa mzuri. Thamani ya uwekezaji katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka kwa asilimia 56.79 na kufikia shilingi trilioni 1.52 katika kipindi kilichoishia Juni 2023, ikilinganishwa na shilingi bilioni 971.68 katika kipindi kilichoishia Juni 2022. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine, pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji. Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja.

**Jedwali Na. 4: Mwenendo wa Uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**
**Mwenendo wa Uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

| | | 30 Juni 2023 | | 30 Juni 2022 | | Ongezeko la thamani | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Meneja wa Mifuko** | **Jina la Mfuko** | **Thamani ya Mfuko (TSH)** | **Bei ya Kipande (TSH)** | **Thamani ya Mfuko (TSH)** | **Bei ya Kipande (TSH)** | **Ongezeko la Thamani ya Mfuko** | **Ongezeko la Bei ya Kipande (%)** |
| UTT AMIS Plc | Mfuko wa Umoja | 319,929,433,437.44 | 926.9394 | 288,593,196,846.12 | 833.6269 | 10.86% | 11.19% |
| | Mfuko wa Wekeza Maisha | 9,164,074,761.02 | 792.0333 | 4,378,246,100.78 | 704.1011 | 109.31% | 12.49% |
| | Mfuko wa Watoto | 10,746,136,127.24 | 583.7908 | 5,730,630,816.89 | 519.3197 | 87.52% | 12.41% |
| | Mfuko wa Jikimu | 20,036,285,535.81 | 166.121 | 18,527,361,484.27 | 156.7019 | 8.14% | 6.01% |
| | Mfuko wa Ukwasi | 724,657,653,436.17 | 362.1494 | 434,652,183,962.98 | 321.9263 | 66.72% | 12.49% |
| | Mfuko wa Hatifungani | 423,569,982,148.27 | 115.8205 | 219,794,849,721.34 | 113.8745 | 92.71% | 1.71% |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Watumishi Housing Investments | Mfuko wa Faida | 15,350,267,908.07 | 104.9707 | Mfuko wa Faida ulikuwa bado haujapata idhini ya kutoa huduma ya uwekezaji. | | | |
| Thamani ya Jumla | | **1,523,453,833,354.01** | | **971,676,468,932.37** | | **56.79%** | |

**Chanzo**: UTT AMIS

### (h) Mwenendo wa Soko la Hisa

Mwenendo wa biashara katika soko la hisa hupimwa kwa kuangalia viashiria ambavyo huonyesha mwelekeo wa ufanisi wa soko. Viashiria hivyo ni pamoja na: Mtaji wa Soko (Market Capitalisation); Fahirisi za Soko (Share Index); mauzo katika Soko la Hisa; na ushiriki kwenye soko la hisa. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 mwenendo wa Soko la Hisa la Dar es Salaam ulikuwa mzuri. Ufanisi huu umetokana na juhudi za Serikali katika kutoa elimu kuhusu fursa na faida za kuwekeza katika masoko ya mitaji.

**Mtaji wa Soko la Hisa**

Mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani yaani *Domestic Market Capitalisation* katika kipindi kilichoishia Juni 2023 uliongezeka kwa asilimia 4.21 na kufikia shilingi trilioni 10.83 ikilinganishwa na shilingi trilioni 10.39 katika kipindi kilichoishia Juni 2022. Kuongezeka kwa mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani kulitokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa. Kampuni hizo ni pamoja na CRDB Bank Plc, NMB Bank Plc, DSE Plc, National Investment Company Limited (NICO), Swissport Tanzania Plc, Twiga Cement Plc, Tanga Cement Plc, Tanzania Breweries Plc na Tanzania Cigarette Plc.

Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa yaani *Total Market Capitalisation* katika kipindi kilichoishia Juni 2023 ulipungua kwa asilimia 3.99 na kufikia shilingi trilioni 15.01 ikilinganishwa na shilingi trilioni 15.63 katika kipindi kilichoishia Juni 2022. Kupungua kwa Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa kumetokana na kupungua kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE kutoka Soko la Hisa la Nairobi (Cross Listed Companies). Kampuni hizo ni pamoja na National Media Group, Jubilee Holding Limited, Kenya Airways na KCB Group Plc.

**Mauzo ya Hisa (Equity Turnover)**

Katika kipindi kilichoishia Juni 2023, Mauzo ya hisa katika Soko la Hisa yalikuwa shilingi bilioni 107.58, ikilinganishwa na shilingi bilioni 126.63 katika kipindi kilichoishia Juni 2022. Kupungua kwa mauzo kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na janga la UVIKO-19; athari za vita ya Russia na Ukraine; na kupungua kwa fedha za kigeni nchini, ambapo wawekezaji wengi wamehamisha uwekezaji wao kutoka kwenye uwekezaji wa hisa, ambao unaonekana unaweza kupata athari za kiuchumi (perceived risk) kwenda kwenye uwekezaji wa Hatifungani za Serikali (Government Bonds), ambao unaoonekana kuwa salama zaidi yaani *risk free*.

**Fahirisi ya Soko (Market Index)**
Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni za ndani yaani *Tanzania Share Index (TSI)* katika kipindi kilichoishia Juni 2023, iliongezeka kwa asilimia 4.2 na kufikia alama 4,091.81 ikilinganishwa na alama 3,928.55 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Juni 2022. Kuongezeka kwa *Tanzania Share Index* kunaashiria ufanisi wa soko la hisa kwa kampuni za ndani hususan kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE, ambazo zinatoa huduma katika sekta za viwanda na fedha.

Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote yaani *All Share Index* katika kipindi kilichoishia Juni 2023, ilipungua kwa asilimia 4.0 na kufikia alama 1,800.04 ikilinganishwa na alama 1,875.52 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Juni 2022. Kupungua kwa *All Share Index* kumetokana na kupungua kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE kutoka Soko la Hisa la Nairobi.

### 1.3.5. Deni la Serikali

#### 1.3.5.1. Mwenendo wa Deni la Serikali
Hadi Juni 2023, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 82,137.9. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba, 2022 inaonesha kuwa viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Mwaka 2022/23, tathmini ya uwezo wa nchi kukopesheka (Credit Rating) ilikamilika ambapo kampuni za Moody’s Investors Service Ltd na Fitch Rating Services Ltd zilichapisha matokeo ya daraja B2+ na B+ mtawalia. Alama hizo zinabainisha kuwa mwelekeo wa hali ya uchumi, usimamizi wa deni, uwekezaji na hali ya kisiasa nchini ni ya kuridhisha.

## 1.4. Maendeleo ya Watu
### 1.4.1. Ongezeko la Idadi ya Watu mwaka 2022
Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, idadi ya watu Tanzania imeongezeka na kufikia watu 61,741,120 mwaka 2022 kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 3.2. Kati ya idadi hiyo, wanawake ni 31,687,990 sawa na asilimia 51.3 na wanaume ni 30,053,130 sawa na asilimia 48.7 ya watu wote.

Aidha, kwa mujibu wa Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi 2020/21, idadi ya nguvu kazi yenye umri wa miaka 15 na kuendelea imeongezeka kwa asilimia 20.6 kutoka watu 25,750,116 na kufikia watu 31,047,894 sawa na asilimia 54.8 ya idadi ya watu wote mwaka 2020/21. Kuongezeka kwa nguvu kazi ni fursa kubwa nchini katika shughuli mbalimbali za uzalishaji pamoja na sekta za huduma na masoko

### 1.4.2. Viashiria vya Maendeleo ya Watu

Katika kuendelea kuboresha maendeleo ya watu, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo: uboreshaji wa huduma za afya; utoaji wa elimu msingi na sekondari bila ada; usambazaji wa umeme mijini na vijijini; utoaji wa huduma ya maji mijini na vijijini; na utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Aidha, tafiti na taarifa mbalimbali zinazotolewa katika vipindi tofauti zinazohusu viashiria vya maendeleo ya watu zimebainisha kuwa, utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo umekua na matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo:

(i) Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 61.8 mwaka 2012 hadi miaka 65.4 mwaka 2022;
(ii) Vifo vya watoto umri chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36 kutoka vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022;
(iii) Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2014/15 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022;
(iv) Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa jumla (*Gross Enrollment Rate*) wa wanafunzi wa elimu ya msingi kutoka asilimia 94.6 mwaka 2012 hadi asilimia 113.2 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 18.6;
(v) Asilimia 70.1 ya kaya zote nchini Tanzania hutumia vyanzo bora vya maji safi ya kunywa; na
(vi) Kuongezeka kwa idadi ya watu wanaomtumia umeme wa Tanesco kama nishati ya kuangazia kutoka asilimia 21.3 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 37.4 mwaka 2022.

#### 1.4.2.1. Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

Serikali imeendelea kutekeleza awamu ya pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ambapo jumla ya kaya zilizokidhi vigezo na kunufaika zimefikia 1,371,916 mwaka 2022/23 katika halmashauri 186 za Tanzania Bara, Pemba na Unguja. Aidha, hadi Agosti 2023, jumla ya shilingi bilioni 347.9 zimetolewa kuwezesha kaya hizo. Vile vile, jumla ya vikundi 19,960 viliundwa vyenye jumla ya wanachama 269,078 (wanawake 230,930 na wanaume 38,148) kwenye Mamlaka 86 za utekelezaji kwa Tanzania Bara na Zanzibar; na jumla ya miradi 14,236 iliibuliwa na jamii na kuanza kutekelezwa katika mamlaka za utekelezaji 123 ambapo jumla ya kaya za walengwa 660,000 zimeshiriki katika kutekeleza miradi hiyo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 186.34.

#### 1.4.2.2. Upatikanaji wa Chakula

Taarifa ya Tathmini ya Mwisho ya Uzalishaji wa Mazao ya Chakula Msimu wa 2021/22 ilionesha kuwa, hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula ilifikia tani 17,148,290 kwa mlinganisho wa nafaka (*Grain Equivalent*) ambapo mazao ya

nafaka yalikuwa tani 9,233,298 na mazao yasiyo nafaka ni tani 7,914,992. Aidha, Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2022/23 yalikuwa tani 15,053, 034 na ziada ilikuwa tani 2,095,256 za chakula. Kiwango cha Utoshelevu wa chakula (*Self Sufficiency Ratio – SSR*) nchini kilifikia asilimia 114 mwaka 2022/23.

# 2.

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO



# SURA YA PILI

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

## 2.1. Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa muhtasari utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 katika kipindi cha robo ya kwanza. Taarifa mahsusi zilizoainishwa katika sura hii ni bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji na maandalizi ya miradi ya maendeleo, kiasi cha fedha kilichotumika na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji na maandalizi ya baadhi ya miradi ya maendeleo. Vilevile, sura hii inabainisha changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha utekelezaji wa mpango na mikakati ya kukabiliana nazo.

## 2.2. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2023/24

### 2.2.1. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2022/23

Katika mwaka 2022/23, Serikali ilitenga shilingi bilioni 15,006.0 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Hadi Juni 2023, jumla ya shilingi bilioni 13,970.7 zilitolewa, sawa na asilimia 93.1 ya lengo la mwaka. Aidha, fedha hizo zilielekezwa katika utekelezaji wa miradi ya sekta za kimkakati ikiwemo:

(i) Shilingi bilioni 1,990.43 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara, Madaraja na Viwanja vya Ndege;
(ii) Shilingi bilioni 1,628.39 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa *(Standard Gauge Railway)*;
(iii) Shilingi bilioni 1,527.0 kwa ajili ya Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji – MW 2,115;
(iv) Shilingi bilioni 370.14 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu;
(v) Shilingi bilioni 364.48 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini;
(vi) Shilingi bilioni 262.21 kwa ajili ya ununuzi wa ndege;
(vii) Shilingi bilioni 676.8 kwa ajili ya mradi wa usambazaji umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini; na
(viii) Shilingi bilioni 192.63 kwa ajili ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na chanjo za watoto kupitia MSD.

### 2.2.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2023/24

Katika mwaka 2023/24, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 15,215.59 kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 11,993.51, sawa na asilimia 78.43 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,282.1, sawa na asilimia 21.57 ni fedha za nje.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ni shilingi bilioni 4,195.6 sawa na asilimia 27.6 ya bajeti iliyoidhinishwa. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele yaliyopatiwa fedha katika kipindi husika ni kama ifuatavyo:

(i) Shilingi bilioni 646.83 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge Railway);
(ii) Shilingi bilioni 246.99 kwa ajili ya Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji – MW 2,115;
(iii) Shilingi bilioni 167.89 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini;
(iv) Shilingi bilioni 92.57 kwa ajili ya mradi wa usambazaji umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini;
(v) Shilingi bilioni 94.03 kwa ajili ya kuchangia Mtaji wa Kampuni ya EACOP inayotekeleza mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania ambapo Serikali kupitia TPDC inashiriki kama Mbia;
(vi) Shilingi bilioni 445.92 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara, Madaraja na Viwanja vya Ndege;
(vii) Shilingi bilioni 40.65 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu;
(viii) Shilingi bilioni 98.15 kwa ajili ya uboreshaji wa Shirika la Ndege la Tanzania; na
(ix) Shilingi bilioni 33.33 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na chanjo za watoto kupitia MSD.

## 2.3. Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

### 2.3.1. Miradi ya Kielelezo

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo ni kama ifuatavyo:

**(i) Mradi Na. 4281: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR)**

Mradi unalenga kujenga reli ya kisasa (Standard Gauge Railway – SGR) ya kati kwa kiwango cha kimataifa. Ujenzi wa reli ya kati unajumuisha kipande cha kutoka Dar es Salaam (Bandari) - Morogoro- Makutupora- Tabora – Isaka – Mwanza (1,219); Tabora – Kigoma (506); Isaka - Rusumo – Kigali (km 495); Uvinza (Tanzania) – Musongati – Gitega (Burundi) (Km 282); na Kaliua – Mpanda - Karema (km 321). Kukamilika kwa ujenzi wa reli utaongeza mwendokasi wa reli kutoka 30km/h za sasa hadi 160km/h na uendeshaji wake utatumia umeme. Aidha, uwezo wa kubeba mizigo utaongezeka kutoka tani 13 kwa eklesi (axle load) hadi kufikia tani 15 kwa kwa eklesi (axle load). Reli hii itaongeza ufanisi katika kutoa huduma ya kusafirisha mizigo kwenda nchi jirani za DRC, Rwanda, Burundi na Uganda.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, malengo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kati yalikuwa ni: kukamilisha ujenzi wa Reli ya Kati kipande cha kutoka Dar es Salaam -

Morogoro (Km 300) na kuanza uendeshaji; na kuendelea na ujenzi wa njia ya Reli kwa kipande cha kutoka Morogoro - Makutupora (Km 422); Mwanza - Isaka (Km 341); Makutupora – Tabora (Km 368); Tabora - Isaka (Km 165); na kuendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha kwa vipande vya Tabora -Kigoma (Km 506); Isaka - Rusumo – Kigali (km 495); Uvinza (Tanzania) – Musongati – Gitega (Burundi) (Km 282); na Kaliua – Mpanda - Karema (km 321).

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.60 ikiwa ni pamoja na ujenzi wa njia ya kuelekea bandarini (Port link) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 64.81; kipande hiki hakikufikia lengo kutokana na athari za UVIKO - 19 ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi kuchelewa kuwasili nchini. Aidha, ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) kimefikia asilimia 95.41 kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 41.95, kipande cha Makutupora-Tabora (km 371) asilimia 12.32; kipande cha Tabora - Isaka (km 165) asilimia 5.02; na kuanza ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Tabora – Kigoma (Km 506) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 0.29. kwa ujumla ujenzi wa reli ya Kisasa kipande cha Dar es Salaam – Mwanza ulikamilika kwa kujenga kilomita 745 ikilinganishwa na kilomita 713.92 zilizopangwa kujengwa katika mwaka 2022/23.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kununuliwa kwa vichwa viwili (2) vya treni na mabehewa 30 kwa ajili ya majaribio na uendeshaji wa awali; kufanyika kwa malipo kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni 17 vya umeme na seti za treni 10 za kisasa (Electric Multiple Unit - EMU) ambapo utengenezaji wa vichwa vya treni umefikia asilimia 43.2 na utengenezaji wa seti za treni umefikia asilimia 38.8; kununuliwa kwa mabehewa 59 ya abiria ambapo mabehewa 14 yamewasili nchini na mabehewa 45 utengenezaji umefikia asilimia 95; na ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo ambapo utengenezaji umefikia asilimia 42. Jumla ya shilingi bilioni 1,628.39 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 646.83 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(ii) Mradi Na. 3172: Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115)**

Mradi huu unalenga kujenga bwawa la kuzalisha umeme wa MW 2,115, miundombinu ya usafirishaji wa umeme na vituo vya kupozea umeme. Uwekezaji katika mradi huu utaongeza kiwango cha nishati ya umeme kwenye gridi ya Taifa na kuchochea fursa za kiuchumi. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi ni: Kukamilika kwa ujenzi wa handaki la kuchepusha maji (diversion tunnel); kuendelea na ujenzi wa kingo saidizi za kuzuia maji yasichepuke (saddle dam) (asilimia 97.4); ujenzi wa tuta kuu (main dam) (asilimia 98.46); ujenzi wa njia za kupeleka maji kwenye mitambo (power water ways) (asilimia 99.60); ujenzi wa jengo la mitambo (power house) (asilimia 80.43); ujenzi wa kituo cha kupokea na kusafirishia umeme (switchyard) (asilimia 99.37); ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi (asilimia 98.30); ujenzi wa barabara za kudumu (asilimia 50.09); na ujenzi wa daraja la

kudumu (asilimia 96.87). Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 92.74. Aidha, zoezi la ujazaji maji linaendelea ambapo kina cha maji ya bwawa kimefikia mita 164.81 kutoka usawa wa bahari. Kwa mujibu wa Mkataba, Mradi wa JNHPP ulipaswa kukamilika tarehe 14 Juni, 2022. Hivyo mradi umechelewa kukamilika katika maeneo yake yote. Aidha, kuchelewa huko kumetokana na kujitoa katika makubaliano ya kutengeneza mitambo kwa Kampuni zilizotarajiwa kutengeneza mitambo ya kuzalisha umeme (Voith Hydro Private Ltd na Andritz Hydro Private Ltd) zikidai kwamba mradi haukuwa umekidhi vigezo vya kimataifa kuhusu masuala ya mazingira, kuchelewa kuajiriwa kwa wataalamu wa usanifu (key design experts) ambapo hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2020 (yaani miaka miwili tangu kusainiwa kwa Mkataba) wataalamu waliokuwa wameajiriwa walikuwa wanne (4) tu kati ya wataalamu 27 na wataalamu wa ujenzi walikuwa 144 kati ya 177 waliopaswa kuwepo katika eneo la mradi na methodolojia hafifu ya ujenzi wa handaki (diversion tunnel) la kuchepusha maji ya Mto Rufiji hivyo kusababisha maji kuingia katika handaki kabla ya ujenzi wake kukamilika. Kwa kuzingatia maslahi mapana ya utekelezaji wa Mradi, TANESCO ilimuongezea Mkandarasi muda wa Mkataba kwa kipindi ambacho TANESCO ingeona kinafaa pasipo kuongeza gharama za ziada kwa Serikali ili kuwezesha usafirishaji na ufungwaji wa mitambo ya kuzalisha umeme pamoja na upatikanaji wa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na vibali vya wafanyakazi ndani ya muda wa Mkataba. Kufuatia hatua hiyo, TANESCO imemuongezea Mkandarasi muda wa Mkataba hadi 14 Januari, 2024. Jumla ya shilingi bilioni 1,527.0 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 246.99 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(iii) Mradi Na. 4294: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**

Mradi unalenga kuboresha utendaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege, vitendea kazi na kuboresha mazingira ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na majengo, karakana na nyumba. Uboreshaji wa Shirika la Taifa la Ndege la Tanzania unalenga kuongeza ufanisi wa utendaji kwa kuweza kuhudumia soko la ndani na nje ya nchi la kusafirisha mizigo na abiria, kutoa huduma ya kusafirisha mizigo na abiria kwa usafiri wa anga na kuchagiza shughuli za utalii na kilimo ikiwa ni pamoja na kusafirisha mazao yanayoharibika haraka (preshables goods) na madini. Aidha, uboreshaji Shirika la Ndege la Taifa kunaunganisha nchi ya Tanzania na mataifa mengine duniani katika usafiri wa anga na kufanya ATCL iweze kuwa na uwezo wa kushindani na mashirika ya ndege ya kimataifa.

Katika mwaka 2022/23, malengo ya mradi yalikuwa ni kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege nne (4), Ndege moja (1) aina ya Boeing 767-300F ya mizigo, Ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9 Max na Ndege moja (1) Boeing 787–8 Dreamliner; na kuendelea kwa ukarabati wa Karakana ya Matengenezo ya Ndege (Hangar) za JNIA na KIA (KIMAFA) na kuendelea kwa ununuzi wa vifaa na vipuri kwa ajili ya kuwezesha kufanya matengenezo makubwa na madogo ya ndege; na kuendelea na ukarabati wa nyumba zilizopo KIA.

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa malipo ya ununuzi wa ndege moja (1) ya mizigo aina ya Boeing 767-300F iliyowasili Juni 2023 na ndege moja (1) aina Boeing 737-9 Max iliyowasili tarehe 03 Oktoba, 2023 na kufanya jumla ya ndege 14 kati ya ndege 19 zilizoanishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (FYDP III); kufanya sehemu ya malipo ya ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9 Max na Boeing 787 - 8 Dreamliner zinazotarajiwa kuwasili mwezi Desemba 2023 na Januari, 2024. Ndege hizi hazikuwasili kwa wakati kutokana na athari za UVIKO-19 iliyosababisha viwanda vya utengenezaji kufungwa; kufanyika kwa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege moja (1) aina ya Boeing 737-7; kuendelea na ukarabati wa miundombinu katika karakana ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro - KIA (KIMAFA) na JNIA ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; kukamilika kwa ununuzi wa vifaa na vipuri kwa ajili ya kuwezesha kufanya matengenezo makubwa na madogo ya ndege aina zote katika hanga za JNIA na KIA; na kuendelea na ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40. Aidha, ATCL imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 24 ambapo kati ya vituo hivyo, vituo 13 ni vya ndani ya nchi na vituo 11 ni vya nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 262.21 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 98.15 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(iv) Mradi Na. 3155: Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas - LNG)* – Lindi**

Mradi unalenga kuzalisha tani milioni 5 za gesi kwa mwaka. Aidha, mradi utachangia katika ukuaji wa uchumi, fursa za ajira na huduma za ugavi na kibiashara. Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa majadiliano ya Mkataba wa Nchi Hodhi (Host Government Agreement–HGA) na Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (Amended Production Sharing Agreement–PSA) kati ya Serikali na Kampuni za Kimataifa za Nishati (International Energy Companies–IECs) ili kuwezesha utekelezaji wa mradi wa LNG; kuanzisha Ofisi ya Mradi wa LNG kwa ajili ya kuratibu, kuwezesha na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za mradi; na kuanzishwa kwa kampuni ya *TPDC Likong'o LNG Company Limited* itakayoshiriki kikamilifu katika mnyororo wa biashara ya mradi wa LNG. Jumla ya shilingi bilioni 8.59 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 460.66 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(v) Mradi Na. 3176: Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) lenye urefu wa km 1,443**

Mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba lenye urefu wa km 1,443 kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) ambapo km 1,115 za bomba hilo zitapita Tanzania na kusafirisha mafuta ghafi, mapipa 216,000 kwa siku. Vile vile, mradi utajumuisha ujenzi wa matenki ya kuhifadhi mafuta, vituo vya kupasha joto mafuta na nyenzo za kupakia mafuta ya kuuzwa nje. Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa malipo ya fidia kwa wananchi 387 kati ya 388 waliopisha maeneo 14 ya ujenzi wa kambi zitakazotumika wakati wa ujenzi wa bomba; kulipwa fidia kwa wananchi 9,416 kati ya

9,510 wanaopisha eneo la mkuza wa bomba; kuendelea kulipia asilimia 15 ya hisa katika Kampuni ya EACOP ambapo jumla ya dola za Marekani milioni 193.03 zimelipwa; kukamilika kwa ujenzi wa kituo kwa ajili ya kuweka mfumo wa kupasha joto mabomba *(thermal insulation plant)* katika kijiji cha Sojo, Nzega (Tabora); kuendelea na upimaji wa ardhi na uwekaji wa mipaka ya mkuza wa bomba kutoka eneo la mpakani Mutukula, Kagera hadi Chongoleani, Tanga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50; na kuendelea kutoa elimu kuhusu manufaa na fursa zitokanazo na mradi katika mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Jumla ya Shilingi bilioni 164.97 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 68.23 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(vi) Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi (Mbigiri)**

Mradi huu unalenga kujenga kiwanda cha kuzalisha shukari chenye uwezo wa kuzalisha takribani tani 250,000 za sukari kwa mwaka. Mradi unatarajiwa kutoa fursa za ajira 100,000. Mradi huu unaendelea kutekelezwa kwa utaratibu wa joint venture. Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara za mashambani kwa kiwango cha changarawe km 72 na kiwango cha udongo km 100; kupandwa miwa katika hekta 3,133 kati ya hekta 3,600 ambazo zimeunganishwa na mfumo wa usambazaji maji; kuendelea na ujenzi wa bwawa lenye mita za ujazo milioni 3.5 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87; kusajiliwa kwa wakulima 245 wa nje ya kiwanda wenye uwezo wa kulima hekta 817 za miwa zinazoweza kuzalisha tani 34,310 za miwa na kutoa tani 3,431 za sukari; na kununuliwa kwa mtambo wa kupakia miwa "Cane Loader". Kwa ujumla ujenzi wa kiwanda umefikia asilimia 95 na kwa upande wa mashamba ya miwa umefikia asilimia 87. Jumla ya shilingi bilioni 110 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 10.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(vii) Mradi Na. 3115: Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia**

**(a) Utafutaji wa Mafuta Kitalu cha Eyasi – Wembere:**

Miradi hii ni kimkakati yenye lengo la kutafuta mafuta na gesi asilia katika bonde la Eyasi Wembelena Mnazi Bay North. Miradi hii inatatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi. Hatua iliyofikiwa ni kupatikana kwa mkandarasi wa kukusanya na kuchakata taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D zenye urefu wa kilomita 260. Jumla ya shilingi bilioni 2.29 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 5.49 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(b) Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini:**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa Mpango wa Kina wa Uchorongaji wa Kisima (Detailed Drilling Program). Jumla ya shilingi bilioni 2.93 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 87.74 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24

**(viii) Mradi Na. 4015: Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa daraja pamoja na barabara unganishi

zenye urefu wa km 1.66 ambapo ujenzi umefikia asilimia 78. Jumla ya shilingi bilioni 159.76 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 14.88 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(ix) Mradi Na. 4191: Daraja Jipya la Selander (Tanzanite Dar es Salaam)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara unganishi zenye urefu wa km 5.2. Jumla ya shilingi bilioni 1.74 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(x) Mradi Na. 1122: Magadi Soda Engaruka**

Mradi wa Magadi Soda Engaruka unalenga kuzalisha malighafi ya magadi pamoja na bidhaa zinazotokana na magadi ikiwemo madini ya chumvi kwa ajili ya matumizi ya viwandani. Utekelezaji wa mradi huu utachochea ukuaji wa viwanda vya kemikali nchini vinavyotumia magadi kama malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali (downstream industries), kuokoa kiasi cha dola za marekani milioni 11.0 ambazo zinatumika katika kuagiza malighafi ya magadi pamoja na bidhaa zinazotokana na magadi kutoka nje ya nchi na kuongeza ajira za moja kwa moja nchini zisizopungua 1,000. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni: Kukamilika kwa uthamini wa mradi na kuendelea na ulipaji wa leseni za uchimbaji; kufanyika kwa utafiti wa kina wa magadi uliohusisha uchimbaji wa mashimo 16 ya utafiti ambapo kiasi cha magadi katika mfumo wa maji (brine) mita za ujazo bilioni 4.68 ziligunduliwa katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 234; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu. Aidha, ujenzi wa viwanda vya kuchenjua Magadi Soda ulitakiwa uwe umeshaanza. Hata hivyo, kutokana na changamoto za upatikanaji wa fedha za kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, ujenzi wa viwanda hivyo haujaanza. Hivyo, ili ujenzi wa viwanda hivyo uweze kuanza, kiasi cha fidia ya shilingi bilioni 14.48 kinahitajika, ujenzi wa miundombinu ikiwemo Barabara za kutoka Mto wa Mbu kwenda Loliondo na barabara ya Magadi Soda kwenda Sokoni, kuunganisha umeme wenye msongo wa kV 33 kwa ajili ya matumizi katika viwanda hivyo na kuhakikisha uwepo wa maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya viwanda na wananchi na kupatikana kwa Leseni ya uchimbaji na kukamilisha malipo ya ada ya leseni ambapo hadi sasa kiasi kilicholipwa ni dola za Marekani 121,900 kati ya dola 447,600 zinazohitajika kulipwa. Kukamilika kwa maandalizi ya mradi husika kutawezesha mradi kuanza utekelezaji na ujenzi wa viwanda husika unatarajiwa kuanza Machi 2024 na kukamilika Juni 2026. Aidha, uzalishaji wa magadi soda unatarajiwa kuanza Julai 2026. Jumla ya shilingi milioni 385.26 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(xi) Mradi Na. 3171: Makaa ya Mawe Mchuchuma na Mradi Na. 3161: Chuma Liganga**

Mradi huu ni pacha na unalenga Kuzalisha tani milioni tatu (3) za makaa ya mawe, tani milioni 2.9 za chuma (Vanadium na Titanium) pamoja na tani milioni 1.0 za chuma cha pua kwa mwaka. Makaa ya mawe kutoka Mchuchuma yatazalisha umeme wa MW 600, ambapo MW 300 zitatumika katika mradi wa Chuma - Liganga

na MW 300 zitaingizwa katika gridi ya Taifa. Mradi unatarajiwa kuchangia katika agenda ya mageuzi ya viwanda hususan katika maeneo ya saruji, chuma cha pua na mbolea. Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha mradi ambapo hadi kufikia Septemba, 2023, jumla ya shilingi bilioni 15.02 zimelipwa kati ya shilingi bilioni 15.43 kwa wananchi 1,048 kati ya 1,144; kukamilika kwa taratibu za kuwapata wachimbaji wadogo kwa ajili ya kuanza uchimbaji wa makaa; kuendelea kwa majadiliano na mwekezaji; kukamilka kwa upembuzi yakinifu na uchorongaji wa kubaini wingi na ubora wa chuma na makaa ya mawe ambapo kiasi cha tani milioni 126 za chuma na tani milioni 428 za makaa ya mawe zimebainika; kufanyika kwa Tathmini ya athari za mradi kwenye mazingira (Environmental Impact Assessment); Kutolewa kwa Leseni za uchimbaji wa madini ya makaa ya mawe; kuboreshwa kwa barabara ya km 250 kwa kiwango cha changarawe kutoka Itoni (Njombe) kuelekea maeneo ya miradi ya Liganga na Mchuchuma. Kwa sasa kilomita 50 za kipande korofi cha barabara kutoka Lusitu hadi Mawengi kinatengenezwa kwa kiwango cha zege. Kukamilika kwa utekelezaji wa mradi husika utawezesha kupunguza matumizi ya fedha za kigeni ambazo zinatumika katika uagizaji wa malighafi ya chuma na bidhaa zake nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 16.08 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(xii) Kanda Maalumu za Kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo**

**Mradi Na. 4920: Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uhuishaji/urejeaji wa Upembuzi Yakinifu na Mpango Kabambe wa Eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi wa Bagamoyo; na kuendelea na ujenzi wa barabara yenye urefu wa km 3 kwa kiwango cha lami (Asphalt Concrete) katika eneo la Bagamoyo SEZ - Zinga inaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 31. Jumla ya shilingi bilioni 1.13 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(xiii) Mradi Na. 4702: Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi – Kilwa Masoko**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na usanifu wa kina ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 95; uchimbaji wa ujazo wa mita za mraba 1,630 kwa ajili ya kuongeza kina (asilimia 20); uandaaji wa ardhi (Land formation) (asilimia 90); mobilazation (asilimia 100); uchunguzi wa udongo (asilimia 100); uchunguzi wa vina vya maji (asilimia 100; ujenzi wa kambi na ofisi za wafayakazi (asilimia 100); na ujenzi wa nguzo za ghati (asilimia 20). kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 25. Jumla ya shilingi bilioni 40.43 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 28.01 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(xiv) Mradi Na. 3165: Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) – Njombe**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa: Uhuishaji wa upembuzi yakinifu wa mradi na njia za kusafirisha umeme; zoezi la tathmini ya ardhi kwa eneo la mradi; na tathmini ya athari za mazingira na jamii.

**(xv) Mradi Na. 3167: Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222) - Njombe**

Hatua iliyofikiwa ni: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa: Uhuishaji wa upembuzi yakinifu wa mradi na njia za kusafirisha umeme; zoezi la tathmini ya ardhi kwa eneo la mradi; na tathmini ya athari za mazingira na jamii.

### 2.3.2. Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

#### 2.3.2.1. Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma

**(a) Reli**

**(i) Mradi Na. 4213: Mfuko wa Reli**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi wa mabehewa 22 ya abiria kwa ajili ya reli ya MGR; kukamilika kwa ukarabati wa mabehewa 159 ya mizigo na mabehewa 14 ya abiria na kuanza kutoa huduma; kukamilika kwa uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na umeme katika njia ya reli ya MGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza; na kuendelea na uundaji wa vichwa viwili (2) vya treni vya njia kuu aina ya 88U na vichwa saba (7) vya sogeza aina ya 64XX ambapo utekelezaji umefikia asilimia 53; kukamilika kwa ununuzi wa mabehewa ya ubaridi matano (5) mapya ya MGR kwa ajili ya kuhifadhi mbogamboga na matunda; na kuanza ukarabati wa njia ya MGR ya Kaliua – Mpanda (Km 210). Jumla ya shilingi bilioni 187.33 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 100.59 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(ii) Mradi Na. 4211: Uboreshaji wa Reli ya TAZARA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kwa marekebisho ya Sheria ya TAZARA ya mwaka 1995 ili kuiwezesha TAZARA kujiendesha kwa tija zaidi; na kuendelea na taratibu za kumpata mzabuni atakayenunua vitendea kazi kwa ajili ya ukarabati wa reli ya TAZARA.

**(iii) Mradi Na.4216: Ukarabati wa Reli ya Kati ya MGR**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kwa taratibu za kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni za kumpata mkandarasi kwa ajili kufanya ukarabati wa maeneo yaliyosalia katika mradi wa TIRP awamu ya kwanza katika vipande vya njia za reli za Kilosa - Gulwe –Igandu, Kilosa – Mikumi, Isaka - Mwanza, Dar es Salaam - Tabora na Tabora – Isaka ikihusisha ubadilishaji wa njia na ujenzi wa vituo vya kupakia na kupakua mizigo vya Ilala na Isaka.

**(b) Barabara na Madaraja**

**Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi**

**(i) Mradi Na. 4147: Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kipande cha Kidatu – Ifakara (km 68) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87. Jumla ya shilingi bilioni 28.31 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 4149: Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235**)

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Sanzate – Natta (km 40) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40; Tarime – Mugumu (km 86) sehemu ya Mogabiri – Nyamongo km 25 (asilimia 27); na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa kipande cha Natta – Mugumu (km 35). Jumla ya shilingi bilioni 12.69 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 4190: Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda (km 211)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa kipande cha Lusitu – Mawengi (km 50); na kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 8. Jumla ya shilingi bilioni 26.98 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 4193: Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro - Singida (km 460)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Handeni – Kiberashi (km 50) kipande cha Handeni - Mafuleta (km 20) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 18.1 na sehemu ya Mafuleta – Kileguru (km 30) maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 3.62 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 4188: Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni - Mkiwa (km 528)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9) kwa kiwango cha lami sehemu ya Noranga – Itigi (Mlongaji – km 25) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 48; ujenzi wa barabara za Itigi Mjini (km 10) umefikia asilimia 90; na kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi sehemu ya Mlongaji - Mkiwa (km 31.9). Jumla ya shilingi bilioni 20.25 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vi) Mradi Na. 4112: Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kipande cha Chagu – Kazilambwa (km 36) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98; kuendelea kwa ujenzi wa kipande cha

Uvinza – Malagarasi (km 51.1) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 38; na kuendelea na ujenzi wa *Urambo Roundabout* ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85. Jumla ya shilingi bilioni 29.93 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vii) Mradi Na. 4041: Barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) na Daraja la Mnywamaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) sehemu ya Amanimakoro – Ruanda (km 35) na ujenzi wa daraja la Mnywamaji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 24.7; na kuendelea na taratibu za kusaini Mkataba wa ujenzi sehemu ya Luanda – Ndumbi Port (km 50). Jumla ya shilingi bilioni 5.99 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(viii) Mradi Na. 4174: Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na ujenzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji. Jumla ya shilingi bilioni 5.68 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ix) Mradi Na. 4024: Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kipande cha Nanganga – Ruangwa (km 53.0) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70. Aidha, taratibu za manunuzi zinaendelea kwa sehemu ya Ruangwa – Nachingwea (km 55.7). Jumla ya shilingi bilioni 7.87 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(x) Mradi Na. 4101: Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kipande cha Tanga - Pangani (km 50) kwa kiwango cha lami ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70 na barabara ya Pangani – Mkange (km 214.5), sehemu ya Tungamaa – Mkange (km 95.2) utekelezaji umefikia asilimia 21; na kuendelea na ujenzi wa Daraja la Pangani lenye urefu wa mita 525 na barabara unganishi (km 25.6) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 7. Jumla ya shilingi bilioni 32.16 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(xi) Mradi Na. 4014: Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 152)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200) sehemu ya Ntendo – Kizungu (km 25) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30. Jumla ya shilingi bilioni 6.65 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(xii) Mradi Na. 4022: Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi sehemu ya Moronga – Makete (km 53.5) kwa kiwango cha lami; na kuanza ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete (km 50) Sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.3). Jumla ya shilingi bilioni 13.34 zimetumika katika

mwaka 2022/23.

**(xiii) Mradi Na. 4123: Barabara ya Dumila – Kilosa (km 141)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Rudewa - Kilosa (km 24) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 93. Jumla ya shilingi bilioni 8.43 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani**

**(i) Mradi Na. 4124: Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 117)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami sehemu ya Matai – Tatanda (km 25) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30 na sehemu ya Tatanda – Kasesya (km 25) ambapo taratibu za kusaini mkataba wa ujenzi zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 7.78 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 4115: Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai – Kamwanga/ Sanya Juu (km 271)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8) kwa kiwango cha lami ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50.5. Jumla ya shilingi bilioni 14.69 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 4154: Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ya Mpanda – Mishamo – Uvinza Sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 35 na sehemu ya Luhafwe – Mishamo Jct (Bulamata) – km 37.25 taratibu za kusaini mkataba ili kuanza ujenzi zinaendelea; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Sitalike (km 71) sehemu ya Kibaoni – Mlele Jct (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10 na sehemu ya Mlele Jct – Sitalike (km 21) taratibu za manunuzi zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 42.17 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 4141: Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa vipande vya Kisorya - Bulamba (km 51) na Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 20.71 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 4162: Barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 121)**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Maswa (km 11). Jumla ya shilingi bilioni 21.37 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vi) Mradi Na. 4164: Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 341.25**)

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu za Kanyani *Junction* – Mvugwe (km 70.5) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 58, Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35) asilimia 75.3, Kibondo *Junction* – Kabingo (km 62.5) asilimia 84.8 na Nduta Junction – Kibondo (km 25.9) asilimia 84.8. Jumla ya shilingi bilioni 86.09 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vii) Mradi Na. 4128: Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Bugene – Kasulo – Kumunazi & Kyaka – Mutukula (km 124) sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20. Aidha ujenzi wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.10) umekamilika. Jumla ya shilingi bilioni 14.06 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Barabara za Mikoa na Kupunguza Msongamano**

**(a) Mradi Na. 4138: Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 138.5)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi  wa barabara ya Goba – Matosa – Temboni (km 6) ambapo ujenzi wa km 1 umekamilika; na kuendelea kwa usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1). Jumla ya shilingi bilioni 1.90 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4145: Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68)**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu Mjini (spur roads) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 55. Jumla ya shilingi bilioni 42.17 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4132: Barabara za Mikoa (km 1,041.91)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kujengwa kwa jumla ya kilometa 66.18 za barabara za mikoa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa 880.46 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Aidha, utekelezaji wa miradi ya madaraja/makalavati umefikia asilimia 88.82 ambapo madaraja madogo 40 yalijengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na madaraja madogo 26 yalijengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Jumla ya shilingi bilioni 29.49 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4285 Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Dar es Salaam)**

**Awamu ya Pili**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa *Lot 1* inayohusisha barabara zenye

urefu wa km 20.3 (Mbagala - Mzunguko wa Bandari (Bendera Tatu)) – Kariakoo, Barabara ya Kawawa – barabara ya Morogoro (Magomeni), Barabara ya Chang'ombe – Barabara ya Kilwa) ambapo ujenzi umefikia asilimia 98. Jumla ya shilingi bilioni 179.89 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Awamu ya Tatu**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara za Azikiwe na Maktaba, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere hadi Gongo la Mboto zenye jumla ya kilomita 23.6 na kituo kikuu cha mabasi Kariakoo; Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi TAZARA ujenzi umeanza ambapo utekelezaji umefikia asilimia 14. Jumla ya shilingi bilioni 34.75 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4146: Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma**
Hatua iliyofikiwa: Kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya mzunguko (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot 1 & 2 km 112.3), sehemu za barabara ya Nala – Veyula – Mtumba – *Ihumwa Dry Port* (km 52.3) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 48; Ihumwa - Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60) asilimia 40; na Kikombo *Junction* – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) asilimia 30. Jumla ya shilingi bilioni 34.75 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Barabara za Vijijini na Mijini**

**Mradi Na. 4170: Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa matengenezo ya mtandao wa barabara za vijijini na mijini wenye urefu wa km 22,873.47; kukamilika kwa ujenzi wa bararaba kwa kiwango cha lami zenye urefu wa km 204.17 na barabara za changarawe zenye urefu wa km 7,068.89, mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa km 74.08; na ujenzi wa madaraja 218 na makalavati 496.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa matengenezo ya barabara kilomita 1,094, ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 12.6 kwa kiwango cha lami, barabara zenye urefu wa km 464.8 kwa kiwango cha changarawe na kukamilika kwa ujenzi wa makalvati 122. Jumla ya shilingi bilioni 556.8 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 124.5 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**Ujenzi wa Nyumba za Serikali na Madaraja**

**(a) Mradi Na. 4126: Ujenzi wa Madaraja Makubwa**
Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa madaraja makubwa nane (8) ya Tanzanite (DSM), Gerezani (DSM), Mpwapwa (Dodoma), Kiegeya (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Kitengule (Kagera) na Daraja la Msingi (Singida). Jumla ya shilingi bilioni 4.93 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4020: Daraja Jipya la Wami (Pwani)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kuanza kutumika kwa daraja la Wami lenye urefu wa mita 510 na barabara unganishi (km 4.3). Jumla ya shilingi bilioni 21.02 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi Jijini Dodoma na kufanya maandalizi ya kuanza awamu ya II; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 150 (Awamu I) za makazi ya watumishi wa umma katika eneo la Nzuguni Jijini Dodoma na kuendelea na awamu ya II ya ujenzi wa nyumba 150 nyingine ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za majaji katika mikoa ya Kilimanjaro, Tabora, Shinyanga na Mtwara; kuendelea na ujenzi wa nyumba za Watumishi Temeke Kota ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30; na kukamilika kwa ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Awamu ya II "Block" A na ujenzi katika Block B umefikia asilimia 66. Jumla ya shilingi bilioni 18.44 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 6580: Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 5.3 kwa kiwango cha lami na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua kilomita 1.8; na maandalizi ya uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi ikiwemo ununuzi wa watalaam washauri kwa ajili ya usanifu wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 10.43 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Usafiri Majini**

**(i) Mradi Na. 4295: Ujenzi na Ukarabati wa Meli**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa meli ya MV Umoja; kuendelea na ujenzi wa Meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 na ukarabati wa MT Sangara umefikia asilimia 90.7; kukamilisha taratibu za kupata mkandarasi na kusaini mkataba wa ujenzi wa meli ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 na meli ya abiria na mizigo yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo na Chelezo zitakazojengwa katika Ziwa Tanganyika na meli moja (1) ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo itakayojengwa katika Ziwa Victoria; kukamilika kwa taratibu za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ukarabati wa meli ya MV. Liemba; na kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa mhandisi mshauri kwa ajili kufanya tathmini ya kina kuhusu ukarabati wa meli ya MV. Mwongozo. Jumla ya shilingi bilioni 23.20 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 8.57 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(ii) Mradi Na. 4201: Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi wa Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Uratibu wa Masuala ya Utafutaji na Uokozi katika Ziwa Victoria (Maritime

Rescue Cordination Centre - MRCC, Mwanza); kukamilika kwa malipo ya awali kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vidogo vitatu (3) vya Utafutaji na Uokozi (Search and Rescue-SARs) katika Ziwa Victoria kwenye eneo la Kanyara - Geita, Ukerewe na Musoma; na kuendelea na taratibu za kumpata mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa boti moja (1) ya matibabu (Ambulance Boat) na boti mbili (2) za utafutaji na uokozi. Jumla ya shilingi bilioni 1.93 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 423.26 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(i) Vivuko**

**(a) Mradi Na. 4125*:* Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya jengo la abiria na ofisi na uzio katika eneo la Kinesi (Mwigobero) ambapo ujenzi umefikia asilimia 35; ujenzi wa maegesho ya Kayenze – Kanyinya umefikia asilimia 50; ujenzi wa maegesho mapya ya Ijinga – Kahangala (Magu) umefikia asilimia 40, ujenzi wa maegesho ya Kajunjumele – Mwaya umefikia asilimia 95 na ujenzi wa maegesho ya Kikove – Ngoheranga umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi bilioni 1.79 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4139: Ujenzi wa Vivuko Vipya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kivuko kipya cha Kisorya – Rugezi ambapo ujenzi umefikia asilimia 64; ujenzi wa vivuko vya Ijinga – Kahangala (Magu) asilimia 60, Bwiro – Bukondo (Ukerewe) asilimia 61, Nyakarilo – Kome (Buchosa) asilimia 55, na ujenzi wa kivuko kipya cha pili kitakachotoa huduma kati ya Nyamisati – Mafia (Pwani) umefikia asilimia 10. Jumla ya shilingi bilioni 17.07 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4144*:* Ukarabati wa Vivuko**

Hatua iliyofikiwa: Kukamilika kwa Ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Kazi, MV Ujenzi, MV Misungwi, MV TEMESA na MV Tanga; na kuendelea na ukarabati wa vivuko, MV Nyerere (asilimia 75), MV Kilombero (asilimia 79), MV Mara (asilimia 87), MV Kitunda (asilimia 60), MV Kyanyabasa (asilimia 60) na ukarabati wa kivuko cha MV Magogoni unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10. Jumla ya shilingi bilioni 5.66 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Bandari**

**(a) Mradi Na. 4227: Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam**

**(i) Bandari ya Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na uchimbaji na upanuzi wa lango la kuingilia na kugeuzia meli hadi kufikia kina cha mita 15.5 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99.6; kuendelea na ukamilishaji wa upembuzi yakinifu wa kuimarisha Gati Na. 8 – 11 ambao umefikia asilimia 90; na kukamilika kwa taratibu za kumpata mkandarasi kwa

ajili ya kuboresha mtandao wa reli ndani ya Bandari ya Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 89.32 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 37.11 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(ii) Bandari ya Tanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uboreshaji wa Bandari ya Tanga unaohusisha kazi ya kuongeza kina kutoka kina cha maji cha mita tatu (3) hadi mita 13 na kuboresha Gati Na. 1 - 2 zenye urefu wa mita 450. Jumla ya shilingi bilioni 185.92 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 46.48 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(iii) Bandari Kavu ya Kwala katika Eneo la Ruvu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuunganishwa kwa Mkongo wa Taifa kwenye eneo la mradi; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba tatu (3) za makazi, ofisi na ufungaji wa umeme; kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro hadi Vigwaza/Kwala; na kuendelea na ujenzi wa yadi na sakafu ngumu (pavement) yenye ukubwa wa hekta tano (5) kwa ajili ya kuhifadhi shehena za mizigo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96; Jumla ya shilingi bilioni 48.84 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi shilingi bilioni 6.06 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(b) Bandari za Maziwa Makuu**

**(i) Bandari za Ziwa Victoria**

Kuendelea na hatua za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mwanza South; kuendelea na uboreshaji wa Bandari ya Mwanza North ambapo mkandarasi anafanya maandalizi ya awali; na kuendelea na ukarabati wa Bandari ya Bukoba ambapo utekelezaji umefikia asilimia 16 na bandari ya Kemondo Bay ambapo utekelezaji umefikia asilimia 14. Jumla ya shilingi bilioni 7.04 zimetumika katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(ii) Bandari za Ziwa Tanganyika**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Gati katika Bandari mpya ya Karema; kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Bandari ya Kigoma; na kuendelea na ujenzi wa Bandari ya Kibirizi na Ujiji unaohusisha ujenzi wa Gati, majengo ya abiria, maghala ya mizigo, minara ya matanki ya maji, ofisi ya meneja wa Bandari, uzio na nyumba ya mlinzi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 94. Jumla ya shilingi bilioni 53.40 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 13.35 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(iii) Bandari Ziwa Nyasa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari ya Kiwira na Itungi; kukamilika kwa ujenzi wa gati, ghala la kuhifadhia makaa ya mawe, jengo

la abiria, ofisi na sehemu ya kuegesha meli (ramp) katika Bandari ya Ndumbi; na kuendelea kwa taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay. Jumla ya shilingi bilioni 7.27 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 1.67 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(e) Usafiri wa Anga**

**Mradi Na. 6267: Mradi wa Uwezeshaji wa Taasisi**

**(i) Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (JNIA TB III) na Kuboresha Huduma katika Viwanja vya Ndege**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa uzio wa usalama katika Kiwanja cha Dodoma; kukamilika kwa usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Dodoma; kukamilika kwa malipo ya ununuzi wa gari la zimamoto; kukamilika kwa uboreshaji wa uzio wa usalama wa Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere pamoja na kufunga mfumo ya ufuatiliaji wa mwenendo wa shughuli za kiusalama na uendeshaji (CCTV) katika eneo linalozunguka barabara ya kutua na kuruka ndege (Runway 05); kukamilika kwa ulipaji wa malipo ya fidia kwa wakazi waliopisha upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Dodoma; na kuendelea na hatua za usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Bukoba. Jumla ya shilingi bilioni 25.92 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 3.72 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(ii) Ununuzi wa Mtambo wa Kufundishia - Chuo cha Bahari Dar es Salaam - DMI**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa malipo ya awali ya mtambo (full mission crane simulator) wa kufundishia ili kuongeza ubora na umahiri katika kuhudumia mizigo kwenye meli na vyombo vingine vya usafirishaji. Jumla ya shilingi milioni 275.41 zimetumika mwaka 2022/23.

**(a) Mradi Na. 4290: Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ufungaji wa rada mbili (2) za hali ya hewa katika mikoa ya Mbeya na Kigoma; kukamilika kwa ukarabati wa Ofisi za hali ya hewa za Mahenge na Songea pamoja na nyumba tatu (3) za wafanyakazi zilizopo Mahenge; kukamilika kwa ununuzi na ufungaji wa vifaa mbalimbali vya hali ya hewa ikiwemo seti tano (5) za vifaa vya utambuzi wa matukio ya radi vilivyofungwa Musoma, Mwanza, Bukoba, Tabora na Kibondo pamoja na vifaa vya kupima hali joto vilivyofungwa katika Kituo cha hali ya hewa kilichopo Singida; kukamilika kwa ununuzi na ufungaji wa kompyuta maalumu "*Cluster Computer*" yenye uwezo mkubwa wa kuchakata taarifa za hali ya hewa iliyofungwa katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (JNIA); kukamilika kwa ukarabati wa ofisi ya hali ya hewa katika Kiwanja cha Ndege cha Songea; kuendelea na matengenezo ya rada mbili (2)

zitakazofungwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75; kuendelea na ukarabati wa karakana ya kutengeneza vifaa vya hali ya hewa katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha JNIA na kituo cha Rada ya hali ya hewa cha Dar es Salaam (Bangulo) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; na kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki na Kituo cha Tahadhari ya Matukio ya Tsunami Jijini Dar es Salaam ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30. Jumla ya shilingi bilioni 11.94 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 483.91 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(b) Mradi Na. 4298: Ununuzi na Usimikaji wa Mitambo ya mawasiliano ya sauti baina ya Mwongoza Ndege na Marubani**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi wa mitambo ya mawasiliano ya sauti; kuendelea na usimikaji na majaribio katika viwanja 12 vya ndege vya JNIA, KIA, Abeid Aman Karume Internanational Airport, Tanga, Arusha, Pemba, Mtwara, Dodoma, Mwanza, Tabora, Kigoma na Songwe; na kuendelea na hatua za maandalizi za ununuzi na usimikaji wa mitambo ya mawasiliano katika Anga la juu (VHF Relays Station) katika vituo 18 vya mawasiliano ya Mwongoza Ndege na Marubani. Jumla ya shilingi bilioni 10.35 zimetumika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 6377: Kuboresha Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia**

**(i) Chuo cha Taifa cha Usafirishaji - NIT**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi wa ndege mbili (2) zenye injini moja (1) kwa ajili ya kufundishia marubani, kifaa maalum (Full Motion Cabin Crew Mock-up) kwa ajili ya mafunzo ya wahudumu ndani ya ndege; kuendelea na ujenzi wa maktaba ambapo utekelezaji umefikia asilimia 45; na kufanyika kwa malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa ndege moja (1) yenye injini mbili (2) kwa ajili ya kufundishia marubani. Jumla ya shilingi bilioni 2.50 zimetumika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4209: Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa usanifu wa jengo la abiria na kuendelea na taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi. Jumla ya shilingi bilioni 27.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4220: Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upanuzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara za viungio, maegesho ya ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari. Jumla ya shilingi bilioni 9.73 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 4206: Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kuruka na kutua ndege, ufungaji wa taa za kuongozea ndege na uzio wa usalama; na

kuendelea kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria pamoja na ufungaji wa mifumo na vifaa vyake ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98. Jumla ya shilingi bilioni 4.66 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 4226: Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Geita; kukamilika kwa kazi za upanuzi na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Songea; kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa Wananchi waliopisha upanuzi na ukarabati wa Viwanja vya ndege vya Lake Manyara na Tanga; na kuendelea na upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Iringa (asilimia 60), Moshi (asilimia 50) na Musoma (asilimia 50). Jumla ya shilingi bilioni 18.53 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 699.99 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(h) Mradi Na. 4286: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi awamu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara ya viungio, maegesho ya ndege, pamoja na usimikaji wa taa za usalama na kuongozea ndege ambapo utekelezaji umefikia asilimia 34.72. Aidha, kwa upande wa awamu ya pili inayohusisha ujenzi wa Jengo la Abiria, Jengo la kuongozea Ndege, Kituo cha Zimamoto, Kituo cha Hali ya Hewa na Vituo vidogo nane (8) vya kufua umeme utekelezaji umefikia asilimia 6.15. Jumla ya shilingi bilioni 51.44 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 4221: Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Jumla ya shilingi milioni 29.14 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(j) Mradi Na. 4222: Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege ambapo utekelezaji ni asilimia 10. Jumla ya shilingi bilioni 7.96 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(k) Mradi Na. 4156: Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

Hatua iliyofikiwa ni: kuanza kwa ujenzi wa maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami, ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Jumla ya shilingi milioni 74.56 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(l) Mradi Na. 4159: Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa jengo jipya la abiria, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama na jengo la kuongezea ndege ambapo utekelezaji ni asilimia 5.5. Jumla ya shilingi bilioni 4.67 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(f) Nishati**

**Miradi ya Kufua umeme**

**(i) Mradi Na. 3164: Kinyerezi I *Extension* (MW 185)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa mradi ambapo mitambo minne (GT5, GT6, GT7 na GT8) inazalisha Megawati 185 na kuingizwa katika Gridi ya Taifa. Jumla ya shilingi bilioni 59.19 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 3169: Kufua Umeme wa Maji Rusumo (MW 80)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa bwawa, handaki la kupitishia maji, kituo cha kupoza na kuchochea umeme (switchyard), jengo la utawala na nyumba 24 za kudumu; kuendelea na ujenzi wa jengo la mitambo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.89 na ufungaji wa mitambo ya kufua umeme asilimia 97. Kwa ujumla mradi umefikia asilimia 99.7. Jumla ya shilingi bilioni 15.71 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme**

**(i) Mradi Na. 3111: Uimarishaji wa Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization)***

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kV132 kutoka Ilala hadi Kurasini kwa kutumia nyaya za ardhini ambapo utekelezaji umefikia asilimia 38; kuendelea na ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa njia ya kusafirisha umeme kV132 kutoka Ubungo – Chalinze – Hale (269km) ambapo sehemu ya Ubungo – Chalinze (97km) imekamilika; kuendelea na ujenzi wa mradi wa maboresho ya njia ya kusafirisha umeme kV132 kutoka Kinyerezi–Gongolamboto – Mbagala (19.7km) na kituo cha kupoza umeme cha Gongolamboto na Mbagala ambapo utekelezaji umefikia asilimia 43.75; na kuendelea na ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 33 (60km) kutoka Nyakanazi – Kakonko na Nyakanazi – Lusahunga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99.

Aidha, kuendelea na uboreshaji wa njia ya kusafirisha umeme kutoka msongo wa kV132 hadi kV220 kwa njia ya Ubungo – Kunduchi – Ununio urefu wa kilomita 18.2 pamoja na kituo cha kupoza umeme cha Ununio chenye uwezo wa 2x120MVA, 220/132/33kV unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 18; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa njia ndogo nane (8) za umeme 33kV kutoka kituo cha

kupoza umeme cha Lemugur (Arusha) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 22.5; kuendelea na ujenzi wa mradi wa vituo vya kupoza umeme wa msongo wa kilovoti 132/33, 35MVA/15MVA vya Mpanda, Ipole, Inyonga, Tabora, Urambo na Nguruka ambapo utekelezaji umefikia asilimia 33; kuendelea na ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132kV kutoka Tabora – Urambo (115km) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10; na kuendelea na ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirishisha umeme wa msongo wa kilovoti 132kV kutoka Tabora – Katavi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 31.5. Jumla ya shilingi bilioni 90.9 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 105.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(ii) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 (Rusumo – Nyakanazi)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 (Rusumo – Nyakanazi) na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi. Jumla ya shilingi bilioni 8.2 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 3175: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Singida hadi Arusha; kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Arusha hadi Namanga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98; kuendelea na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Lemugur katika eneo la Kisongo mkoani Arusha ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; na kukamilika kwa usambazaji wa umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 98.5. Jumla ya shilingi bilioni 55.6 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 180.20 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(iv) Mradi Na. 3179: Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Rufiji – Chalinze – Kinyerezi – Dodoma**

**Awamu ya kwanza (Rufiji – Chalinze)**: Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99; na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Chalinze (kV400/220/132) umefikia asilimia 84.3. Jumla ya shilingi bilioni 90.82 mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 13.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**Awamu ya pili (Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi)**: Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ulipaji fidia kwa waguswa kwa sehemu ya Kinyerezi–Chalinze ambapo waguswa 991 kati ya 1,237 sawa na asilimia 80.11 wameshalipwa kiasi cha shilingi bilioni 8.6 na waguswa 2,565 kati ya 2,889 sawa na asilimia 88.79 kwa sehemu ya Chalinze–Dodoma wameshalipwa shilingi bilioni 9.42; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii. Jumla ya shilingi bilioni 18.02 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 3166: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 - North West Grid Extension (Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi)**

**Awamu ya Kwanza: Iringa – Mbeya – Tunduma–Sumbawanga (TAZA)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa taarifa za tathmini (evaluation reports) za zabuni za wakandarasi wajenzi wa mradi ambapo taratibu za kupata kibali (No Objection) kutoka kwa wafadhili zinaendelea; na kuendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi 6,500 wanaopisha mradi ambapo wananchi 4,705 washamelipwa. Jumla ya shilingi bilioni 16.43 zimetumika kulipa fidia katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 781.49 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**Awamu ya Pili: Kigoma – Nyakanazi**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme; kuendelea na zoezi la ulipaji wa fidia katika eneo la Kidahwe na eneo la mkuza wa njia ya usafirishaji umeme ambapo wananchi 2,910 kati ya 3,220 wamelipwa sawa na asilimia 90.4; kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ambapo utekelezaji umefikia asilimia 66. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 67. Jumla ya shilingi bilioni 25.3 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vi) Mradi Na. 3113: Usambazaji wa Nishati ya Umeme Vijijini**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuunganishwa kwa jumla ya vijiji 10,987 kati ya vijiji 12,318 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 89.19; kusambazwa umeme katika vitongoji 28,659 kati ya 64,760 sawa na asilimia 44.25; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji na kusambaza kupitia waendelezaji binafsi wa Ikondo-Matembwe (Makete, Njombe) na Mwenga (Mufindi, Iringa) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi bilioni 676.8 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 92.57 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**Miradi ya Usambazaji wa Gesi Asilia**

**(i) Mradi Na. 3162: Usambazaji wa Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi katika kiwanda cha Sapphire Float Glass Ltd (Dar es Salaam); kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi asilia katika kiwanda cha KEDA Ceramics Tanzania Co. Ltd (Pwani); kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kupunguza msukumo wa gesi *(*Lindi*)*; kuunganishwa kwa nyumba 209 katika mtandao wa miundombinu ya gesi asilia (Lindi); kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha CNG cha DANGOTE kilichopo Mkuranga; kuendelea na ujenzi wa kituo cha CNG (Dar es Salaam) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70; kuendelea na ujenzi wa bomba la usambazaji wa gesi asilia la Mwenge – Mbezi Beach (km 12.4) ambapo utekelezaji umefikia asilimia

99; na kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kusambazia gesi asilia katika makazi 980 yaliyopo katika mkuza wa Bomba la Gesi asilia katika Mikoa ya Pwani na Lindi. Jumla ya Shilingi bilioni 8.01 zimetumika katika mwaka 2022/23 na Shilingi milioni 332.28 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

#### 2.3.2.2. Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi

#### A. Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge

**(i) Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa makazi ya Katibu wa Bunge katika eneo la kilimani - Dodoma; kuendelea na ujenzi wa nyumba mbili (2) za viongozi wa Bunge katika eneo la Kilimani ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85.7; kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ununuzi na usimikaji wa mitambo mipya ya ulinzi na usalama; na kuendelea na hatua za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa makumbusho ya Bunge. Jumla ya shilingi bilioni 4.49 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 945 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(ii) Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la utawala, ukumbi wa Msekwa, na ukumbi mkubwa wa Bunge; kuanza kwa ujenzi wa kisima na tenki kwa ajili ya kuhifadhia maji katika jengo dogo la utawala ili kukabiliana na majanga ya moto. Jumla ya shilingi milioni 471.20 zimetumika katika mwaka 2022/23.

#### B. Kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika Utumishi wa Umma

**Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**(i) Mradi Na. 6315: Ujenzi wa Makazi ya Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba ya makazi ya Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John P. Magufuli; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba ya makazi ya Rais wa Awamu ya Kwanza Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere; na kuendelea na ujenzi wa Klabu ya Viongozi - Makao Makuu eneo la Nzuguni ambapo ujenzi wa uzio umefikia asilimia 65. Jumla ya shilingi bilioni 6.43 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6284: Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa Mfumo wa Utendaji Kazi kwa mtumishi (PEPMIS) na kwa taasisi (PIPMIS), Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) na Mfumo wa Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi wa Umma (e-HRP); kuboreshwa kwa moduli ya Watumishi Portal yenye huduma za kielektroniki za

uhamisho wa watumishi, mikopo ya watumishi, taarifa binafsi za mtumishi na hati ya malipo ya mishahara; kuibuliwa na kuboreshwa kwa mifumo mipya ikiwemo mifumo ya e-Mrejesho, e-Mikutano, e-Rufaa, e-Dodoso pamoja na Shared Helpdesk; na usanifu na ujenzi wa Mfumo maalum wa kuwezesha mifumo ya Serikali kusomana na kubadilishana taarifa (Government Enterprise Service Bus, GovESB) ambapo mifumo 62 ya taasisi 54 imewezeshwa kuwasiliana na kubadilishana taarifa kupitia (GovESB). Jumla ya shilingi bilioni 4.2 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**C. Mfuko wa Mahakama**

**(i) Mradi Na. 6310: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Wilaya**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama ya wilaya ya Manyoni; na kuendelea na ujenzi wa Mahakama za wilaya za Liwale ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99, Kwimba (asilimia 99) na Ulanga (asilimia 86). Miradi mingine inayotekelezwa ni ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Ubungo (asilimia 80) na Korogwe (asilimia 52); na ukarabati wa jengo la Mahakama ya Wilaya Maswa (asilimia 70). Jumla ya shilingi bilioni 6.3 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 158.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24 .

**(ii) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 37; na ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) kwa ajili ya makazi ya Majaji Jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87.5. Jumla ya shilingi billioni 3.8 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 6312: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo tisa (9) ambapo Mahakama ya Mwanzo Madale - Kinondoni utekelezaji umefikia asilimia 75, Kinesi - Rorya (asilimia 99), Mahenge - Kilolo (asilimia 99), Luilo – Ludewa (asilimia 99), Newala – Newala (asilimia 85); Usevya – Mlele (asilimia 99); Nyakibimbili - Bukoba (asilimia 99), Kabanga–Ngara (asilimia 90); Mlimba Kilombero (asilimia 70) na Mang'ula – Kilombero (asilimia 95). Jumla ya shilingi bilioni 4.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 6314: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama Kuu**
Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu Tabora na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi (Dar es Salaam); na kuendelea na ukarabati wa jengo la zamani la Mahakama Kuu Dodoma (asilimia 29). Jumla ya shilingi bilioni 1.7 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 235.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(v) Mradi Na. 6215: Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Mahakama (Citizen Centric Judiciary Modernisation Project)**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama za wilaya 18 ambapo jumla ya shilingi bilioni 17.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**D. Utawala Bora na Utawala wa Sheria**

**(a) Mradi Na. 5501: Kuimarisha Upatikanaji wa Haki za Binadamu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwajengewa uwezo kwa watumishi 45 wa Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu uratibu na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mikataba ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza haki za binadamu nchini; na kukamilika kwa rasimu ya Mpango Kazi wa pili wa kitaifa wa kulinda haki za binadamu nchini kwa kupata maoni ya pande zote mbili za Muungano wa Tanzania. Jumla ya shilingi milioni 78 zimetumika katika kipindi cha mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 5502: Mpango Kazi Endelevu wa Kupambana na Rushwa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaa rufaa sita (6) za malalamiko ya wananchi yenye viashiria vya rushwa na kuviwasilisha TAKUKURU; kushughulikiwa kwa mashauri 15 ya rushwa kubwa katika mahakama ya rushwa na uhujumu uchumi; kukamilika kwa mapitio ya majalada 55 ya kesi za rushwa kwa ajili kuwajengea uwezo Waendesha Mashtaka Wafawidhi wa Mikoa mitano (5) ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya na Mwanza.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa mfumo wa usimamizi wa taarifa unaoshughulikia mikataba, malalamiko na kesi ambao upo katika hatua ya majaribio; na ujenzi wa mfumo wa mawasiliano wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi kidijitali (contact centre) upo katika hatua ya majaribio**.** Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 5507: Upatikanaji wa Haki za Wanawake na Watoto wa Kike**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwajengea uwezo viongozi wa Serikali za Mitaa 280 na watoa huduma ya msaada wa kisheria 40 kuhusu haki za wanawake na watoto wa kike, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, elimu ya kisheria, mirathi, ndoa, na taratibu za upatikanaji wa haki na wajibu kwa mujibu wa sheria katika mikoa minne (4) ya Dodoma, Manyara, Shinyanga na Ruvuma. Jumla ya shilingi milioni 135 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 5508: Upatikanaji wa Haki kwa Maendeleo Endelevu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa maandalizi ya mahitaji ya mfumo wa kubadilishana taarifa miongoni mwa Taasisi za Haki Jinai; kukamilika kwa andiko la kutungwa kwa Sera ya Adhabu; kununuliwa kwa magari mawili (2) ya kufuatilia huduma za utoaji haki nchini; na kuwezesha utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Huduma za Msaada wa kisheria ijulikanayo “Mama Samia Legal Aid Campaign”

katika halmashauri zote za mikoa ya Dodoma, Manyara, Shinyanga na Ruvuma. Jumla ya shilingi bilioni 2.11 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 6201: Haki Mtandao**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwajengea uwezo washiriki 65 ambao ni watoa huduma za msaada wa kisheria, wasaidizi wa kisheria, wasajili wasaidizi, na madawati ya huduma za kisheria kwenye magereza na Polisi kuhusu mifumo ya kidijitali ya utoaji wa huduma za kisheria chini ya Wizara ya Katiba na Sheria; kukamilisha mpango wa mawasiliano ya huduma zinazotolewa na Wizara kwa wananchi; kupatikana kwa vitendea kazi vya TEHAMA kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za kisheria kidijitali kwa Wizara, Taasisi ya Isanga na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Jumla ya shilingi milioni 830.7 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 6207: Kuboresha Uwajibikaji wa Kitaasisi katika Kupambana na Rushwa na Kuongeza wigo wa kuifikia Haki**

Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa ukaguzi kwa Taasisi 34 za Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria kutoka wilaya 27 za mikoa tisa (9) ya Tanzania Bara; kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa mahabusu na wafungwa kwa njia ya huduma ya msadaa wa kisheria inayotolewa na mawakili bila malipo (Pro Bono) katika magereza ya Segerea na ukonga ambapo jumla ya wafungwa 56 walipatiwa huduma; kuwajengea uwezo viongozi wa kimila na kidini kuhusu utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala; kuwajengea uwezo viongozi wa Serikali za mitaa kuhusu utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala, ukatili wa kijinsia na haki za wanawake. Jumla ya shilingi milioni 400 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 1.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(g) Mradi Na. 6517: Haki ya Mtoto**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Haki Mtoto; kukamilisha kukusanya maoni ya wananchi kuhusu maboresho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971; kusajili jumla ya watoto 426,307 wenye umri chini ya miaka mitano (5) katika mikoa 23 ya Tanzania Bara inayotekeleza mpango huo; Kukamilisha kuboresha mfumo wa utoaji Haki – Jinai kwa Watoto; kufanya ukaguzi wa watoto wanaokinzana na sheria katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na mikoa mitatu (3) ya Kimashtaka ambayo ni Temeke, Kinondoni na Ilala. Jumla ya shilingi bilioni 5.29 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

**(i) Ofisi na Makazi ya Viongozi wa Mikoa na Wilaya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Ikulu ndogo mbili (2) katika mkoa wa Dodoma; kuendelea na ujenzi wa Ikulu Ndogo nne (4) na ukarabati wa Ikulu Ndogo nne (4) za Wilaya; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba nne (4) za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya na kuendelea na ujenzi wa nyumba nane (8) za Makatibu

Tawala wa Mikoa na Wilaya; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba moja (1) na ukarabati wa nyumba moja (1) za Wakuu wa Wilaya; kuendelea na ujenzi wa nyumba sita (6) na ukarabati wa nyumba nane (8) za Wakuu wa Wilaya; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba moja (1) na ukarabati wa nyumba moja (1) za Wakuu wa Mikoa; kuendelea na ujenzi wa nyumba moja (1) na ukarabati wa nyumba mbili (2) za Wakuu wa Mikoa; kukamilika kwa nyumba tisa (9) za Maafisa Tarafa na kuendelea na ukamilishaji wa nyumba nane (8) za Maafisa Tarafa.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni: kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya nne (4); na kuendelea na ujenzi wa ofisi 14 za Wakuu wa Wilaya na ukarabati 15 za Wakuu wa Wilaya; kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi moja (1) ya Mkuu wa Mkoa na ukarabati wa Ofisi mbili (2) za Wakuu wa Mikoa; kuendelea na ujenzi wa ofisi sita (6) za Wakuu wa Mikoa; kuendelea na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa; kukamilika kwa ujenzi wa ofisi 15 za Makatibu Tarafa. Aidha, ujenzi wa jengo jipya la Soko la kisasa la Kariakoo na ukarabati wa jengo la zamani unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 91. Jumla ya shilingi bilioni 62.3 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 22.24 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/34.

**(ii) Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Majengo ya Huduma Jumuishi za Sheria yanayojengwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika mikoa miwili (2) ya Kimashtaka ya Ilala (Kinyerezi) na Pwani; kuendelea na ujenzi wa majengo ya Huduma Jumuishi za Sheria katika mikoa ya Kimashtaka ya Morogoro (asilimia 75), Mbeya (asilimia 76), Shinyanga (asilimia 68), Manyara (asilimia 70), Njombe (asilimia 30), Katavi (asilimia 30), Rukwa (asilimia 30) na Geita (asilimia 30); na kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu Dodoma (asilimia 29.6). Jumla ya shilingi bilioni 14.66 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la Huduma Jumuishi za Sheria la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jijini Mwanza (asilimia 80) na Arusha (asilimia 10). Jumla ya shilingi bilioni 1.78 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(iv) Ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na Awamu ya Pili ya ujenzi wa majengo katika mji wa Serikali Mtumba ambapo ujenzi wa majengo 29 ya wizara (26) na Taasisi (3) umefikia wastani wa asilimia 67.8; kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya awali katika Mji wa Serikali Mtumba ikiwemo ya maji, umeme, mawasiliano na barabara zenye urefu wa km 51.2 kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 351.41 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 34.77 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(v) Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama Dodoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Makao Makuu Jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asimilia 94. Jumla ya shilingi bilioni 17.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vi) Ofisi na Makazi ya Viongozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa majengo 12 kati ya majengo 49 muda mrefu ya Halmashauri; kukamilika kwa majengo mawili (2) ya Halmashauri za Wilaya za Tanganyika na Iringa kati ya majengo 30 mapya ya utawala; na ujenzi wa nyumba 46 za wakurugenzi ambapo nyumba 11 zimekamilika na nyumba 78 za wakuu wa idara ambapo nyumba nane (8) zimekamilika. Jumla ya shilingi bilioni 93.06 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 32.18 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/34.

**(i) Mradi Na. 6209: Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo kusaidia ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, masoko ya kijiji, vyumba vya madarasa na vyumba vya maabara. Jumla ya shilingi bilioni 15.99 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**E. Mradi Na. 6501: Vitambulisho vya Taifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kusajiliwa na kutambuliwa kwa watu 898,204 kati yao wageni ni 2,516 na wakimbizi ni 95 na kufanya jumla ya watu waliosajiliwa kufikia 24,083,933 ambapo namba za utambulisho wa Taifa (NIN) zilizozalishwa zimefikia 20,222,032. katika Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara na Zanzibar; kununuliwa kwa kadi ghafi milioni 8.5 kwa ajili ya kuzalisha vitambulisho vya Taifa; kuzalishwa na kusambazwa kwa vitambulisho 1,849,931 kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa kufikia 12,863,269; kuunganishwa na kuboreshwa kwa mifumo na miundombinu ya mtandao wa mawasiliano kati ya Ofisi za Usajili za Wilaya na Makao Makuu ambapo ofisi mbili (2) zimeunganishwa na kufanya jumla ya ofisi zilizounganishwa kufikia 144; kuunganishwa kwa Taasisi 7 katika mfumo wa Usajili na Utambuzi na kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa na mfumo kufikia 76. Jumla ya shilingi billion 49.1 zimetumika katika kipindi cha mwaka 2022/23.

**F. Usalama wa Raia**

**(i) Mradi Na. 6302: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Tanzania Bara**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa vituo vitano (5) vya Polisi vya Daraja “A”, viwili (2) Daraja “B” na viwili (2) Daraja ‘C’; kuendelea na ujenzi wa kituo cha Polisi Daraja “A” katika Mji wa Serikali Mtumba Dodoma (asilimia 90), Ikungi (asilimia 75) na Lindi (asilimia 90); kituo cha Polisi Daraja "B" Mkarama Singida (asilimia 75), Namtumbo (asilimia 30), Siha (asilimia 75), Mara (asilimia 40) na Chemba (asilimia 60); Daraja ”C” na ujenzi wa nyumba za makazi ya askari Ludewa ambapo

utekelezaji umefikia asilimia 98, Mbande Temeke (asilimia 80), Chang'ombe Dodoma (asilimia 50) na Songambele Urambo (asilimia 40); ujenzi wa ofisi za makamanda wa Polisi za Mikoa ya Mara (asilimia 95), Katavi (asilimia 75), Njombe (asilimia 60) na ujenzi wa nyumba 3 za kuishi Makamishna wa Polisi Jijini Dodoma umefikia (asilimia 99); na majengo manne (4) ya ghorofa nne (4) katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam (asilimia 83). Jumla ya shilingi bilioni 13 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6303: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Zanzibar**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kituo cha Polisi Kizimkazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65; kuendelea na ukarabati wa jengo la Kilimanjaro Ziwani Mjini Magharibi (asilimia 80), bweni la kuishi Askari Bububu Mjini Magharibi (asilimia 99), Jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Mjini Magharibi (asilimia 30), nyumba 3 za ghorofa za makazi ya familia 12 Askari zilizopo Mwera Mjini Magharibi (asilimia 70); Ujenzi wa nyumba ya kuishi Kamishna wa Polisi Zanzibar (asilimia 30); Ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja "C" Dunga Mjini Kusini Unguja (asilimia 98); Ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja "B" (asilimia 30). Jumla ya shilingi bilioni 2.4 zimetumika katika mwaka 2022/23.

### G. Uhamiaji

**Mradi Na. 6301: Ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Uhamiaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kukabidhiwa kwa Ofisi ya uhamiaji ya Mkoa katika mikoa ya Geita, Manyara na Lindi; kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75 na Ofisi ya Makao Makuu ya Uhamiaji Dodoma (asilimia 53); kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Uhamiaji cha Raphael Kubaga kilichopo Boma Kichakamiba Wilayani Mkinga (Tanga) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 94. Jumla ya shilingi bilioni 5.70 zimetumika katika kipindi cha mwaka 2022/23.

### H. Huduma za Zimamoto na Uokoaji

**Mradi Na. 6582: Upanuzi wa Huduma za Zimamoto na Uokoaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa magari matatu (3) ya zima moto na uokoaji; kuendelea na ujenzi wa nyumba sita (6) zenye uwezo wa kuhudumia familia 60 za Askari Kikombo - Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 68.3 na chumba maalumu katika mkoa wa Ilala (asilimia 79.2). Jumla ya shilingi bilioni 6.4 zimetumika katika kipindi cha mwaka 2022/23.

### I. Magereza

**(i) Mradi Na. 6103: Mipango ya Ulinzi na Usalama Magerezani**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi na ufungaji wa CCTV - Camera katika magereza matano (5). Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na.6305: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa magereza sita (6) katika Wilaya ya Kilosa (asilimia 70) na Gairo – Morogoro (asilimia 40), Kakonko – Kigoma (asilimia 50), Kaliua – Tabora (asilimia 40), Karatu – Arusha (asilimia 70), Msalato – Dodoma (asilimia 60), Hospitali ya Jeshi eneo la Msalato kwa kujenga jengo la wagonjwa wa nje - OPD (asilimia 70), jengo la Mama na mtoto (asilimia 45), jengo la Maabara (asilimia 45) na jengo la Power House (asilimia 70). Jumla ya shilingi bilioni 3.13 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 4428: Uimarishaji wa Mashamba ya Magereza**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la magereza Idete – Morogoro ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80. Jumla ya shilingi milioni 785 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 4491: Kuboresha Upatikanaji wa Maji safi Magerezani**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa visima 13 katika magereza ya Kwitanga – Kigoma, Ruanda – Mbeya, Malya – Simiyu, Pawaga – Iringa, King'ang'a – Dodoma, Mugumu – Mara, Mwanga – Kilimanjaro, Ubena – Pwani, Kitete – Rukwa, Kasulu – Kigoma, Kiomboi – Singida, Mang'ola – Arusha, Wazo Hill - Dar es Salaam. Jumla ya shilingi milioni 747 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**2.3.2.3. Mapinduzi ya TEHAMA**

**A. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

**(i) Mradi Na. 4283: Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mikongo ya mwisho (last mile connectivity) kwenye taasisi 200 za kimkakati; kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa mkongo wa majini km 60 ili kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia ziwa Tanganyika; kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Taifa cha kutunzia taarifa (data) - Zanzibar; kukamilika kwa ununuzi wa mitambo kwa ajili ya vituo 112 vya kutolea huduma ambapo usimikaji umefanyika kwenye vituo 61 vya kutolea huduma; kukamilika kwa usimikaji wa nguzo 10,624 zitakazotumika kujenga mkongo wa juu kwenye maeneo mbalimbali ya njia za mkongo; na kujengwa kwa km 1,663 za njia mpya za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Utekelezaji huu umewezesha Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kufikia kilomita 8,319 na kuunganishwa kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali (MDAs) 235 pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) 77. Jumla ya shilingi bilioni 65.56 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 30.78 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(ii) Mradi Na. 4234: Mfumo wa Anwani za Makazi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uhakiki wa taarifa za anwani za makazi kwenye

halmashauri 24 Tanzania Bara na Zanzibar ambapo idadi ya anwani zilizosajiliwa kwenye Mfumo zimefikia 12,768,909 kati ya anwani hizo 10,760,228 zina majengo na 2,008,681 hazina majengo; kukamilika kwa uboreshaji wa Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi; kuandaliwa kwa rasimu ya sheria ya kusimamia anwani za makazi; na kukamilika kwa zoezi la uhakiki wa taarifa sambamba na kukusanya taarifa za mita za umeme katika Manispaa ya Ubungo ambapo jumla ya mita 63,390 zilikusanywa ili kuwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya mapato yatokanayo na kodi ya majengo na Kuunganisha Mfumo wa NaPA na mifumo mingine ya kutolea huduma ikiwemo TRA, NIDA na ILIMS. Jumla ya shilingi bilioni 16.29 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 3.89 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(iii) Mradi Na. 4280: Tanzania ya Kidijitali**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa mkakati wa uchumi wa kidijitali; kukamilika kwa mapitio ya Sera ya TEHAMA ya Mwaka 2016; kuendelea na zoezi la uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA ambapo mifumo ya NIDA, RITA, UHAMIAJI, ZCSRA na NAPA umefikia asilimia 30; kuanza ujenzi wa daftari la kielektroniki la Serikali ambapo huduma 1,005 zinazotolewa na taasisi 56 zimenakiliwa; kuanza kwa ujenzi wa minara 758 inayojengwa na kampuni za Tigo, Vodacom na Airtel kwa kutoa ruzuku kwenye kampuni hizo za simu; kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa mfumo utakaosaidia kutoa Takwimu za TEHAMA; kuendelea na upanuzi wa mtandao wa Serikali katika ofisi 900 zikiwemo vituo vya afya, mahakama za mwanzo; na vituo nane (8) vya ubunifu vimepatikana katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza, Lindi, Zanzibar na Dodoma. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kupata wakandarasi watakaofanya ukarabati zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 10.2 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 4279: Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi na ufungaji wa miundombinu ya utangazaji ya redio na televisheni katika vituo vya TBC1, TBC2 na Tanzania Safari; kukamilika kwa ufungaji wa mitambo ya redio katika maeneo saba (7) ya Wilaya za Kilwa, Njombe, Ileje, Maswa, Serengeti pamoja na visiwa vya Pemba na Unguja; kukamilisha ufungaji wa mifumo ya kisasa ya kuendeshea mikutano mtandaoni katika Ofisi za Shirika Dar es salaam na Dodoma; kukamilika kwa miradi ya ujenzi wa vituo vya kurushia matangazo ya redio kwa kushirikiana na UCSAF katika Wilaya za Ngorongoro, Uvinza, Mlele,Makete, Kyela, na Mbinga; kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Kituo cha Taifa cha Televisheni (TVT) – Mikocheni Dar es Salaam; kundelea na ujenzi wa makao makuu ya TBC eneo la Vikonje – Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20; na kukamilika kwa ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo mfumo wa kupokea na kuchanganya picha, vifaa vya kurusha matangazo mbashara ya Televisheni (Live U - 7), mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na katika matukio ya nje (Tricaster system, CG, and

monitoring), na jenereta tano (5) kwa ajili ya matangazo ya mbashara nje ya studio. Jumla ya shilingi bilioni 6.55 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 6567: Habari kwa Umma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa na kurushwa katika chaneli ya TBC1 vipindi 36 vya "KAZI IENDELEE" vinavyohusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kununuliwa kwa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya ukusanyaji, uchakataji na uandaaji wa taarifa ikiwemo kamera moja na visaidizi vyake na kifaa kimoja cha kurushia matangazo mubashara; kuchapisha na kusambaza nakala 5,000 za jarida la Nchi Yetu linaloelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ya kimkakati; kukamilika kwa ununuzi wa magari matatu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Idara ya Habari – MAELEZO na kuratibu mikutano ya Taasisi za Serikali 54 kwa ajili ya kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli zake kwa umma kupitia vyombo vya habari. Jumla ya shilingi milioni 991 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 711 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(vi) Mradi Na. 6505: Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha uchapachaji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20; na kununuliwa kwa mitambo ya kisasa ya uchapaji wenye vipande 12. Jumla ya shilingi bilioni 14.93 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(vii) Mradi Na. 6226: Kujenga Kituo Kikuu cha Kuendeleza Ubunifu wa TEHAMA na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Sekta ya TEHAMA Nchini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa vituo vitatu (3) vya kanda vya watengeneza bidhaa za TEHAMA ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40; kuendelea na ujenzi wa kituo cha kuwezesha uanzishwaji wa kampuni changa za TEHAMA cha Dar es Salaam ambapo utekelezaji umefikia asilimia 45; kukamilika kwa matengenezo ya mfumo jumuishi utakaounganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu TEHAMA; kufanya tafiti moja ya TEHAMA. Jumla ya shilingi milioni 500 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 2.75 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(viii) Mradi Na. 4937: Ujenzi wa Kiwanda cha Kupiga Chapa (Government Press Development Programme)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la kiwanda cha kupiga chapa nyaraka za Serikali ambapo utekelezaji umefikia asilimia 97; kununuliwa kwa mashine moja (1) ya kuchapa na kufanya matengenezo ya mashine 13 ambazo zilikuwa hazifanyi kazi; na kuanza kwa ujenzi wa jengo la utawala na ununuzi wa malighafi za uchapishaji. Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 3.45 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

### 2.3.3. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma

#### 2.3.3.1. Uzalishaji Viwandani

**(i) Mradi Na. 6103: Kituo cha Kuendeleza Teknolojia ya Magari Tanzania**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na utafiti na kuunda *prototype* ya gari la Deraya, Nyumbu, na zimamoto na vipuri vitano (5) vya magari ya zimamoto; kuendelea na ununuzi wa mashine na mitambo kwa ajili ya karakana kuu ya kukalibu chuma kitengo cha *grey and ductile cast iron;* kununua mashine aina ya *customized truck head* kwa ajili ya maabara ya utafiti; na kuendelea kujenga uwezo wa wataalam katika kufanya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia ya magari na mitambo.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa ghala (2) kwa ajili ya kuhifadhi malighafi na bidhaa zinazozalishwa na TATC ambapo utekelezaji umefikia asilimia 15, majengo ya karakana kuu ya kukalibu chuma awamu ya kwanza (asilimia 15) na jengo la mkondo wa kuunda magari (asilimia 15) na jengo la mkondo wa kuunda magari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 15; na kuendelea na ukarabati wa majengo, barabara na miundombinu ya milki ambapo utekelezaji umefikia asilimia 74. Jumla ya shilingi bilioni 12.0 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 1214: Kuendeleza Programu ya Maendeleo ya Viwanda - PCP**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa tathmini ya bidhaa za magunia ya mkonge na Jute katika mikoa mitatu (3) ya Dar es Salaam, Morogoro na Tanga ambapo ilibainika kuwa mwenendo wa uzalishaji wa magunia ya mkonge umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2022 zilizalishwa tani 27.56 ikilinganishwa na tani 53.24 kwa mwaka 2021. Jumla ya shilingi milioni 50 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 4901: Programu ya BEST– BEGIN**

Hatua iliyofikiwa: Kuboreshwa kwa sheria 14 zinazoweka vikwazo katika mazingira ya kufanya biashara; kuanzishwa kwa sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Katika Sekretarieti za Mikoa na Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Kitengo cha Mazingira ya Biashara katika Wizara ya Viwanda na Biashara; kuandaliwa kwa Mwongozo wa Majukumu ya Sehemu na Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuafanyika kwa usanifu na utengenezaji wa mfumo wa Government Enterprise Service Bus (GovESB) ambapo mifumo 55 ya Taasisi 50 imewezeshwa kuwasiliana na kubadilishana taarifa. Jumla ya shilingi bilioni 3.3 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shlingi milioni 785.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(iv) Mradi Na. 6260: Mradi wa Kuwezesha Taasisi**

**(a) Kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa na kusimikwa kwa mashine ya *overhead crane*; usimikaji wa kinu cha kuyeyushia chuma (*induction furnace*) umefikia asilimia 99; kukamilika kwa ukarabati wa mfumo wa umeme; na kuendelea kwa majaribio ya uzalishaji wa vipuri kwa kutumia kinu cha kuyeyushia chuma kwa awamu ya pili. Jumla ya shilingi bilioni 1.94 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Eneo la Kongano ya Viwanda – TAMCO**

Hatua iliyofikiwa ni: kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa mita 400 (*China boda road*); kukamilika kwa ujenzi wa mita 230 za barabara ya Viuatilifu; na kuanza kwa ujenzi wa kiwanda cha TATA kwa ajili ya kuunganisha magari. Jumla ya shilingi milioni 132.04 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi wa kuunganisha Matrekta ya URSUS**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea kufanya mazungumzo na Serikali ya Poland kupitia Wawakilishi wa Timu Maalum ya Serikali ya Majadiliano (GNT); na kuendelea kufuatilia madeni kwa wakulima (716) waliokopa matreka hayo. Jumla ya shilingi milioni 236.9 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Kongane la Viwanda Nyanza**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa ghala Na. 1 na kuendelea na ukarabati wa ghala Na. 2 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi milioni 87.01 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(e) Mradi wa kiwanda cha Viuadudu (TBPL)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanikiwa kwa jaribio la pili la viuatilifu na kupata kibali cha kuanza uzalishaji; kukamilika kwa usajili wa dawa ya kibaiolojia ya kuua wadudu (Biopesticides) na kupata cheti cha uzalishaji kwa kipindi cha miaka mitano (5) mfululizo. Jumla ya shilingi bilioni 1.24 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(f) Mradi wa Makaa ya Mawe wa Katewaka**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uthaminishaji wa mali za waathirika 689 wa mradi wa makaa ya mawe Katewaka katika Kijiji cha Nkomang’ombe; na kuendelea na majadiliano na mwekezaji ili kuweza kusaini mkataba wa ubia. Jumla ya shilingi milioni 357.1 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(g) Kufanya Maandalizi ya Uchimbaji wa Chuma Ghafi (iron ore) Maganga Matitu**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa uthaminishaji na uhakiki wa mali za wananchi 381 wanaopisha mradi. Jumla ya shilingi milioni 202.75 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(h) Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini - CAMARTEC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Kiwanda Darasa cha kubangua Korosho katika Wilaya ya Manyoni Mkoani Singida chenye jumla ya vifaa, mashine na mitambo 129; kukamilika kwa ujenzi wa Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (KITEKI) Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha chenye jumla ya zana za kilimo na mashine 49; kufanyika kwa utafiti wa kubaini mahitaji na kiwango cha matumizi ya zana za kilimo, mifugo, uvuvi na teknolojia za vijijini katika Mikoa ya Songwe (Momba), Dodoma (Chemba) na Arusha (Karatu); kukamilika kwa ukarabati wa majengo mawili ya Utawala (Block A na Block B) na nyumba mbili (2) zilizopo katika Kiwanja Na.18 Themi Hill na Kiwanja Na. 83 Kanisa Road (Uzunguni) - Arusha; na kukamilika kwa ununuzi wa jenereta tatu (3) za kuzalisha umeme kwa ajili ya matumizi ya Karakana ya Kituo. Jumla ya shilingi milioni 873.75 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(i) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji taarifa za tathmini ya viwanda na kuainisha fursa za uwekezaji katika Kanda ya Mashariki; kuanza utengenezaji wa mfumo wa kanzidata ya viwanda; kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala ili kutoa nafasi ya kuanzisha kituo cha Taarifa za Viwanda na Ubashiri wa teknolojia na viatamizi kwa wabunifu wa teknolojia ambapo ujenzi umefikia asilimia 70; kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya upimaji ubora bila kuharibu (Non Destructive Testing - NDT) mabomba ya mafuta na gesi ili kuendelea kukidhi viwango vya Kimataifa; kutolewa kwa mafunzo ya kuongeza ujuzi unaohitajika wa NDT kwa wataalam watatu (3); kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya uanzishaji wa maabara ya ngozi ambavyo ni *UV/visible spectrophotometer with software UV solutions, Baxit Differential Scanning Calorimeter BXT.DISC100,Testex, Crock meter (against rubbing) electronic/motorized model (reciprocating), Finish Film adhesiortester Gotester, Elmendorf tearing tester range 1600gm, Testex, na Thickness gauge,analogue oto 10mm*; na kukamilika kwa maabara ya nishati. Jumla ya shilingi bilioni 1.12 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 165.77 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(j) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo – TEMDO**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa usanifu wa mtambo wa kuchakata mkonge ili kupata nyuzi bora; kukamilika kwa usanifu wa teknolojia ya kutengeneza matofali yanayohimili joto kali kwa awamu ya pili; kuendelea na uundaji wa mtambo wa kutengeneza sukari kwa kiwango cha mjasiriamali wa kati (*sugar mini-processing*

*plant, Capacity 200TCD*) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70; kukamilika kwa usanifu wa kuendeleza teknolojia ya kuhifadhi maziwa ili yasiharibike mapema na usanifu wa teknolojia ya kuhifadhi mazao ya mbogamboga kwenye ubaridi (*cold rooms*); kubuni, kusanifu na kutengeneza jokofu la kuhifadhia maiti la kisasa lenye uwezo wa kuhifadhi miili sita (6) kwa wakati mmoja; kuanza kwa utengenezaji kibiashara kwa vifaa tiba mbalimbali ikiwemo vichomea taka hatarishi za hospitalini, vitanda vya wodini vya kawaida, vitanda vya uchunguzi wa madaktari, vitanda vya kujifungulia, *drip stands, hospital screens,* majokofu ya kuhifadhia maiti, na makabati ya wodini; kukamilika kwa usanifu wa mtambo wa kuteketeza taka ngumu za hospitali mahsusi kwa kuchomea damu isiyofaa, mabaki ya wanyama na dawa zilizoharibika na kupitwa muda; kukamilika kwa usanifu wa mtambo wa kukausha korosho pamoja na teknolojia ya mtambo wa kuchakata chikichi ili kuongeza thamani; kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 38 katika maeneo mbalimbali ikiwemo matumizi ya teknolojia ya mashine za *Computerized Numerical Control Machines - CNC*. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(k) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo (SIDO)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilisha ukarabati wa miundombinu ya barabara, mitaro na kalvati katika Soko la SIDO – Mwanjelwa (Mbeya) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; kukamilika kwa ukarabati wa majengo 12 ya viwanda katika Mikoa ya Dar es Salaam (4), Mbeya (1), Arusha (2), Tanga (1), Kigoma (2) na Tabora (2) na ujenzi wa majengo mawili (2) ya viwanda katika Mikoa ya Tanga na Geita; kuendelea na ujenzi wa kituo cha mafunzo na ofisi Nyasa (Ruvuma) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95, majengo ya viwanda katika wilaya za Manyoni (1) na Kahama (2) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 na asilimia 70 mtawalia; kusimikwa kwa mashine za kisasa za kukeleza vyuma, kukata na kukunja mabati (steel plates), kuchomelea na kukata vyuma kwa ajili ya kuimarisha vituo vya Uendelezaji Teknolojia katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mbeya; kutengeneza jumla ya mashine 714 na vipuri 1,891 vya aina mbalimbali kupitia Vituo saba (7) vya kuendeleza Teknolojia (TDCs) kwa ajili ya viwanda vidogo; na kutoa mikopo 2,656 yenye thamani ya shilingi bilioni 6.8 kwa wajasiriamali kupitia mfuko wa NEDF. Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 4486: Uzalishaji Viwandani kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na mapitio na uandishi wa mikakati ya sekta ndogo za nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi na kuanza kutengeneza mikakati mipya ya mafuta, korosho na mkakati wa kuvikuza na kuviendeleza viwanda; kukamilisha taratibu za umiliki wa ardhi yenye ukubwa wa ekari 62 katika Wilaya ya Kahama (Shinyanga); kukamilika kwa utambuzi na tathmini ya kongano za viwanda vya mazao ya kilimo na sekta nyingine zenye fursa za ukuaji wa jasiriamali ndogo na za kati katika mikoa ya Tanzania Bara. Jumla ya shilingi milioni 870.08 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vi) Kuendelea Kueneza Dhana ya KAIZEN Nchini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo ya uhamasishaji wa KAIZEN kwenye mikoa saba (7) ya Lindi, Ruvuma, Mara, Pemba, Shinyanga, Iringa na Kigoma ambapo washiriki zaidi ya 700 walifikiwa; na kufanyika kwa kongamano la wakufunzi wa KAIZEN Tanzania ambapo wakufunzi 80 walishiriki. Jumla ya shilingi milioni 200 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(l) Mchango wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Katika Uchumi wa Viwanda**

**Kilimanjaro International Leather Industries Co Ltd (KLICL)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa eneo la utengenezaji wa bidhaa za ngozi, maabara na kantini, Jengo la Jenereta na barabara za ndani; Kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo mifumo ya maji taka, barabara za ndani na uzio ambapo utekelezaji umefikia asilima 80. Aidha, utekelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata ngozi umefikia asilimia 95. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 95. Jumla ya shilingi bilioni 126.23 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Kiwanda cha Nyama cha Nguru Hills Ranch - Morogoro**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa kiwanda ambapo shughuli zilizotekelezwa ni ujenzi wa majengo, mifumo ya umeme na maji, majokofu ya upoozaji, uunganishaji wa umeme mkubwa na ufungaji wa mashine. Jumla ya shilingi bilioni 20.35 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Kiwanda cha Kuchakata Tangawizi cha ‘Mamba Ginger Factory Limited**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa kiwanda na kuanza uzalishaji. Jumla ya shilingi bilioni 1.83 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Kiwanda cha Chai cha Mponde - Tanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa kiwanda na kuanza uzalishaji. Aidha, hadi kufikia Juni, 2023 jumla ya Wakulima 1,181 walifanikiwa kuuza chai yao kiwandani kupitia Vyama vya Ushirika vya Wakulima (AMCOS). Jumla ya shilingi bilioni 1.19 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(vii) Mradi Na. 4933: Uendelezaji wa Kanda Maalumu za Kiuchumi**

**Eneo Maalum la Uwekezaji Manyara**

Hatua iliyofikiwa: Kukamilika kwa uandaaji wa Mpango Kabambe *(Master Plan*) na Upembuzi Yakinifu *(Feasibility Study)* wa eneo la mradi. Jumla ya shilingi milioni 71.72 zimetumika katika mwaka 2022/23.

### 2.3.3.2.Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia ASDP II

### A. Kilimo

**(a) Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II**

**(i) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa skimu mpya 25 zenye jumla ya ukubwa wa hekta 53,234 katika mikoa ya Katavi, Iringa, Mbeya, Rukwa, Songwe, Dodoma, Mwanza, Pwani, Tabora, Singida, Geita, Kagera, Arusha na Morogoro; kuendelea kukamilisha ukarabati wa skimu 30 zenye ukubwa hekta 41,771 katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Iringa, Katavi, Kilimanjaro, Mwanza, Ruvuma, Tabora na Manyara; kuendelea na ujenzi wa mabwawa 14 yenye jumla ya mita za ujazo 131,535,000 katika mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Singida, Rukwa, Simiyu, Geita, Dodoma, Mwanza, Manyara na Tabora. Aidha, jumla ya ajira 298,635 zimezalishwa katika utekelezaji wa miradi hii.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kununuliwa kwa magari 53 na mitambo 15 kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na mitambo 15 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; na kununuliwa na kusambazwa kwa mashine maalum za kukusanya mapato *Point Of Sales* (POS) 160 kwenye skimu zinazoendelea na uzalishaji. Jumla ya shilingi bilioni 99.3 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Kuwezesha Uanzishwaji wa Mashamba Makubwa ili kuwa Kitovu Cha Teknolojia Bora kwa Wakulima Wadogo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kubainisha, kupima na kuweka mawe ya upimaji kwa ajili ya kuyapatia hati miliki mashamba makubwa ya pamoja 28 yenye ukubwa wa ekari 196,889 katika Mikoa ya Dodoma (ekari 34,613), Kagera (ekari 5,640), Mbeya (ekari 52,165), Njombe (ekari 87,501), Kigoma (ekari 14,875) na Pwani (ekari 2,095) kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (Building a Better Tomorrow - BBT); kukamilika kwa upimaji wa mashamba ya Mlazo/Ndogowe (ekari 11,320), Chinangali (ekari 400), Membe (ekari 7,907), Ikumbulu (ekari 3,558), Lwalaje (ekari 13,405), Nkung'ungu na Mapogoro (ekari 27,231); kusafishwa kwa shamba la Chinangali lenye ukubwa wa ekari 400 na mashamba yenye ukubwa wa ekari 77.8 katika vituo atamizi vya Bihawana (ekari 22), Mlingano (ekari 4), Uyole (ekari 3), Mubondo (ekari 10), Ukiriguru (ekari 8.9), NSI - Kidatu (ekari 2.4), Horti Tengeru (ekari 4), Mtwara (ekari 10), Ilonga (ekari 3.5) na Tumbi (ekari 10); kusafishwa kwa ekari 5,500 za shamba la Mlazo/Ngogowe; kukamilika mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana 812 wa BBT katika vituo atamizi; na kulipa fidia ya shamba la Chinangali lenye ukubwa wa ekari 400. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 6.6 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(iii) Kuimarisha Vituo vya Utafiti na Utafiti wa Mbegu Bora**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za TARI Makao Makuu – Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 41, Kituo cha TARI Kihinga – Kigoma (asilimia 75), miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya utafiti katika vituo 16 vya TARI vyenye hekta 804 (asilimia 25), ghala tano (5) zenye vyumba vya ubaridi (cold rooms) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,075 za mbegu katika vituo vya TARI Selian, Hombolo, Tumbi, Naliendele na Dakawa (asilimia 30), maabara ya TARI Mlingano kwa ajili ya uzalishaji wa miche kwa njia ya chupa (asilimia 40) na uzio wa kituo cha TARI Uyole lenye hekta 1,042 (asilimia 15); kukamilika kwa ukarabati wa maabara ya TARI Tengeru; na kuidhinishwa kwa aina tano (5) za mbegu mpya za zabibu katika Kamati ya Taifa ya Mbegu. Jumla ya shilingi bilioni 17.61 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 4.24 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(iv) Kuimarisha Huduma za Ugani, Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima**

**(a) Ukarabati wa Vyuo vya Kilimo na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa miundombinu 53 katika vyuo vya Mafunzo ya Kilimo Tumbi, Igurusi, Ilonga na National Sugar Institute; kukamilika kwa ujenzi wa madarasa katika chuo cha National Sugar Institute - NSI; na utoaji wa chakula kwa wanafunzi wa vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo.

Shughuli nyingine iliyotekezwa ni: kununuliwa kwa vifaa vya mafunzo katika Vyuo vya Mafunzo ya kilimo vya HORTI Tengeru, MATI (Ilonga, Tumbi na Uyole) na Bihawana FTC. Jumla ya shilingi bilioni 7.14 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 1.14 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(b) Kuimarisha Huduma za Ugani**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuboresha mazingira ya utoaji huduma kwa kununua na kusambaza pikipiki 5,889 kwa maafisa ugani katika mikoa 25; kununua na kusambaza viti 1,020 na meza 23 katika Vituo vitano (5) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (WARCs) katika mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu; kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 667 wa Halmashauri 142 kutoka katika mikoa 25 kuhusu matumizi ya vifaa vya kupima afya ya udongo na maafisa ugani 203 kuhusu kilimo biashara; na kununuliwa kwa vifaa 143 vya upimaji wa afya ya udongo kwa maafisa ugani wa Halmashauri 143, vishikwambi 580 na visanduku vya ugani (Extension Kits) 1,000 katika Halmashauri 46.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kuanzishwa kwa kituo cha ufuatiliaji (Control Center) kwa ajili ya kufuatilia matumizi ya pikipiki za Maafisa Ugani na kuratibu ufungaji wa GPS kwenye pikipiki ambapo pikipiki 5,436 zimefungwa GPS katika mikoa 25 ya Tanzania Bara; na kuanzishwa kwa kituo cha huduma za mawasiliano ya kilimo (Call Centre) kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa ushauri wa kitaalam na

taarifa mbalimbali kwa wadau wa kilimo. Jumla ya shilingi bilioni 13.33 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 3.05 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(v) Kuongeza Tija na Uzalishaji**

**(a) Upatikanaji wa Mbegu Bora**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuzalishwa na kusambazwa tani 1,004 za mbegu bora za Alizeti kwa wakulima kwa bei ya ruzuku katika wilaya 39 za mikoa ya Dodoma, Kagera, Mbeya, Mwanza na Singida. Kati ya kiasi hicho, tani 300 zimezalishwa na Sekta Binafsi; kuzalisha miche 230,000 ya parachichi na miche 466,000 ya chikichi; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Kilimi (Nzega) lenye ukubwa wa hekta 400 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70, Arusha (hekta 200) asilimia 15 na Msimba (Kilosa) hekta 200 asilimia 25; kukamilika kwa uchimbaji wa visima virefu sita (6) katika shamba la mbegu la Msimba; kuanzishwa kwa mashamba mapya ya mbegu yenye hekta 850 katika maeneo ya Mwele – Tanga, Msimba – Kilosa na Kilimi – Nzega; kukamilika kwa ukarabati wa ghala la kuhifadhi mbegu na usimikaji wa mtambo mpya wenye uwezo wa kuchakata tani tatu (3) za mbegu kwa saa katika shamba la Msimba; kununuliwa kwa matrekta sita (6) na zana zake kwa ajili ya mashamba ya Msungura, Namtumbo, Msimba, Dabaga, Mbozi na Kilimi; na kununuliwa magari tisa (9) ya kusambaza mbegu.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa uzio wenye urefu wa km12 katika shamba la mbegu la Kilimi-Nzega ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60; na kutambuliwa kwa maeneo sita (6) ya kuchimba visima katika shamba la Ngaramtoni (Arusha). Jumla ya shilingi bilioni 20.4 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 4.99 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(b) Upatikanaji wa Mbolea ya Ruzuku**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa na kusambazwa kwa mbolea ya ruzuku tani 531,091 kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini; na kusajiliwa kwa waingizaji wakubwa wa mbolea 29, mawakala wadogo 4,511, wazalishaji wa ndani watatu (3) wa mbolea na wakulima 3,459,563 kwenye mfumo wa kielektroniki. Mpango wa mbolea ya ruzuku umewezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kwa asilimia 46 kutoka tani 363,599 kwa mwaka 2021/22 hadi tani 531,091 mwaka 2022/23 na kuwezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021/22 hadi tani 20,402,014 mwaka 2022/23. Jumla ya shilingi bilioni 214.8 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Upatikanaji wa Viuatilifu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa na kusambazwa kwa viuatilifu lita 153,890.26 na kilo 2,000 za kudhibiti visumbufu vya milipuko ya viwavijeshi katika mikoa 18 nchini; kununuliwa na kusambazwa kwa viuatilifu vya zao la pamba jumla ya Ekapaki 12,

650,000 (lita1,265,000) ambapo wakulima 550,000 wamenufaika katika mikoa 17; kununuliwa na kusambazwa kwa viuatilifu vya zao la korosho tani 15,015.03 na lita 2,684,470.5 ambapo wakulima 483,000 wamenufaika katika mikoa 23; kununuliwa na kusambazwa kwa lita 84,938.48 za viuatilifu vya zao la tumbaku ambapo wakulima 70,318 wamenufaika; na kutolewa kwa mafunzo ya matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wakulima, wafanyabiashara, maafisa ugani na wanyunyiziaji katika mikoa ya Mwanza, Mara, Mbeya, Iringa, Morogoro, Lindi, Mtwara na Arusha. Jumla ya shilingi bilioni 34.57 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 40.50 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(vi) Kuimarisha Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa ghala nane (8) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 250 ambapo utekelezaji katika ghala la Litisha umefikia asilimia 98, Lipaya (asilimia 21.58), Liula (asilimia 40.8), Hangangadinda (asilimia 70); Lilondo A (asilimia 5); Matetereka (asilimia 40.2); Kizuka (asilimia 93); na Gumbiro (asilimia 93) katika Halmashauri ya Madaba na Songea; na kuendelea na ujenzi wa ghala 28 katika Mkoa wa Ruvuma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40.

Shughuli nyingine iliyotekelezwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa ghala la mkongotema lenye uwezo wa kuhifadhi tani 200 katika halmashauri ya Madaba. Jumla ya shilingi bilioni 4.05 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vii) Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA kununua mahindi tani 17,257.857 na mtama tani 1,036.457 na Bodi ya Mazao Mchanganyiko – CPB kununua mahindi tani 26,479.83, mtama mweupe tani 1,751.81, maharage tani 66.65, mafuta ghafi ya alizeti tani 128.93, mchele tani 691.25, maharage ya soya tani 239.95, maharage ya njano tani 40.88, mpunga tani 3,511.90 na ngano tani 11,419.72; kukamilika kwa maandalizi ya uanzishwaji wa mnada wa chai kwa njia ya mtandao. Aidha, hadi robo ya kwanza ya mwaka 2023/24, jumla ya tani 199,506 za nafaka zimenunuliwa kupitia katika vituo 75 vilivyopo katika kanda nane (8) za NFRA. Kiasi hicho kinafanya hifadhi ya chakula katika ghala zote za NFRA kuwa tani 244,598. Jumla ya shilingi bilioni 17.46 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 153.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(viii) Kuboresha Mifumo ya Kitaasisi, Bodi na Sheria**

**(a) Mifumo ya Kielektroniki ya kutoa huduma katika Sekta ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kutumika kwa Mfumo wa M-Kilimo kwa kutoa huduma ya ushauri wa kilimo bora cha mazao mbalimbali ikiwemo kujibu kero zinazohusu utoaji wa mbolea ya ruzuku kwa wadau wa kilimo 89,107; na kuendelea na matumizi ya mfumo wa kutoa huduma za biashara ya mazao (Agriculture Trade Management

Information System - ATMIS) ambapo jumla ya wakulima 600 wamesajiliwa na kupata huduma.

**(b) Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Mitaji katika Sekta ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo; na kupunguza riba ya mkopo kwa wakulima na kuwa chini ya asilimia 10. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kutolewa kwa mikopo ya kilimo yenye thamani ya shilingi bilioni 801 kupitia Benki ya CRDB kwa Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) 472; kutolewa kwa mikopo katika sekta ya kilimo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.62 kupitia benki ya NMB; na kutolewa mikopo 20 yenye thamani ya shilingi milioni 704 kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo – AGITF; na kuanzisha huduma ya *soft loan* kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake kupata mitaji ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kilimo. Jumla ya shilingi milioni 200 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ix) Kuimarisha Usimamizi wa Maendeleo ya Ushirika**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha TANECU (Newala) cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 za korosho kwa mwaka; na kusajiliwa kwa vyama viwili (2) vya ushirika katika vikundi vidogo vya wakulima 120 wa mazao ya mboga na matunda katika mikoa ya Arusha, Mbeya na Njombe; na kutoa mafunzo kwa wakulima 8,807 kuhusu uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya Mbogamboga katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe.

Shughuli nyingine iliyotekelezwa ni: kuanzishwa kwa mfumo wa TEHAMA wa usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambapo vyama 4,661 vimesajiliwa katika mfumo huo. Jumla ya shilingi bilioni 1.01 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4499: Kudhibiti Sumukuvu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa ghala 14 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 21,500 za mahindi na karanga katika mikoa 10 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 97, Kituo Mahili cha Usimamizi wa Mazao ya Nafaka katika Wilaya ya Kongwa (asilimia 76) na Maabara ya Utafiti wa Magonjwa ya Mimea Kibaha mkoani Pwani (asilimia 99); kutolewa kwa mafunzo kwa vijana 420 kupitia Chuo cha Mafunzo ya Ufundistadi (VETA) kuhusu utengenezaji wa vihenge vya chuma kwa ajili ya kuhifadhi mazao vijijini; na kutolewa kwa mafunzo kwa wakulima 69,010 na wafanyabiashara 5,147 kuhusu udhibiti wa Sumukuvu.

Shughuli nyingine iliyotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa maabara kuu ya kilimo kwa ajili ya kudhibiti ubora wa mazao Mtumba - Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 28. Jumla ya shilingi bilioni 21.87 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4497: Kuongeza Uhifadhi wa Nafaka**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa vihenge (20) na ghala nne (4) katika wilaya za Babati, Mpanda na Sumbawanga; kuendelea na ujenzi wa vihenge 36 na ghala nne (4) kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao kufikia tani 501,000 katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4427: Kuendeleza Kilimo na Uvuvi - AFDP**

Hatua iliyofikiwa: Kutolewa kwa mafunzo maalum ya kisayansi ya muda mfupi kwa watafiti 46 (breeders) kuhusu teknolojia ya mbegu kwenye mazao ya mahindi, maharage, alizeti na kunde; kukamilika kwa EIA katika miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya Msimba (Kilosa), Kilimi (Nzega); kuendelea na ujenzi wa maabara ya mbegu katika mashamba ya utafiti ya TARI mkoani Morogoro; na kutolewa kwa mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu 79 kutoka TOSCI. Jumla ya shilingi billioni 2.05 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**B. Mifugo**

**Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

**(i) Kuimarisha Afya ya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa majosho 246 na kuendelea na ujenzi wa majosho 11 katika Mikoa 25; kununuliwa kwa lita 52,560 za dawa ya kuogesha mifugo na kusambazwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 172, mashamba matano (5) ya kuzalisha mitamba na taasisi zilizo chini ya Wizara; kusambazwa kwa chanjo za mifugo dozi 696,393,500 dhidi ya magonjwa mbalimbali ya kipaumbele kati ya hizo, dozi 177,150,500 zilizalishwa nchini na dozi 519,243,000 ziliagizwa kutoka nje ya nchi; na kununuliwa kwa gari lenye mfumo baridi kwa ajili ya kusambaza chanjo. Jumla ya shilingi bilioni 8.48 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Kuimarisha Huduma za Ugani**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa magari 13 kwa ajili ya uratibu wa ugani na pikipiki 1200 kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini; kukamilika kwa taratibu za uanzishwaji wa mashamba darasa matano (5) ya ufugaji kuku katika Mikoa ya Ruvuma (Songea MC - 3) na Shinyanga (Kishapu - 2) kwa ajili ya vikundi vya wanawake vinavyojishughulisha na ufugaji wa kuku; na kununuliwa kwa ng'ombe 2,400 kwa ajili ya unenepeshaji kwenye vituo 8 vya BBT-Mifugo vilivyolenga vijana na wanawake 238 kujifunza ufugaji wa kibiashara ili kuchochea ajira za vijana na wanawake, na kuongeza malighafi kwenye viwanda vya kuchakata nyama na kuuza nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 8.1 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Kuimarisha Huduma za Tafiti**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa vifaa shamba vikiwemo matrekta (4), *disc plough* (3), *harrow* (2), *bailer* (1) na *forage chopper* (1) kwa ajili ya kuwezesha utafiti wa mifugo hususan utafiti wa malisho pamoja na kununuliwa kwa mbuzi 2070 kwa ajili ya shughuli za kitafiti katika vituo vya utafiti wa mifugo vya TALIRI Tanga, Kongwa, Mabuki, Uyole na Mpwapwa. Jumla ya shilingi milioni 800.7 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iv) Uboreshaji wa Mbari kwa ajili ya Uzalishaji wa Maziwa na Nyama**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa ng'ombe wazazi 1,160 na kusambazwa katika Mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba ya Mabuki (500), Sao Hill (500) na Kitulo (160); kununuliwa kwa madume bora 366 ya ng'ombe na kusambazwa kwa wafugaji kupitia vikundi vya wafugaji katika Halmashauri saba (7); kuzalishwa kwa mitamba 955 iliyoongezwa kwenye kundi la ng'ombe wazazi katika mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba; kuzalishwa kwa jumla ya dozi 149,975 za mbegu za mifugo katika kituo cha NAIC kwa ajili ya uhimilishaji; kusimikwa kwa mtambo wa kuzalisha Nitrogen kwenye Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC); na kuhimilisha ng'ombe 124,613 katika mikoa 26. Jumla ya shilingi bilioni 6.9 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(v) Kuimarisha Miundombinu ya Masoko ya Mifugo na Mazao Yake**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa mnada wa Lupa – Chunya na Buzirayombo – Chato; kuendelea na ujenzi wa minada ya Mkongeni – Morogoro (asilimia 85), Majimoto – Katavi (asilimia 10), Utengule – Mbeya (asilimia 75) na Lugodalutale – Iringa (asilimia 75), Kilyamatundu – Rukwa (asilimia 50), Bukombe (asilimia 65) na Kasamwa – Geita (asilimia 70), Huzi – Dodoma (asilimia 20) na Kintinku – Singida (asilimia 30); kuendelea na ujenzi wa mnada mmoja (1) wa mpakani wa Randa – Mara (asilimia 95); na kuendelea na ujenzi wa vituo 10 vya kukusanyia maziwa vya Kwemakame (asilimia 70) na Msomera (asilimia 85) – Tanga, Malimbika - Dar es Salaam (asilimia 80), Magogoni – Morogoro (asilimia 70), Lukani – Kilimanjaro (asilimia 75), Ngaramtoni – Arusha (asilimia 75), Komunge – Mara (asilimia 70), Maswa – Simiyu (asilimia 70), Karagwe – Kagera (asilimia 85) na Makambako – Njombe (asilimia 70). Jumla ya shilingi bilioni 3.1 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vi) Kuimarisha Unywaji wa Maziwa Shuleni**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuongezeka kwa shule za msingi na sekondari zinazoshiriki katika Mpango Mkakati wa Unywaji Maziwa kutoka shuleni 39 hadi 134; na kukamilika kwa ujenzi wa vituo nane (8) vya unywaji maziwa vya Morogoro (4) na Mbeya (4). Jumla ya shilingi milioni 138.87 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(vii) Kuimarisha Huduma za Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa matatu (3) ya Kimambi na Matekwe – Lindi na Mhanga (Singida); kukamilika kwa uchimbaji wa visima virefu vitatu (3) vya Matanzi (Pwani), Makatapola (Iringa) na Lwami (Kilimanjaro); na kuendelea na usafishaji wa maeneo hekta 175 kwa ajili ya kupanda malisho katika shamba la Vikuge la kuzalisha malisho na mbegu za malisho ambapo usafishaji wa eneo umefikia asilimia 75.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mabwawa 11 ya Oloirieni (asilimia 20) na Naalaram (asilimia 95) – Arusha, Kwekikwembe (asilimia 40) na Msomera – Tanga (asilimia 55), Kongwa – Dodoma (asilimia 20), Vinyenze – Pwani (asilimia 80), Chang'ombe – Mbeya (asilimia 20), Kihumbo (asilimia 40) na Bukabwa – Mara (asilimia 40) na Kaiwang (asilimia 70) na Leralumo (asilimia 20) – Manyara na Msaginia – Katavi (asilimia 70); na kuendelea na uchimbaji wa visima virefu vitatu (3) vya Kitaraka – Singida (asilimia 10), Kapele - Kasinde - Songwe (asilimia 10) na Kinamwigulu – Maswa (asilimia 70). Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(viii) Kuboresha Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa kumbi mbili (2) za mihadhara zenye uwezo kuhudumia wanafunzi 250 kila moja katika kampasi ya Mabuki; kukamilika kwa ujenzi wa hosteli mbili (2) zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 216 kila moja katika kampasi za Morogoro na Mpwapwa; na kuendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara zenye uwezo kuhudumia wanafunzi 250 kila moja katika kampasi za Mpwapwa (asilimia 80) na Morogoro (asilimia 85). Jumla ya shilingi bilioni 2.12 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ix) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na Tafiti za TALIRI**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa ng'ombe wazazi 1,000 kwa ajili ya NARCO; kununuliwa kwa Matrekta tisa (9), *harrow* (**2**), *Bailers* nne (4), *Mowers* nne (4), *Trailers* nne (4), *chisel plough* mbili (2), *disc plough* (**3**), *forage chopper* (**1**) na *Hay rakes* 10 ili kuimarisha uzalishaji wa NARCO na kuwezesha TALIRI kufanya tafiti za mifugo; pamoja na kuchimba visima virefu vitatu (3) katika Ranchi ya Kongwa. Jumla ya shilingi bilioni 3.8 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**C. Uvuvi**

**(a) Mradi Na. 4701: Mradi wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi – (South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth – SWIOFish)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala la ofisi ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu - Mafia ambapo ujenzi umefikia asilimia 90; kuendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari - Kunduchi, Dar es Salaam ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65; na kukamilika

kwa ujenzi na ununuzi wa samani za ofisi katika Maabara ya Utafiti wa Uvuvi katika kituo cha TAFIRI - Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 3.49 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 1.48 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(b) Kuimarisha na Kuendeleza Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi na ununuzi wa samani za Ofisi ya Maeneo ya Pamoja ya Usimamizi wa Uvuvi (CFMA) katika Kijiji cha Karema (Tanganyika); Kukamilika kwa ujenzi wa FRP Busega (Simiyu), kuendelea na ujenzi wa ofisi mbili (2) za ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi za Nyakalilo (Sengerema) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60 na Sota - Rorya (Asilimia 60); kununuliwa kwa pikipiki 50 za maafisa ugani wa uvuvi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi; kuendelea na taratibu za kupata wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya vituo nane (8) vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi vya Kigoma, Tanga, Mtwara, Muleba, Kagera, Mtera, Ikola na Singida na ukarabati wa vituo viwili (2) vya Kipili na Buhingu; kuendelea na taratibu za ununuzi wa boti 10, mizani mitano (5), magari sita (6) na pikipiki 20 kwa ajili ya maafisa ugani katika vituo vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Jumla ya shilingi milioni 234 zimetumika mwaka 2022/23.

**(i) Kujenga na Kuimarisha Miundombinu ya Uvuvi (Mialo na Masoko)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo na miundombinu ya kuuzia samaki katika mwalo wa Chifunfu/Kijiweni (Sengerema); kuendelea na ujenzi ya mwalo wa Igabiro (Bukoba) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60; kupatikana kwa wazabuni wa kujenga mialo mitatu (3) ya Chato Beach (Chato), Karungu (Nkasi), na Ng’ombo (Nyasa); kuendelea na ujenzi wa masoko katika halmashauri mbili (1) ambapo soko la Kasanga (Kalambo) utekelezaji umefikia asilimia 80, na Masuche - Momba (asilimia 2); mkandarasi kukabidhiwa eneo la ujenzi la Kyamkwikwi katika halmashauri ya Muleba; kuendelea na ukamilishaji wa mikataba minne (4) ya ujenzi wa masoko ya Tunduma (Tunduma), Kyamkwikwi (Muleba), Nyamikoma (Busega) ), Manda (Ludewa) na Zingibari (Mkinga). Jumla ya shilingi milioni 245.3 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(ii) Kujenga na Kukarabati Miundombinu ya Ukuzaji Viumbe Maji (Vituo na mashamba darasa)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kwa ujenzi wa mashamba darasa (6) katika Halmashauri sita (6) ambapo utekelezaji katika Wilaya za Kongwa umefikia asilimia 90, Iringa (asilimia 60), Njombe (asilimia 80), Songea (asilimia 95), Tandahimba (asilimia 15) na Ruangwa (asilimia 75); kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala, kitotoleshi, maabara, matanki na mabwawa katika Kituo cha Ruvula – Mtwara ambapo utekelezaji upo katika hatua za umaliziaji; kuendelea na ujenzi wa kitotoleshi, ukarabati na upanuzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji cha Nyengedi - Lindi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 25; kuendelea na ujenzi wa Kitotoleshi cha vifaranga vya samaki na upanuzi wa kituo cha Ruhila - Songea ambapo

utekelezaji umefikia asilimia 35. Jumla ya shilingi milioni 950.57 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(iii) Kuimarisha upatikanaji wa zana, vifaa na pembejeo za uvuvi na ukuzaji viumbe maji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa utengenezaji na usambazaji wa boti 160 za kuwakopesha wavuvi; kuendelea na matengenezo ya vizimba 615 vya kufugia samaki; kuendelea na taratibu za kuwezesha upatikanaji mikopo kwa wakulima wa mwani katika benki ya TADB; na kutolewa kwa mafunzo kwa vijana 200 wanaojishughulisha na uvuvi na ukuzaji viumbe maji kupitia programu maalum za BBT LIFE. Jumla ya shilingi bilioni 24.73 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(iv) Kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa kitotoleshi katika Kampasi ya Gabimori - Mara ambapo utekelezaji umefikia asilimia 25 na ujenzi wa maabara katika Kampasi ya Mikindani - Mtwara (asilimia 40); na kuendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara katika Kampasi ya Nyegezi (Mwanza) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 na maabara (asilimia 60). Jumla ya shilingi milioni 217.4 zimetumika mwaka 2022/23.

**(v) Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa awamu ya pili ya utafiti wa uwingi, bioanuwai na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika ambapo aina 7 za samaki na sampuli jumla ya 639 zilikusanywa na kusafirishwa kwenda Uingereza; kufanyika kwa utafiti, kutambuliwa na kufanyiwa vipimo vya '*Bathymetry'* kwa maeneo 81 yanayofaa kufugia samaki katika mikoa ya Mara, Simiyu, Geita na Kagera; kuanza kwa ujenzi wa atamizi maalum mbili (2) katika kituo cha Nyegezi - Mwanza na Sota - Rorya za ukuzaji viumbe maji zenye vizimba 40, kitotoleshi, mabwawa ya kufugia samaki na mtambo wa kutengeneza chakula cha Samaki. Jumla ya shilingi bilioni 3.36 zimetumika mwaka 2022/23.

**(vi) Kuimarisha Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa boti moja (1) yenye vioo chini (glass bottom boat) ili kuongeza utalii baharini katika maeneo tengefu (eco-tourism) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60. Jumla ya shilingi milioni 188 zimetumika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4703: Ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa Jengo la Utawala la RAS MKWAVI (Block B); na kuandaa na kuhuisha *Bussiness Model* na Mpango wa Biashara wa miradi itakayotekelezwa na Shirika; kuanza taratibu za kupata mkandarasi wa kukarabati gati la kuegeshea meli (Floating Jetty RAS MKWAVI – Dar es Salaam; kuanza taratibu za manunuzi ya magari mawili (2) ya ubaridi; na kununuliwa kwa mtambo wa kuzalisha barafu kwa ajili ya kituo cha RAS MKWAVI – Dar es Salaam.

Jumla ya shilingi milioni 29.1 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 195.8 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(d) Programu 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na taratibu za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki, mfumo wa umeme na maji, kisima cha maji, ununuzi wa gari la ubaridi la kusafirisha samaki katika vituo vya ukuzaji viumbe maji vya Kingolwira (Morogoro), Mwamapuli (Katavi) na Rubambagwe (Geita); kuendelea na mchakato wa ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi; kukamilika kwa tathmini ya athari za mazingira na jamii kwa ajili ya ujenzi wa soko la samaki Kipumbwi (Pangani); kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kuvutia samaki (Fish Aggregate Device – FADs) na utambuzi wa maeneo ya kuweka vifaa hivyo katika pwani ya bahari ya Hindi; kuendelea na taratibu za manunuzi ya mitambo minne (4) ya umeme ya kukaushia dagaa katika mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara na Geita. Jumla ya shilingi milioni 596.45 zimetumika mwaka 2023/24.

#### 2.3.3.3. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia

**(i) Mradi Na. 1119: Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (Sustainable Management of Mineral Resources Project - SMMRP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununua na kusimika vifaa vya utafiti wa kisayansi (geoscience) na vifaa vya maabara na uchunguzi katika Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania – GST (Dodoma); kununua mitambo mitano (5) ya uchorongaji. Ununuzi wa mitambo hii kutawezesha wachimbaji kuweza kuchoronga na kupata taarifa sahihi za kisayansi kuhusu maahapo yalipo na kuweza kuchimba kwa tija bila ya kupoteza mtaji; kununuliwa kwa mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa mbadala.Mitambo hii itaongeza uzalishaji wa nishati mbadala na hivyo kupunguza ukataji wa kuni kwa ajili ya kuni na mkaa wa miti; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kuhifadhia sampuli za miamba choronge eneo la Kizota - Dodoma; kutengeneza mfumo wa usimamizi na utoaji leseni za madini nchini; ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya matumizi ya ofisi Dodoma; kununua magari 12 ya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za uchimbaji na biashara ya madini nchini; na kununuliwa kwa mawe mawili (2) makubwa ya madini ya Tanzanite yenye jumla ya uzito wa kilo 5.22 kutoka kwa mchimbaji mdogo. Jumla ya shilingi bilioni 11.8 zimetumika katika kipindi cha mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 1120: Kituo cha Jemolojia Tanzania (Tanzania Geomological Centre)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwawezesha watumishi tisa (9) wa Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi (Thailand, China na India); na kukamilika kwa usanifu wa Kituo cha Jemolojia (Tanzania Geomological Centre) Jijini Arusha, Phase I . Jumla ya shilingi milioni 716.34 zimetumika katika kipindi cha mwaka 2022/23 na shilingi milioni 298.64

katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

#### 2.3.3.4. Huduma

**A. Maliasili na Utalii**

**Utalii**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa Programu ya *Tanzania - the Royal Tour* ambapo idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi watalii 1,454,920 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 57.7 na mapato yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,310 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,527.72 sawa na ongezeko la asilimia 93. Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2023, idadi ya watalii wa kimataifa walioingia nchini imeongezeka kufikia watalii 759,327 ikilinganishwa na watalii 575,397 katika kipindi kama hicho mwaka 2022; kuongezeka kwa idadi ya watalii wa ndani waliotembelea maeneo ya hifadhi, vituo vya malikale na makumbusho kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 1,115,342 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 41.3 na idadi ya watalii waliotembelea hifadhi za misitu ya mazingira asilia kutoka watalii 67,677 mwaka 2021 na watalii 210,987 mwaka 2022 hadi watalii 97,862 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023; na huduma za malazi zinazokusanya tozo ya kitanda kwa siku (bed night levy) zimeongezeka kutoka 8,681 mwaka 2021 hadi 9,059 mwaka 2022.

**Maliasili**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupungua kwa ujangili na uvunaji haramu wa maliasili ambapo umepelekea kuongezeka idadi ya wanyamapori, ikiwemo tembo kutoka 43,330 mwaka 2014 hadi 60,000, faru weusi kutoka 163 mwaka 2019 hadi 238 mwaka 2022 katika Mfumo Ikolojia Ruaha – Rungwa; kuongezeka kwa upatikanaji wa malighafi ya mazao ya misitu (mbao) katika mashamba ya miti ya Serikali kutoka wastani wa mita za ujazo 1,000,000 kwa mwaka 2021/22 hadi mita za ujazo 1,226,807.3 kwa mwaka 2022/23; kuandaliwa kwa Mpango wa Uhifadhi wa Mji Mkongwe Mikindani (2022/23 – 2026/27); kutoa elimu na vifaa (mizinga ya nyuki 176, tochi zenye mwanga mkali 221, vuvuzela 125, *Roman candles* 107, vingo'ora 20, fataki 170, honi 70 na pilipili ya unga na mbegu) kwa ajili ya kudhibiti uvamizi wa hifadhi na shoroba kwa ajili ya shughuli za kibinadamu; kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kupitia Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori; na kudhibiti mimea vamizi kupitia Mpango Mkakati wa kitaifa wa Kutokomeza Mimea Vamizi (2019 - 2024).

**(a) Mradi Na. 5203: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa usanifu wa viwanja vya ndege sita (6) ambavyo vitajengwa katika hifadhi za Ruaha (3), Mikumi (1) na Nyerere (2) ambapo zabuni kwa ajili ya ujenzi imetangazwa; kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya huduma

za kitalii ikiwemo malango, vituo vya kutolea taarifa na kambi za utalii katika hifadhi za Taifa za Nyerere, Ruaha, Udzungwa na Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Kilombero; ununuzi wa matrekta saba (7) pamoja na viambata vyake 23 kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo ya hifadhi; kuwezesha vijana 120 kutoka wilaya za Kilolo, Iringa, Mvomero, Chamwino na Rufiji kupata mafunzo ya mbinu za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; kuwezesha vikundi 159 vyenye jumla ya wanachama 3,816 kwa kuwapatia fedha mbegu jumla ya shilingi bilioni 1.45 katika vijiji 15 vya awamu ya kwanza vinavyopakana na hifadhi za Taifa Ruaha, Nyerere, Mikumi na Udzungwa; kufanyika kwa tafiti nne (4) za wanyamapori katika hifadhi za kipaumbele zinazohusiana na migogoro baina ya binadamu na wanyamapori; ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu ya Umwagiliaji ya Madibira katika wilaya ya Mbarali ambapo Mfereji mkuu wenye kilometa 2.9 na mfereji wa upili Kilometa 6.9 imekamilika; kupandwa kwa miche ya miti 18,000 rafiki kwa maji na mazingira katika vyanzo vya maji katika wilaya za Makete (5,000), Wanging'ombe (7,000), Mufindi (5,000) na Mbarali (1,000).

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuandaliwa kwa Mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vya Miyombweni, Igenge na Kigenge vilivyopo katika wilaya za Makete, Mufindi, na Mbarali. Jumla ya shilingi bilioni 47.8 zimetumika katika Mwaka 2022/2023 na shilingi bilioni 7.62 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(b) Mradi Na. 4812: Mradi wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara**

Hatua iliyofikiwa ni: kuwezesha kufanyika kwa doria za ki-intelijensia na ushirikiano na nchi jirani katika kanda 10 zilizowezesha kukamatwa kwa vipande 59 vya meno ya tembo, meno mazima ya tembo 29, silaha 19, vichwa 28 vya Swala Tomi, pikipiki mbili (2) nyamapori aina 101 mbalimbali na majangili 93; na ununuzi wa vifaa vya doria ikiwemo mahema 24, GPS 20, Komputer 15, Sare jozi 100 na Kamera 15 na kusambazwa kwa Kanda za Kiikolojia za Kuratibu Doria za Kupambana na Ujangili na Kikosi Kazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kwa wananchi katika maeneo mbalimbali yenye migongano ya wanyamapori na binadamu kuhusu mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu (matumizi ya mabomu ya pilipili, mizinga ya nyuki, mazao ambayo hayapendwi na tembo) katika Wilaya za Iringa, Mbarali, Wanging'ombe na Manyoni. Jumla ya shilingi bilioni 2.7 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4647: Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kwa viongozi 296 wa vikundi vya upandaji miti, wakulima hodari 160 na wakulima 6,146 kuhusu namna ya kusimamia na kuendesha vikundi; kutoa misumeno 335 ya kupogolea miti kwa vikundi 80 vya

upandaji miti; na kutolewa kwa vifaa vya kupambana na majanga ya moto (fire beaters 393 na knapsack fire sprayers 36). Jumla ya shilingi bilioni 2.8 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4650: Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (Forestry and Value Chain Development Programme - FORVAC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwezesha uvunaji wa miti aina ya Burkea africana, Brachistegia spefiformis, Entandofragma storzi, Ptreocarpus tinctoris na nyinginezo ambapo kiasi cha shilingi 264,250,000 kilipatikana kutokana na mauzo ya 7,560 m3 za mbao kutoka katika misitu mitano ya vijjji katika Wilaya za Songea na Liwale; kununuliwa kwa vifaa vya ufugaji nyuki, useremala, vinyago, uyoga na mianzi katika maeneo ya vijiji vya mradi; kukamilika kwa ununuzi, ufungaji na usajiri wa viwanda jongea viwili (mobile sawmills) vya kuchakata mazao ya misitu kwa njia endelevu; na kununuliwa kwa mitambo ya kukausha mazao ya misitu kwa kutumia teknolojia ya mionzi ya jua katika Wilaya ya Liwale na Ruangwa. Jumla ya shilingi bilioni 2.93 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4651: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki - BEVAC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa ofisi ya mradi iliyopo Pemba; kununuliwa kwa magari matatu (3) na pikipiki 20 kwa ajili ya maafisa; kutolewa kwa mafunzo kuhusu mbinu za ufugaji bora wa nyuki kwa vyama vya ushirika 19 vyenye jumla ya wafugaji nyuki 1,204; kuwaunganisha wafanyabiashara sita (6) wanaouza asali nje ya nchi na wafugaji nyuki 296 na vikundi 29; na kuwezesha kampuni 10 za uuzaji na usafirishaji wa asali nje ya nchi kupata cheti cha ubora kitakachowezesha kampuni hizo kuuza asali katika masoko mbalimbali duniani. Jumla ya shilingi bilioni 2.94 zimetumika katika Mwaka 2022/2023.

**B. Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**(i) Mradi Na. 6293: Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukarabatiwa kwa jengo lililokuwa Makao Makuu ya Ofisi ya Kamati ya Ukombozi ya OAU ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95 na kuanzishwa kwa makumbusho ya kisasa kuhusu historia ya Bara la Afrika; Elimu ya uzalendo wa kuenzi na kuhifadhi kumbukumbu za harakati za ukombozi wa Bara la Afrika imeendelea kutolewa kwa zaidi ya watu milioni mbili (2) kutoka ndani na nje ya Tanzania kupitia mitandao ya kijamii, makongamano, matamasha, makala jongefu na mijadala bayana. Jumla ya shilingi milioni 515 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 4353: Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa majengo sita (6), ikiwemo mifumo ya maji safi na maji taka, umeme na mtandao; kuendelea na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuanzisha kituo cha redio na televisheni; kuendelea na ujenzi wa jukwaa la

kuendeshea Tamasha ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98; kununuliwa kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia; na kufanyika kwa Tamasha la 41 la Kimataifa la Utamaduni na Sanaa Bagamoyo. Jumla ya shilingi bilioni 1.19 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 6502: Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.07 kwa wasanii na wadau 45 waliokidhi vigezo; kuanza kwa hatua za utoaji wa mikopo kupitia benki za bishara ambapo makubaliano yamesainiwa na benki za NBC na CRDB na jumla ya shilingi bilioni 1.33 zimewekwa katika benki husika kwa ajili ya kukopesha wanatasnia za utamaduni na sanaa; na kutolewa kwa mafunzo kwa wasanii 6,511. Jumla ya shilingi bilioni 2.40 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 6385: Ujenzi wa Chuo cha Michezo cha Malya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 68; na kukamilika kwa michoro na kutangazwa kwa zabuni ya ujenzi wa kituo cha kukuza na kuendeleza vipaji (Sports Academy). Jumla ya shilingi bilioni 1.34 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 6523: Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa Mshauri Elekezi wa ukarabati wa kiwanja cha Benjamini Mkapa na Uhuru na kuandaliwa kwa makadirio ya majenzi (BOQ) na michoro ambapo kwa ujumla ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa umefikia asilimia 5; na kukamilika kwa ukarabati mdogo wa miundombinu ya eneo changamani la michezo. Jumla ya shilingi bilioni 1.06 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(vi) Mradi Na. 6521: Kuimarisha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kukiuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanzishwa kwa vituo 30 vya kufundisha Kiswahili katika Balozi za Tanzania Abu Dhabi, Uholanzi, Zimbabwe, Cuba, Ufaransa na Saudi Arabia na ndani ya nchi; kuendesha darasa la kwanza la Kiswahili nchini Malawi katika Chuo Kikuu cha Hebron; kushiriki na kutoa mada ya ubidhaishaji wa Kiswahili katika Kongamano la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) lililofanyika nchini Burundi; kuendesha Kongamano la Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) lililofanyika Chuo Kikuu cha HOWARD nchini Marekani; na kufanyika kwa maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Kiswahili Duniani jijini Dar es Salaam. Jumla ya shilingi milioni 300 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(vii) Mradi Na. 6527:Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalumu za Michezo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa tathmini ya shule 56 za sekondari zilizoteuliwa kuwa shule maalum za michezo; kununuliwa kwa vifaa vya michezo; na kuanza kwa

maboresho ya miundombinu ya michezo katika shule 56 za Sekondari katika mikoa ya Tabora, Tanga, Arusha, Pwani, Dodoma na Mtwara. Jumla ya shilingi milioni 767.88 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(viii) Mradi Na. 6504:Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi Pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Sports Arena (Dar es Salaam na Dodoma)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa vituo vya mazoezi na kupumzikia wananchi katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 25 na asilimia 5 mtawalia; kupatikana kwa eneo la ekari 12 kwa ajili ya ujenzi wa Arena ya Michezo Dar es Salaam lililopo Kawe, Tanganyika Packers. Jumla ya shilingi bilioni 6.27 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**C. Sekta ya Fedha, Biashara na Masoko**

**(i) Benki ya Maendeleo TIB**

Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi kufikia Juni 2023, Benki ya Maendeleo TIB ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 14.09 ambayo ipo kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii zikiwemo kilimo miradi mitano (shilingi milioni 993.28), umeme mradi mmoja (shilingi milioni 204.34), Taasisi za fedha miradi mitatu (shilingi bilioni 2.03), Milki halisi (Real Estate) mradi mmoja (Shilingi milioni 488.32), Madini mradi mmoja (shilingi bilioni 1.60), Utalii miradi miwili (shilingi bilioni 2.91), Mikopo binafsi mia moja na ishirini na nane (shilingi bilioni 2.17), Maji Mijini na Vijijini miradi miwili (shilingi bilioni 3.69). Kati ya miradi hiyo, asilimia 73.82 ni miradi ya sekta binafsi na asilimia 26.18 ni miradi ya sekta ya Umma.

**(ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – TADB**

Hatua Iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo ya moja kwa moja yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 151.7 katika sekta ya kilimo. Kiasi hicho kilitolewa kuwezesha shughuli mbalimbali za kilimo, ikiwemo pembejeo za kilimo, zana za kilimo, mikopo ya mashine, mikopo ya maghala, ujenzi wa viwanda na ununuzi wa mifugo. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Agosti, 2023, benki imetoa mikopo ya moja kwa moja yenye thamani ya shilingi bilioni 46.859.

**(a) Huduma za Bima**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandikishwa na kutolewa kwa leseni 1,324 zikijumuisha Kampuni 33 za bima, Kampuni tatu (3) za bima mtawanyo (Reinsurance), madalali sita (6) wa bima mtawanyo, madalali 100 wa bima, wakala 930 wa bima na benki wakala 31 (bancansurance), watoa huduma ya bima kidigitali tisa (9), watakwimu bima wanne (4), Wachunguzi binafsi wa bima (Private Insurance investigators) watatu (4); wakadiriaji hasara wa bima 46; na Maafisa Wauza Bima 100. Aidha, Mamlaka iliendelea kufanya ukaguzi kwa watoa huduma za bima ambao ni makampuni ya bima 12, matawi ya kampuni 4 za bima, madalali wa bima 12; benki wakala 26; Watoa huduma za bima kidijitali (IDPs) 4 na mawakala wa bima 369; kufanya ukaguzi wa bima kwa vyombo vya moto 33,160,000; na kupokea

malalamiko/madai 643 ambayo yalishughulikiwa ambapo malalamiko 76 yalipatiwa ufumbuzi na kulipwa, 16 yalikataliwa, matatu (3) yalipelekwa mahakamani, 14 yalipelekwa kwa Msuluhishi wa Migogoro ya Bima na 534 bado yanaendelea katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

**(b) Huduma Jumuishi za Fedha**

Katika kipindi cha mwaka 2022/23 Benki Kuu iliendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kuwa huduma za kifedha zinawafikia wananchi wengi na kwa gharama nafuu. Hatua zilizofikiwa ni pamoja na kukamilisha utafiti wa huduma za fedha wa mwaka 2023 (Tanzania Finscope Survey, 2023) ambao ulibainisha kuwa asilimia ya watu wazima wanaotumia huduma za fedha imeongezeka toka asilimia 65 mwaka 2017 hadi asilimia 76 mwaka 2023. Utafiti huo pia ulibainisha kuwa watanzania wengi wanazifikia na kutumia huduma za fedha kupitia simu za mkononi.

**(c) Huduma ndogo za Fedha**

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2022/23, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kusimamia na kusajili watoa huduma ndogo za kifedha ambapo ya leseni 1,307 zilitolewa kwa watoa huduma Daraja la Pili, leseni 801 kwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo, na kusajili Vikundi 42,257 vya Kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha. Aidha, hadi mwishoni mwa mwezi Juni 2023, Watoa huduma ndogo za fedha Daraja la Pili wamekopesha mikopo yenye thamani ya shilingi billioni 915 kwa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini.

**(d) Mradi Na. 6251: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uundwaji na kuanza kutumika kwa moduli mbili za Mfumo wa Usimamizi wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya mtandao (NeST); kukamilika kwa uandaaji wa Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini (Monitoring and Evaluation Guideline) kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na taasisi anazozisimamia; kufunga na kuunganishwa mfumo wa MUSE na mifumo mingine sita (6) ambayo ni GePG, PlanRep–TR, PlanRep – LGA, ERMS na mifumo ya benki za biashara (CRDB na NMB); kuunganishwa na kufungamanishwa kwa Mfumo wa Ufuatiliaji na Uchambuzi wa Taarifa za Fedha na mifumo ya PlanRep - TR na MUSE; kuendelea na uundaji wa mfumo wa ukusanyaji wa gawio na fedha taslim kutoka Taasisi na Mashirika ya Umma; kuandaa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI); kuhuisha Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato katika Serikali za Mitaa (TAUSI) na kuhuishwa kwa Mfumo wa Kihasibu wa Kuripoti Mapato na Matumizi katika Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS); kuandaa Mfumo wa Kusimamia Viashiria Hatarishi (GERMIS); kuandaa mahitaji ya Mfumo wa Huduma Ndogo za Kifedha; kukamilika kwa ukarabati wa Ofisi za Hazina Ndogo katika mikoa Kigoma, Kagera na Ruvuma. Jumla ya shilingi bilioni 14.8 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 900 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(e) Mradi Na. 6244: Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea ujenzi wa miradi 26 ya kimkakati katika Halmashauri 23 ambapo miradi 20 imefikia hatua ya ukamilishaji (miradi 13 kati ya hiyo imeanza kutoa huduma ikiwemo Mradi wa Stendi ya Mabasi ya mbezi luis katika Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo, Mradi wa Soko la Kimataifa la Kakoizi na Mradi waKiwanda cha Chumvi katika Wilaya ya Momba, Mradi wa Maegesho ya Malori na Mradi wa Stendi ya Mabasi katika Halmashauri ya Mji Tunduma na Mradi wa Stendi ya Mabasi katika Halmashauri ya Jiji Mwanza) na miradi saba (7) ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Jumla ya shilingi bilioni 27.74 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 13.65 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**D. Masoko**

**(a) Soko la Bidhaa Tanzania – TMX**

Soko la Bidhaa Tanzania lilianza rasmi mauzo ya bidhaa kwa majaribio mwaka 2019, Soko la Bidhaa liliwezesha biashara ya zao la ufuta katika wilaya za Kondoa na Babati ambapo jumla ya Tani 520 ziliuzwa. Kufuatia mafanikio hayo, mwaka 2020, mauzo yaliongezeka kufikia Tani 41,164 ikiwa ni ongezeko la baadhi ya mikoa kwa zao la Ufuta, dengu, choroko na Korosho. Msimu wa mwaka 2021, Soko la Bidhaa lilitegemea ongezeko zaidi la Bidhaa kwa wingi kwa Mazao yaliyofanyiwa majaribio na kuonesha mafanikio makubwa na badala yake kutokana na changamoto mbalimbali za wadau wakiwemo wafanyabiashara, Mazao hayo hayakuweza kuuzwa kama ilivyotarajiwa.

Hatua iliyofikiwa ni: Kuuzwa kwa tani 47,237.15 za Kahawa (Kagera) kwa thamani ya shilingi bilioni 105.82, tani 219.3 za ufuta kwa shilingi bilioni 0.65 na tani 1066.1 za kakao kwa shilingi bilioni 6.42; kuendelea na maandalizi ya kuuza mifugo hai (ngómbe, mbuzi na kondoo) na ngozi zinazotokana na Wanyama hao; kuanza kwa maandalizi ya kuuza madini ya vito. Aidha, Soko la Bidhaa kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba, Bodi ya Usimamizi Stakabadhi za Ghala na Tume ya Maendeleo ya Ushirika linaendelea na maandalizi ya kuuza pamba kupita Soko la Bidhaa Tanzania ambapo mizani ya kidigitali inaendelea kufungwa katika vyama vya msingi vya ushirika ili kukidhi matakwa ya kuweza kuuza kupitia Soko la Bidhaa.

Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania linakumbwa na changamoto kubwa ya kuuzwa kwa mazao ambayo tayari yameimarika katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Mazao hayo ni pamoja na korosho, ufuta, soya, kakao, mbaazi na choroko. Mazao haya tayari yamekwisha imarika katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na ni mazao yenye uzalishaji mkubwa ambapo yangeuzwa kupitia Soko la Bidhaa yangechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha kipato cha mkulima, upatikanaji wa fedha za kigeni na hatimaye kuchangia katika uchumi wa taifa. Katika kukabiliana na changamoto hizo, inapendekezwa kutolewa kwa tamko la kisera litakaloruhusu mazao yaliyo katika

Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania, kujumuisha bidhaa nyingine za mifugo, misitu na madini ili yawewe kuuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania na kuunganisha sheria inayosimamia Stakabadhi za Ghala na Sheria ya Masoko ya Bidhaa.

### 2.3.4. Kukuza Biashara na Uwekezaji

#### 2.3.4.1. Huduma za Biashara na Masoko

**Mradi Na. 6260: Mradi wa Kuwezesha Taasisi**

**(a) Uendelezaji wa Masoko ya Bidhaa**

Hatua iliyofikiwa ni kujengea uwezo wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika mikoa. Jumla ya shilingi milioni 300 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Kuimarisha Maendeleo ya Soko la Ndani na Nje - TANTRADE**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanikisha mauzo ya tani 147,061 za mazao yakiwemo zabibu, muhogo, mchele, asali, nyama yenye thamani ya shilingi bilioni 208.2 ambazo ziliuzwa kwa wanunuzi wa ndani na nje; kuzinduliwa kwa Mfumo wa *TanTrade Biashara Mobile App* unaowezesha wafanyabiashara kupata taarifa za masoko; kufanyika kwa tafiti ya masoko katika nchi ya Zambia; kuratibiwa kwa misafara ya kibiashara katika nchi za Malawi na Sudani Kusini ambapo mauzo ya Dola za Marekani 100,000 yalifanyika pamoja na miadi ya biashara yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 15.4 kwa mauzo ya bidhaa na mazao; kuratibiwa kwa Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yaliyohusisha washiriki 3,500 (kampuni za ndani 3,233 na kampuni za nje 267 kutoka nchi 19), watembeleaji 300,701, kupatikana kwa mauzo yenye jumla ya shilingi bilioni 3.9, na mikataba ya kibiashara yenye thamani ya shilingi bilioni 16.98 ilisainiwa; na kujenga uelewa kwa wafanyabiashara katika mikoa ya Ruvuma, Kigoma na Mwanza kuhusu fursa zinazopatikana katika Eneo la soko huru la Biashara Afrika (AfCFTA). Jumla ya shilingi milioni 694 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 322 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(c) Kuendeleza Biashara Kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa majengo na ujenzi wa uzio mpya wenye urefu wa mita 716 katika Kampasi ya Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa mradi wa jengo la ghorofa 10 la vipimo na viwango katika Kampasi Kuu ya Dar es salaam ambapo utekelezaji umefikia asilimia 5. Jumla ya shilingi milioni 638.16 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 1.04 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(d) Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa – TBS**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa usanifu wa jengo na miundombinu katika eneo la ujenzi wa maabara na ofisi katika Kanda ya Ziwa (Mwanza); na kuendelea na utafiti wa utengenezaji vinasaba ambavyo vitatumika kwenye mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa. Shughuli nyingine iliyofanyika ni: Kuendelea na ujenzi wa maabara na ofisi katika Kanda ya Kati (Dodoma) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 45. Jumla ya shilingi bilioni 4.14 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(e) Kuendeleza Biashara Kupitia Wakala wa Vipimo (WMA)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya makao makuu ya Wakala wa Vipimo Mkoa wa Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70.75; kuanza kwa taratibu za ununuzi wa vifaa 30 kwa ajili ya kupima na kuhakiki usahihi wa Mita za Taxi (Taxi Meter); kuanza kwa taratibu za ununuzi wa *flow meter* tatu (3) za kuhakiki mita za mafuta kwenye maghala ya mafuta na migodini. Jumla ya shilingi bilioni 2.73 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(f) Kuendeleza Biashara kupitia Tume ya Ushindani (FCC)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za Utafiti katika Sekta ndogo ya miamala ya Fedha kwa ajili ya kutambua kama kuna ukiukwaji wa misingi ya ushindani; na kuendelea na hatua mbalimbali za uandaaji wa mfumo wa kielektroniki wa utoaji huduma. Jumla ya shilingi milioni 350 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(g) Kuendeleza Biashara Kupitia Baraza la Ushindani (FCT)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Mfumo wa Baraza wa Uwasilishaji, Upokeaji, Usajili na Usikilizaji wa Kesi kwa njia ya mtandao (*FCT Appeals Management System*); kukamilika kwa uboreshaji wa Maktaba na Ofisi ya Kumbukumbu ya Baraza la Ushindani; kununuliwa kwa magari mawili (2); na kukamilika kwa uboreshaji wa Ofisi ya Baraza na *Court* ili kuboresha shughuli za Ofisi na uendeshaji wa kesi/mashauri. Jumla ya shilingi milioni 605.09 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**Kuimarisha na Kukuza Ushiriki wa Sekta Binafsi**

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi nchini ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa ndani ya nchi, kuongeza mauzo nje na kuzalisha ajira. Viwanda hivyo ni pamoja na: Kiwanda cha sukari Bagamoyo ambacho kinazalisha tani 30,000 za sukari kwa mwaka na kutoa ajira 600; kiwanda cha sukari cha Kagera ambacho kimeongezewa uwezo kwa kufungwa vinu vipya viwili (2) na hivyo kuongeza uzalisha wa sukari kutoka tani 84,000 hadi tani 123,190 kwa mwaka na kuzalisha ajira 11,103; Kuondoa na kupunguza ada, tozo na faini 106; na kurekebisha sheria 27 zinazolenga kuondoa kodi, ada na tozo. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

**(a) Kukuza Ushiriki wa Watanzania na Kampuni za Ndani katika Miradi ya Kimkakati**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji taarifa za ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati katika mikoa tisa (9) ambapo imebainika kuwa ajira 145,245 zilizalishwa katika miradi mikubwa ya kimkakati; kuandaliwa kwa kanzidata ya watoa huduma katika miradi ya kimkakati na uwekezaji na kuihuisha na mifumo mingine ya kanzidata za Serikali ikiwemo BRELA, TIC, TRA na NIDA; kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika shughuli za uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia nchini ambapo kampuni saba (7) zinashiriki; na kusajiliwa kwa kampuni 1,971 za ndani kwenye Mfumo wa *Common Qualification System (CQS)* kwa ajili ya kupatiwa kipaumbele cha fursa zilizopo kwenye miradi ya mafuta na gesi.

**(b) Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja (One Stop Facilitation Centre - OSC)**

Serikali imeendelea kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Msukumo wa kipekee ulitolewa katika utekelezaji na ugharamiaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambapo sekta binafsi ilipewa jukumu la kuchangia shilingi trilioni 40.6. Aidha, ili kufikia azma hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuiwezesha sekta binafsi kubuni na kutekeleza miradi katika sekta za uchumi ikiwemo viwanda, kilimo, uzalishaji na mifugo. Hatua hizo ni pamoja na:

(a) Kuboresha utoaji huduma za uwekezaji kupitia dirisha la Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja (*One Stop Facilitation Centre - OSC*). Jumla ya wateja 13,836 walihudumiwa na miradi 240 imesajiliwa (miradi 94 wageni, 89 watanzania, 57 ubia kati ya wageni na watanzania) yenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,387.17 na inatarajiwa kutoa ajira kwa watanzania wapatao 39,243. Kati ya miradi 240 iliyosajiliwa, miradi 187 sawa na asilimia 77.9 imeanza utekelezaji kwenye sekta za Kilimo (18), majengo ya biashara (10), miundombinu (2), rasilimali watu (5), viwanda (101), huduma (5), mawasiliano (1), utalii (9) na usafirishaji (36);

(b) Utoaji leseni za viwanda vipya: Serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetoa leseni za viwanda vipya 193 kwa kipindi mwaka 2022/23 na leseni 58 kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

(c) Serikali imeendelea kuimarisha majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi kupitia mabaraza ya biashara ya mikoa na wilaya ambapo Serikali imewezesha kufanyika kwa mikutano katika mikoa 13; na kufanyika kwa Mkutano wa 35 wa Kamati Tendaji ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) na Mkutano wa 13 wa Baraza la Taifa la Biashara;

(d) Kufanyika kwa vikao vinne (4) na vyama mwavuli vya sekta binafsi; kufanyika kwa utambuzi wa muundo wa sekta binafsi nchini ambapo jumla ya Kampuni 488 zenye ukomo wa ahadi zimesajiliwa BRELA na Jumuiya za Biashara 22

zimesajiliwa na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya nchini; kufanyika kwa tathmini ili kubaini mchango wa sekta binafsi kupitia sekta mbalimbali katika uchumi.

Jumla ya shilingi bilioni 4.3 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 332 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**Ujenzi wa Vituo vya Uwezeshaji**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kutoa mafunzo na kuratibu utendaji wa vituo 17 vya uwezeshaji; na ukarabati wa vituo vitatu (3) vya uwezeshaji vya Mbinga (Ruvuma), Malele (Rukwa) na Nyangwale (Geita) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 33. Jumla ya Shilingi milioni 664 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

#### 2.3.4.2. Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji

**A. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa Sheria ya uwekezaji namba 10 ya mwaka 2022 na Kanuni za Uwekezaji Tanzania za mwaka 2023; kukamilika kwa rasimu ya maboresho ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji; kurekebishwa kwa tozo, ada na faini 106 zinazoweka vikwazo katika mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji; kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Mfumo wa Pamoja wa Huduma kwa Wawekezaji Tanzania (TeIW); kufanyika kwa makongamano kumi (10) kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa mitaji kutoka nje (FDI); Kusainiwa kwa Hati 50 za Makubaliano zenye lengo la kuvutia uwekezaji kutoka nje kwa kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini; na kuanza uendelezaji wa Kongani ya Viwanda ya Kwala ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30.

**B. Kuratibu, kuhamasisha, Kutangaza na Kuwezesha uwekezaji**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa Mfumo wa kukusanya mapato ya ardhi (land rent) yatokanayo na Hati isiyoasili (deliverative rights); kupatikana kwa hati zisizo za asili 601 za mashamba na viwanja zenye ukubwa wa hekta 456,601.254 kwa ajili ya uwekezaji; kuendelea na uhakiki wa hekta 13080.08 zilizopokelewa kutoka kwa watu binafsi; kuendelea kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye hekta 56,900 ardhi zilizopokelewa kutoka Taasisi na Mashirika ya Umma na hekta 78,144.35 zinazomilikiwa na Kituo cha Uwekezaji; na kukamilika kwa ujenzi na uunganishwaji wa mfumo wa *interactive map and dashboard* katika mashamba matatu (3) yaliyopo Uvinza (Kigoma), shamba la Mkulazi (Morogoro) na Kiwanja kilichopo Arusha.

**C. Ushirikiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia**

**(i) Mradi Na. 6391: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Vitega Uchumi, Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini**
Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa majengo matano (5) katika Ubalozi

wa Tanzania Lusaka (Zambia); jengo la kitega uchumi na makazi ya watumishi katika Ubalozi wa Tanzania Harare (Zimbabwe), majengo matatu (3) ya makazi ya watumishi katika Ubalozi wa Tanzania Lilongwe (Malawi), jengo la Makazi ya Mkuu wa Utawala (HOC) eneo la Masvagen 28 Ubalozi wa Tanzania Stockholm (Sweden), na Makazi ya Balozi eneo la Avenue Wellington 150 Ubalozi wa Tanzania Brussels (Ubelgiji); kuendelea na ukarabati wa majengo manne (4) katika Ubalozi wa Tanzania Pretoria (Afrika Kusini) ambao umefikia asilimia 15, jengo la Makazi ya Balozi eneo la Vedettvagen 26 Ubalozi wa Tanzania Stockholm umefikia asilimia 90, jengo la zamani la ofisi katika ubalozi wa Tanzania Washington D.C (Marekani) umefikia asilimia 14.94; kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa majengo na kitega uchumi katika Balozi za Tanzania Kinshasa (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) na Nairobi (Kenya); kutangazwa kwa zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa (Ethiopia) na ujenzi wa majengo kumi (10) ya kimkakati katika Ubalozi wa Tanzania Lusaka (Zambia). Shughuli nyingine ni kununuliwa kwa jengo la Mkuu wa Utawala na Fedha katika Ubalozi wa Tanzania, Berlin (Ujerumani). Jumla ya shilingi bilioni 8.74 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

**Upanuzi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara kwenye Chuo cha Diplomasia ambapo utekelezaji umefikia asilimia 18. Jumla ya shilingi milioni 663.00 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 6317: Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki na Binadamu katika eneo la Lakilaki Jijini Arusha ambapo utekelezaji upo katika hatua za awali ikiwa ni pamoja na kukamilisha upimaji wa udongo katika eneo la mradi pamoja na kufanyika kwa malipo ya awali. Jumla ya shilingi bilioni 8.3 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

### 2.3.5. Kuchochea Maendeleo ya Watu

#### 2.3.5.1. Afya

**(a) Mradi Na. 5487: Hospitali ya Taifa ya Muhimbili**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa utengenezaji wa mfumo mpya wa utoaji huduma kupitia TEHAMA; kukamilika kwa ukarabati wa vyumba vitano (5) vya ICU, vyumba vya radiolojia (MRI 1, CT SCAN 1 na X-Ray 2) na Hospitali ya watoto pamoja na upanuzi wa jengo la OPD; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wodi maalum kwa wagonjwa binafsi na wagonjwa mashuhuri ambapo awamu ya kwanza ya utekelezaji imefikia asilimia 85. Jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 6364: Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha upandikizaji viungo na sehemu ya kufulia nguo, wodi ya kawaida ya watoto, wodi ya mama wajawazito mahututi, wodi ya uangalizi maalumu wa mama wajawazito (HDU) na chumba maalum kwa ajili ya kufanya matengenezo ya vifaa tiba (biomedical workshop); kukamilika kwa ukarabati wa wodi za watoto wachanga mahututi (NICU); kutolewa kwa huduma za uchunguzi za kibingwa ambapo jumla ya vipimo vya maabara 11,096 (Plain X-Ray 3,070, CT Scan 2,601, USS 4,055, MRI 720, loroscopy 507 na mammography 223) vilifanyika; na kuwezesha mafunzo ndani na nje ya nchi kwa watumishi 82 katika fani mbalimbali za kibingwa katika masomo ya uzamili.

Aidha, hospitali imetoa huduma mpya za kupunguza uzito kwa kuwekewa puto (Intragastricballoon) ambapo jumla ya wagonjwa 114 wamepatiwa huduma hiyo na upandikizaji wa uloto (bone marrow transplant) ambapo wagonjwa 11 wamehudumiwa. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 5491: Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ununuzi wa vifaa tiba (Vipandikizi) na utoaji wa huduma za tiba kwa njia ya mkoba (Outreach Program) ambapo jumla ya wateja 4,528 walipatiwa huduma hiyo katika Hospitali za Mikoa ya Mtwara, Lindi na Dar es Salaam. Jumla ya shilingi milioni 500 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 5419: Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) ambapo huduma zimeanza kutolewa. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 5412: Taasisi ya Saratani Ocean Road**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, chumba cha MRI, na chumba cha tiba mtandao; kufungwa kwa mashine ya PET/CT SCAN; na kununuliwa na kusimikwa kwa mashine mbili (2) za LINAC na mbili (2) za COBALT. Jumla ya shilingi bilioni 4.0 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 5424: Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa Ambukizi – Kibong’oto (Kilimanjaro)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na jengo la utawala; kuendelea na ujenzi wa maabara ya Kisasa (BSL 3) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98; na kuendelea na ujenzi wa jengo la Radiolojia kwa ajili ya kusimika CT-Scan ambapo utekelezaji umefikia asilimia 67. Jumla ya shilingi bilioni 1.3 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na 5425: Hospitali ya Rufaa ya Afya ya Akili Mirembe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba ya Mtumishi - Hombolo; kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99 na jengo la huduma za dharura (EMD) asilimia 98; na kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 14 katika fani za kibingwa katika vyuo vya ndani na nje. Jumla ya shilingi bilioni 4.0 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 5426: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Ziwa, Bugando**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa majengo ya wagonjwa mahututi (chumba cha wagonjwa mahututi, chumba cha wagonjwa mahututi wa upasuaji na chumba cha watoto wachanga wanaohitaji uangalizi maalum). Jumla ya shilingi milioni 997.0 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 5427: Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi; na kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za tiba - mionzi kwa matibabu ya magonjwa ya kansa (Radiotherapy) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 69. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(j) Mradi Na. 5422: Hospitali ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za uzazi katika eneo la Meta; ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU), jengo la huduma za dharura (EMD) na chumba cha tiba mtandao; kununuliwa kwa vifaa tiba ikiwemo *patient monitors* (18), Vitanda (104), na Bed Lockers (100). Jumla ya shilingi bilioni 1.12 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(k) Mradi Na. 5428: Hospitali ya Benjamini Mkapa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa chumba cha kutolea tiba mtandao na jengo la huduma za CT - Scan; kuanza kutolewa kwa huduma ya upandikizaji wa Uloto (Bone marrow Transplant) ambapo wagonjwa watatu (3) wamehudumiwa; kukamilika kwa upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU); na kuendelea na ujenzi wa jengo la Tiba Mionzi (Radiotherapy) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 24. Jumla ya shilingi bilioni 3.1 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(l) Mradi Na. 5408: Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Burigi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa awamu ya tatu (3) ya ujenzi wa nyumba 20 za watumishi, njia za kupita wagonjwa na barabara za ndani ya eneo la Hospitali, jengo la huduma za uchunguzi kwa njia ya mionzi (Radiolojia) awamu ya kwanza, jengo la mashine ya kufua umeme (power house) na ujenzi wa jengo la ghorofa mbili (2) la wodi; kuendelea na ujenzi wa uzio na jengo la huduma za uchunguzi kwa njia ya mionzi (Radiolojia) awamu ya pili ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85 na asilimia 72 mtawalia. Jumla ya shilingi bilioni 3.7 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(m) Mradi Na. 5423 Hospital ya Rufaa ya Kanda ya Kusini - Mtwara**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU), nyumba ya mtumishi na ukarabati wa chumba cha tiba mtandao; na kuendelea na ujenzi wa Jengo la Huduma za Dharura (EMD) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80 na jengo la OPD umefikia asilimia 91. Jumla ya shilingi bilioni 3.9 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(n) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni:

**(i)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Njombe:** Kukamilika kwa nyumba ya mtumishi na ukarabati wa jengo la huduma za CT-Scan. Jumla ya shilingi bilioni 2.2 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(ii)** **Hospitali ya Mkoa Simiyu:** Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 88, jengo la wagonjwa mahututi (asilimia 97), jengo la huduma za dharura (asilimia 97) na nyumba ya mtumishi (asilimia 99). Jumla ya shilingi bilioni 1.3 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(iii)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita:** Kuendelea na ujenzi wa jengo la Afya ya Uzazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 45, jengo la wagonjwa wa nje (asilimia 99.5), jengo la wagonjwa mahututi (asilimia 98) na jengo la huduma za dharura (asilimia 98); na kukamilika kwa nyumba ya mtumishi. Jumla ya shilingi bilioni 3.8 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(iv)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songwe:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la OPD; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90, jengo la huduma za dharura (asilimia 89) na jengo la huduma za afya ya uzazi (asilimia 55). Jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(v)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi:** Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba ya mtumishi, majengo ya uchunguzi na afya ya uzazi, miundombinu ya ICT, HVAC, Lift, Hewa Tiba, chumba cha tiba mtandao, jengo la OPD na jengo la huduma za *CT-Scan*; na kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za dharura na jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99. Jumla ya shilingi bilioni 12.9 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(vi)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida (RRH):** Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la huduma za CT – Scan, chumba cha tiba mtandao, na ujenzi wa nyumba ya mtumishi; na kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za dharura na jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90. Jumla ya shilingi bilioni 7.4 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(vii)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za CT-Scan, jengo la wagonjwa mahututi, jengo la huduma za dharura na nyumba ya mtumishi. Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimetumika katika mwaka 2022/23**;**

**(viii)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mara:** Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba mbili (2) za watumishi; kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98 na jengo la huduma za dharura (asilimia 40). Jumla ya shilingi bilioni 1.0 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(ix)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Arusha (Mount Meru):** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, chumba cha tiba mtandao na jengo la huduma za CT - Scan na ujenzi wa nyumba ya mtumishi. Jumla ya shilingi bilioni 3.2 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(x)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwanza (Sekou Toure):** Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la huduma za CT-Scan, chumba cha tiba mtandao na nyumba ya mtumishi. Jumla ya shilingi milioni 537 zimetumika katika mwaka 2022/23;

**(xi)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Mwananyamala:** Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za dharura, ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi na ukarabati wa jengo la huduma za X-ray. Jumla ya shilingi bilioni 3.23 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(xii)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Temeke:** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la huduma za dharura na jengo la huduma za CT – Scan; na kuendelea na ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi ambao utekelezaji umefikia asilimia 96. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 zimetumika kwa mwaka 2022/23;

**(xiii)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Pwani (Tumbi):** kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, jengo la huduma za dharura, jengo la huduma za CT – Scan na ujenzi wa nyumba ya mtumishi. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 zimetumika kwa mwaka 2022/23;

**(xiv)** **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kigoma (Maweni): Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la** kuhifadhia maiti, nyumba ya mtumishi na ukarabati wa chumba cha tiba mtandao; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi, jengo la huduma za CT-Scan na huduma za dharura ambapo utekelezaji wa majengo hayo umefikia asilimia 99 na jengo la OPD asilimia 95. Jumla ya shilingi milioni 400 zimetumika katika mwaka 2022/23;

(xv) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kilimanjaro (Mawenzi):** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, jengo la huduma za dharura na ujenzi wa nyumba ya mtumishi; na kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 zimetumika katika mwaka 2022/23;

(xvi) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Manyara:** Kukamilika kwa ukarabati wa chumba cha tiba mtandao na nyumba ya mtumishi na ujenzi wa jengo la kutolea huduma za CT – Scan; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa Nje (OPD) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99, jengo la Damu Salama (asilimia 75), wagonjwa mahututi (asilimia 88) na huduma za dharura (asilimia 80). Jumla ya shilingi bilioni 3.5 zimetumika katika mwaka 2022/23;

(xvii) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mbeya:** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, ujenzi wa nyumba ya mtumishi na jengo la huduma za CT-Scan; na kuendelea na ujenzi wa jengo la upasuaji (theatre & CSSD) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 zimetumika katika mwaka 2022/23;

(xviii) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mtwara:** Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la huduma za CT - Scan. Jumla ya shilingi bilioni 2.2 zimetumika katika mwaka 2022/23;

(xix) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma:** Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la huduma za dharura, ujenzi wa nyumba ya mtumishi, ujenzi wa jengo la huduma za CT - Scan na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 zimetumika katika mwaka 2022/23;

(xx) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Tanga: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za CT-**Scan, ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa mahututi, jengo la huduma za dharura na chumba cha tiba mtandao pamoja na ujenzi wa nyumba ya mtumishi. Jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika katika mwaka 2022/23; na

(xxi) **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kagera**: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi, ujenzi wa jengo la huduma za dharura na jengo la huduma za CT - Scan na nyumba ya Mtumishi. Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(o) Mradi Na 2208: Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ya Taifa (NIMR)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa tafiti za afya za magonjwa 113 ya binadamu, utafiti hali ya maambukizi ya malaria nchini kwa kutumia mbinu za vinasaba katika mikoa 13 ya Tanzania Bara, utafiti wa usalama na ufanisi wa chanjo ya TANCoV

1.3.20 SARS-CoV-2, utafiti wa kuzuia ugonjwa wa kisukari Afrika, utafiti na uchunguzi wa Kifua Kikuu ili kukomesha Kifua Kikuu katika ukanda wa Afrika, na utafiti kuhusu kutathmini ya usugu wa vimelea vya ugonjwa wa malaria dhidi ya dawa ya mseto barani Afrika; uimarishaji uwezo wa mfumo wa afya na kupeleka afua ya *Praziquantel* ya watoto (Pediatric Praziquantel) kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa wa kichocho kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano; kufanyika kwa jaribio nasibu la awamu ya tatu ya dawa ya Metformin kwa watu walioambukizwa VVU wanaokaribia kupata ugonjwa wa kisukari; na kufanyika kwa utafiti wa vyakula tiba kwa ajili ya afya ya uzazi na kutatua mahitaji muhimu ya virutubisho na madini kabla na wakati wa ujauzito. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 katika mwaka 2022/23.

**(p) Mradi Na. 5444: Mradi wa Huduma za Bidhaa za Dawa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo kwa zahanati (5,892) na vituo vya afya (759) utekelezaji umefikia asilimia 54, hospitali za wilaya (225) (asilimia 62), hospitali za rufaa za mikoa (40) (asilimia 94); Hospitali za Kanda (6), Hospitali maalum (5) na ya Taifa utekelezaji wake umefikia asilimia 84. Aidha, ununuzi wa vifaa tiba vya afya ya kinywa na macho kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri 71, vifaa tiba vya zahanati 300 na vifaa tiba katika vituo vya Afya 159 vya tozo umekamilika. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya ambapo ujenzi wa Kiwanda cha kuzalisha mipira ya mikono (gloves) kilichopo Idofi mkoa wa Njombe kimefikia asilimia 85. Jumla ya shilingi bilioni 190.99 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 16.66 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(q) Mradi Na. 5432: Uimarishaji wa Huduma za Chanjo**

Hatua iliyofikiwa ni: kutolewa Chanjo kwa watoto (*surviving infants)* 2,318,004 ikilinganishwa na lengo la Watoto 2,166,170 sawa na asilimia 107 ambapo chanjo zilizotolewa ni chanjo ya Penta 3, chanjo ya Polio ya matone OPV3 asilimia 108, sindano (IPV) asilimia 109, Surua rubella 1 asilimia 113, Surua Rubella 2 asilimia 96, HPV1 asilimia 84 na HPV2 asilimia 64. Jumla ya shilingi bilioni 41.3 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(r) Mradi Na. 5492: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutoa huduma ya tiba na matunzo kwa watu wapatao 2,544,198; kutolewa kwa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ambapo vituo 7,386 sawa na asilimia 99 ya vituo vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto vinatoa huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT); kutolewa kwa huduma za upimaji VVU kwa wajawazito 2,464,099 kati ya 2,491,099 waliohudhuria kliniki ambapo wajawazito 70,754 sawa na asilimia 2.7 walibainika kuwa wanaishi na maambukizo ya VVU na kuanzishiwa dawa za ARV na kuzuia maambukizi kwenda kwa mtoto; kupimwa kwa Watoto 60,914 sawa na asilimia 80 ya Watoto waliozaliwa na akina mama wanaoishi na

VVU walipimwa kipimo cha kwanza cha uchunguzi wa maambukizi ya VVU katika umri wa miezi miwili ambapo asilimia 1 ya watoto hao walibainika kuwa na maambukizi. Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(s) Mradi Na.5498: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa na kusimikwa kwa mashine za kisasa aina ya Truenut 37 kwenye vituo vya afya 30 vinavyotoa huduma za Kifua Kikuu katika mikoa 24 ambapo jumla ya watu 1575 walipata huduma; kutolewa kwa huduma za mkoba kliniki tembezi (Mobile Vans outreach services) ambapo watu 8,298 walichunguzwa na kupimwa Kifua Kikuu; kutekeleza shughuli ya tambua TB ambapo jumla ya wagonjwa 155 sawa na asilimia 35 wa Kifua Kikuu Sugu waligundulika na kuanzishiwa matibabu; na kutolewa kwa tiba kinga ya ugonjwa wa Ukoma kwa makundi hatarishi ambapo watu 1,344 na ugawaji wa jozi za viatu 165 ili kupunguza athari za ulemavu kwa waathirika wa Ukoma. Jumla ya shilingi bilioni 9.00 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(t) Mradi Na. 5406: Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza na Yasiyo ya Kuambukiza**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa wodi mbili (2) kwa ajili ya matibabu ya magonjwa hatarishi na milipuko katika Hospitali ya Kisopwa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60; na kuendelea na tathmini ya huduma za mionzi nchini katika hospitali tano (5) - BMH, Mbeya, ORCI, KCMC na Bugando ili kuangalia huduma zinazotolewa. Jumla ya shilingi bilioni 4.1 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(u) Mradi Na. 2204: Mafunzo na Maendeleo ya Wataalamu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati katika Chuo cha Tabora *Clinical Officers Training Centre*, Ngudu *School of Environmental Health Science*, Kilosa *Clinical Officers Training Centre*, Kagemu *Environmental Health Science*, Chuo cha Korogwe SON, Mtwara COTC na ujenzi wa Nachingwea SON umefika asilimia 48; kutolewa kwa ufadhili wa masomo kwa watumishi 457 kati yao watumishi 318 ni fani za ubingwa na ubobezi na watumishi 139 ni Mafunzo kwa mfumo wa Set. Jumla ya shilingi bilioni 45.5 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 8.1 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(v) Mradi Na. 5416: Mipango ya Afya na Uendeshaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwekwa kwa mfumo wa tiba mtandao, kununuliwa na kuanza kutumika kwa vifaa vya TEHAMA katika hospitali za kanda za Bugando na Benjamin Mkapa na hospitali tatu (3) za kibingwa (Muhimbili, MOI na JKCI) na hospitali maalum ya Ocean Road. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 zimetumika kwa mwaka 2022/23.

**(w) Mradi Na. 5401: Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali 12 na kuendelea na ujenzi

wa hospitali 47 za halmashauri; na kukamilika kwa ukarabati wa hospitali 10 kongwe na kuendelea na ukarabati wa hospitali tisa (9) za halmashauri. Jumla ya shilingi bilioni 57.24 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 30.69 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/34.

**(x) Mradi Na. 5429: Huduma ya Afya ya Msingi**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa zahanati 228 na kuendelea na ujenzi wa zahanati 72 katika Halmashauri zote nchini; kukamilisha ujenzi wa vituo viwili (2) vya afya katika Halmashauri za Wilaya za Msalala na Ukerewe; na kununuliwa kwa vifaa na vifaa tiba kwa vituo vya afya 296, zahanati 288 na hospitali za Halmashauri 69 zilizokamilika. Jumla ya shilingi bilioni 81.8 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 53.82 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/34.

**2.3.5.2. Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

**(i) Mradi Na. 6330: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa kumbi pacha za mihadhara zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,008, bweni la wasichana la ghorofa nne (4) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 568 na ununuzi wa samani (viti, vitanda na magodoro) kwa ajili ya kumbi pacha za mihadhara na hosteli iliyojengwa katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Jengo la Utawala lenye vyumba vya ofisi 17 na kumbi mbili (2) ndogo za mikutano zenye uwezo wa kuhudumia watu 40 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale; kukamilika kwa ukarabati wa jengo la utawala katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba, maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 120, ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 260, mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 kila moja na nyumba moja ya mtumishi; kukamilika kwa ufungaji wa mifumo ya TEHAMA, mashine za kiuhandisi (Poker Machines na Mobile Block Machines) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Mabughai); kuendelea na ujenzi wa Bwalo la Chakula lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60 na hosteli ya ghorofa mbili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole (asilimia 68); na ununuzi wa magari (Lori na pick up) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Mabughai. Jumla ya shilingi bilioni 4.65 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi Na. 6259: Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango ya Maendeleo**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na kuandaliwa kwa MTAKUWWA Awamu ya Pili; kukamilika kwa maandalizi ya Programu ya miaka mitano (2022 – 2026) ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kwenye Jukwaa la Kimataifa la Kizazi chenye Usawa; kuendelea na uidhinishwaji wa mapitio

ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) na Mkakati wa utekelezaji wake (2005) na Sera ya Taifa ya wazee (2003); kuanzishwa kwa Dawati la Jinsia katika Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (Saint John's University) na hivyo kufikisha idadi ya madawati 270 ya Jinsia yaliyoanzishwa mpaka sasa katika Vyuo Vya Elimu ya Juu na Kati; kufanyika kwa kampeni maalum ya kupinga ukatili dhidi ya watoto hususan ukeketaji katika mikoa ya Manyara na Mara yenye matukio mengi ya ukeketaji ambapo idadi ya watu waliotoa taarifa imeongezeka na kufikia 215,000 mwaka 2023 ukilinganisha na idadi ya watu 71,667 mwaka 2020; kukamilika kwa mfumo wa huduma kwa wateja unaotumika kutoa huduma zote za Wizara; kutolewa kwa mafunzo kwa waratibu 216 wa Dawati la Jinsia katika Mikoa sita (6) ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Mwanza, Geita na Shinyanga. Jumla ya shilingi bilioni 2.07 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi Na. 5414: Uhai na Maendeleo ya Mtoto**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kwa watumishi 3457 wakiwemo walimu, Maafisa Maendeleo ya jamii na Maafisa elimu kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Madawati ya Ulinzi na Usalama ya Watoto ndani na nje ya shule (2022); kuanzishwa kwa Madawati 1,852 ya ulinzi wa Mtoto katika shule za msingi (1,342) na sekondari (510); kutolewa kwa elimu ya uelewa katika jamii kuhusu Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/22 - 2024/25) kwa Waheshimiwa Wabunge 124, watumishi wa Wizara 44 na wataalamu 156 kwenye mikoa 10 ya Tabora, Lindi, Dar es saalam, Morogoro, Arusha, Manyara, Mbeya, Rukwa, Kagera na Dodoma; kutolewa mafunzo kwa wazazi 104 na vijana balehe 94 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya kuhusu Programu ya Malezi Jumuishi kwa Kundi la Vijana Balehe; na kuendelea na maandalizi ya Video fupi zenye ujumbe maalum ambazo zitatumika kwenye vyombo vya habari ikiwemo redio na Runinga kwa ajili ya kutoa tahadhari ya matumizi yasiyofaa ya mitandao ya kijamii kwa watoto, wazazi na jamii kwa ujumla. Jumla ya shilingi milioni 662.8 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi Na. 6290: Uchakataji wa Taarifa na Uandaaji Programu (Programming and Data Processing)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli, Mlale, Ruaha, Uyole, Taasisi ya Ustawi wa Jamii (Kampasi ya Kisangara) na Makazi ya Wazee Kibirizi (Kigoma), Kilima (Kagera) na Nandanga (Lindi). Jumla ya shilingi milioni 200 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 5451: Kuwezesha huduma za Ustawi wa Jamii**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ya makazi ya wazee ya Ipulli, Njoro na Misufini, Mahabusu ya watoto Mbeya na Arusha na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara. Jumla ya shilingi bilioni 1.09 zimetumika katika mwaka 2022/23.

#### 2.3.5.3. Elimu

**(a) Mradi Na. 4312: Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ualimu vya Singachini, Songea, Mamire, Katoke na Vikindu; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika shule za msingi na sekondari kama ifuatavyo: ujenzi wa shule mpya 40 za msingi, madarasa 96 ya shule za msingi katika shule 46, mabweni 4 katika shule za msingi tatu (3), nyumba saba (7) za walimu katika shule saba (7) za msingi, mabweni 62 katika shule za sekondari 44, madarasa 46 ya shule za sekondari katika shule 23, maabara 16 katika shule 9 za sekondari, maktaba 4 za sekondari, nyumba za walimu 13 katika shule za sekondari 22 ambapo utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 80; na ukarabati wa shule kongwe za msingi 45 na 16 Sekondari ( asilimia 80); kuendelea na ujenzi wa Chuo vya Ualimu Sumbawanga (asilimia 92), Muhonda (asilimia 92) na Dakawa (asilimia 90) na shule ya Mfano ya Sekondari Dodoma (asilimia 90); na kuwajengea uwezo maafisa 1,670 wa Uthibiti Ubora wa Shule kuhusu utekelezaji wa mtaala mpya. Jumla ya shilingi bilioni 65.7 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 4321: Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi (MMEM) LANES II**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa tathmini ya ubora wa shule kwa shule 7,133 Tanzania Bara ambapo asilimia 69 ya shule zote zimefanyiwa tathmini; kutoa Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA) kuhusu namna ya kufundisha wanafunzi kwa kufuata mtaala wa umahiri kwa viongozi wa kielimu 2,427, maafisa elimu kata 2,364, wathibiti ubora wa wilaya 21, walimu mahiri wa awali na msingi 3,690 na walimu wa wanafunzi wenye mahitaji maalum 972; uchapaji na usambazaji wa nakala 1,687,140 na 4,154,226 za vitabu vya kiada kwa darasa la III – V na darasa la I na II mtawaliwa, nakala 3,885,000 za vitabu vya ziada kwa ajili ya wanafunzi wa awali; kuratibu mafunzo ya mbinu za ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalum kwa mikoa ya Iringa, Lindi, Katavi, Songwe na Rukwa; kukamilika kwa ujenzi wa madarasa 182 ya awali ya mfano na kuendelea na ujenzi wa madarasa 140; kukamilika kwa hosteli moja (1) ya watoto wenye mahitaji maalum na kuendelea na ukamilishaji wa hostel tisa (9); na kukamilika kwa ukarabati wa vituo 208 vya mafunzo ya walimu (Teachers Resouces Centre – TRC) na kuendelea na ukarabati wa TRC 44. Jumla ya shilingi bilioni 26.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 4319: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (Boost Primary Student Learning)**

Kuendelea na ujenzi wa shule mpya 302 za msingi ambapo shule 95 sawa na asilimia 31 ujenzi umekamilika na shule 205 zipo hatua ya ukamilishaji na mbili hatua a msingi; kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwenye shule za msingi

zilizopo ambapo vyumba vya madarasa 1,838 kati ya 2,942 (62%), matundu ya vyoo 1,484 kati ya 2,923(51%) kwa Shule za Msingi, vyumba vya madarasa 230 kati ya 368(63%) ya mfano ya Elimu ya Awali, matundu ya vyoo 585 kati ya 1,104 (53%) vya wanafunzi wa Elimu ya Awali, vyumba vya madarasa 34 kati ya 40 (85%) vya wanafunzi wenye mahitaji maalum na nyumba za walimu 33 kati ya 41(80) ujenzi ulikuwa umekamilika; na kukamilika kwa ukarabati wa shule za msingi 4 chakavu.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kufanya tathmini ya mahitaji ya miundombinu kwenye Shule za Msingi 17,182 zilizopo katika Halmashauri zote; kutolewa kwa mafunzo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Maafisa Elimu wa Mikoa, timu za utekelezaji wa mradi ngazi za Mkoa na Halmashauri ambapo jumla ya watendaji 2,888 wamepatiwa mafunzo; kutoa Mafunzo ya Walimu Kazini (MEWAKA) kwenye shule za Msingi 2,952 kwenye Halmashauri 26 (Halmashauri 1 kila Mkoa) za majaribio; na kukamilika kwa uaandaji wa miongozo ya utawala bora na kiongozi cha usimamizi wa shule pamoja na moduli 12 za mafunzo endelevu ya walimu kazini. Jumla ya shilingi bilioni 265.08 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 3280: Programu ya Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa matundu 7,587 ya vyoo, sehemu za kunawia mikono 2,980 na uwekaji wa matenki 1,338 ya kuhifadhia maji katika shule za msingi 446 za halmashauri 86 za Tanzania Bara ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98; kuendelea na ujenzi wa matundu 1,742, miundombinu ya kunawia mikono 660 miundombinu ya kuvunia maji ya mvua na ununuzi wa matanki ya kuhifadhia maji 306 katika shule za msingi 102 katika mikoa nane (8) na halmashauri 51. Jumla ya shilingi bilioni 20.3 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4390: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza ujenzi wa shule mpya 212 za Sekondari za kata na shule 16 za bweni za Wasichana za Kitaifa, ujenzi wa nyumba 212 za walimu (2 in 1), ukarabati wa shule chakavu na kongwe na ukamilishaji wa mabweni ya wanafunzi Kidato cha tano na kutoa mafunzo kazini kwa Walimu wa shule za Sekondari 3,000 na maafisa 210 wa idara ya elimu ngazi ya mkoa na halmashauri. Aidha, kuendelea na ujenzi shule mpya 232 za Sekondari za kata zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400 kila moja ambapo ujenzi wa shule 14 umekamilika; kuendelea na ujenzi wa shule 10 maalumu za bweni (kidato cha 5 & 6) za wasichana kwa masomo ya Sayansi na upanuzi wa shule 11 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50; kukamilika kwa upanuzi wa shule kongwe 18 za sekondari na vituo nane (8) vya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ili vitumike kutoa elimu kwa njia mbadala kwa wasichana walio nje ya mfumo rasmi; kutoa mafunzo kazini kwa walimu 22,000 wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa lengo la kuwajengea walimu umahiri kwenye mada ngumu na umahiri kwenye masuala ya maabara, na mafunzo ya

walimu 500 wa TEHAMA ili kuwezesha ufundishaji wa masomo kwa njia ya TEHAMA. Jumla ya shilingi bilioni 357.07 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(f) Mradi Na. 6390: Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa maabara 10 za sayansi katika shule tano (5) za Sekondari; kuendelea na ujenzi wa ofisi za walimu katika shule 7 za sekondari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95, madarasa 114 (asilimia 95), nyumba 52 za walimu (asilimia 50), mabweni 10 ya wasichana katika shule 10 za sekondari katika shule za Msingi na Sekondari (asilimia 95), matundu ya vyoo 1,008 katika shule 80 za msingi na 22 za sekondari (asilimia 90), ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia katika vyuo vikuu viwili vilivyopo Tanzania Zanzibar ambavyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar katika Kampasi ya Pemba (the State University of Zanzibar (SUZA) -Pemba Campus na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (Karume Institute of Science and Technology (KIST) (asilimia 95); kutolewa kwa mafunzo ya ujuzi kwa wanufaika 11,793 katika maeneo ya kilimo - uchumi, kilimo, utalii na huduma za ukarimu, usafirishaji na uchukuzi, ujenzi, nishati na TEHAMA; kuendelea na ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule nane (8) (asilimia 95). Jumla ya shilingi bilioni 15.78 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 6363: Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha - ATC**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 436, madarasa nane (8) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 880, maabara sita (6) zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 270 na ofisi 26 zenye uwezo wa kuhudumia watumishi 104; na kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa hospitali ya taaluma na tiba (polyclinic) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95.3. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(h) Mradi Na. 4397: Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ambapo kwa upande wa ujenzi hatua iliyofikiwa ni kama ifuatavyo: vyuo 33 (29 vya Wilaya na 4 vya Mikoa) ujenzi umefikia wastani wa asilimia 98; ujenzi wa vyuo 65 vya wilaya na mikoa vipo katika hatua ya ujenzi wa msingi; jengo la ofisi ya VETA Makao Makuu upo katika hatua ya awali; karakana nne (4) katika chuo cha Kihonda (asilimia 25); bweni moja (1) katika Chuo cha Wilaya ya Simanjiro (asilimia 65); mabwalo ya chakula katika Vyuo vya Wilaya ya Namtumbo (asilimia 86), Ileje (asilimia 20) na karakana ya uchomeleaji na uungaji wa vyuma katika Chuo cha cha Mkoa wa Manyara (asilimia 79); Kuendelea na ukarabati wa vyuo katika mkoa wa Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99, Mtwara (asilimia 99), Dar es Salaam (65) na Mwanza (asilimia 64); na kuendelea na ukarabati wa vyuo vya wilaya za Kitangari (asilimia 98), Wanging’ombe (asilimia 95), pamoja na majengo ya makazi ya wafanyakazi Tabata (asilimia 85). Jumla ya shilingi bilioni 40.5 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 4323: Kuendeleza Elimu ya Ualimu - TESP**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na uundaji wa mfumo wa usahihishaji wa kielektroniki ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85; ujenzi na ukarabati wa maabara za sayansi, maktaba na vyumba vya TEHAMA katika Vyuo vya Morogoro ambapo utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 90, Tukuyu (asilimia 92), Kasulu (asilimia 90), Patandi (asilimia 91), Mpwapwa (asilimia 70) na Dakawa (asilimia 70); ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na kuunganisha vyuo 35 vya ualimu katika Mkongo wa Taifa (asilimia 40); kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa vyuo vya ualimu 35; na kutoa mafunzo kwa wakufunzi 341 na walimu 137 kuhusu maandalizi ya utekelezaji wa mitaala mipya ya ufundi, mafunzo ya masuala ya usawa wa kijinsia na ujumuishi kwa wasaidizi wa wakuu wa vyuo na waratibu wa masuala ya usawa wa kijinsia na ujumuishi katika Vyuo vya ualimu, wafanyakazi wa Wizara Makao Makuu, na wathibiti ubora wa Kanda na mafunzo ya masuala ya mazingira kwa wasimamizi 181 katika vyuo vya ualimu. Jumla ya shilingi bilioni 12.35 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(j) Mradi Na. 4340: Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 636.4 kwa wanafunzi 198,105 ambapo wanafunzi 73,513 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 124,592 ni wanaoendelea na masomo; kuwezesha ukusanyaji wa mikopo iliyoiva ya shilingi bilioni 169.8 sawa na asilimia 86.6 ya lengo; kutolewa kwa shilingi bilioni 2.99 kwa ajili ya kudhamini wanafunzi 636 wenye ufaulu wa juu zaidi katika programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) kupitia Samia Scholarship; na kukagua waajiri na kubaini waajiriwa 32,150 wanaodaiwa. Jumla ya shilingi bilioni 656.9 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(k) Mradi Na. 4392: Mradi wa Elimu wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi wa ESPJ**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ukarabati na ujenzi wa vyuo 14 vya maendeleo ya wananchi (FDCs) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95, vyuo 25 vya Ufundi Stadi vya Wilaya (asilimia 98) na Chuo cha Ufundi cha Dodoma (asilimia 98.5). Jumla ya shilingi bilioni 27.7 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(l) Mradi Na. 4315: Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation Project - HEET)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na taratibu za manunuzi ya kuwapa wakandarasi na washauri elekezi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vyuo 22 vya elimu ya juu vinavyonufaika na mradi; kutoa mafunzo kwa taasisi 22 zinazonufaika na mradi kuhusu kuhuisha na kuandaa mitaala mipya inayoendana na mahitaji ya soko la ajira; kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 369 (ndani na nje ya nchi) ambapo 250 ni uzamivu (Phd) na 119 ni uzamili (masters); kuendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia ya mwaka 2013, Sayansi na

Teknolojia ya mwaka 1996, Utafiti na Maendeleo ya Mwaka 2010, na Bayoteknolojia ya Mwaka 2013; kutoa mafunzo kwa taasisi nane (8) kwa ajili ya uanzishaji wa ofisi za uhawilishwaji wa Teknolojia na Usimamizi wa Miliki; kuwajengea uwezo waratibu wa miradi wa Taasisi 22 zinazonufaika na mradi na Wizara Makao Makuu kuhusu ufanyaji kazi wa Kamati za Ushauri za Vyuo Vikuu/taasisi na wadau wa kisekta (Industrial Advisory Committee – IAC) katika maeneo ya utafiti, mafunzo, ubunifu, ubiasharishaji, ushauri na ushirikiano na mawasiliano ya jamii; kuendelea na uandaaji wa mkakati wa Kitaifa wa usawa wa Kijinsia kwa Elimu ya Juu; kutoa mafunzo ya ukatili na unyanyasi wa kijinsia kwa madawati ya kijinsia 21 katika Taasisi 21 zinazonufaika na mradi; kuandaa mwongozo unaozingatia masuala ya wenye mahitaji maalum, kijinsia na masuala ya usalama wakati wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu. Jumla ya shilingi bilioni 133.3 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(m) Mradi Na. 4314: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa maabara ya baiolojia ya viumbe hai ambapo utekelezaji umefikia asilimia 88, maktaba awamu ya kwanza (asilimia 10) na mabweni mawili (asilimia 15); na kuendelea na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya chuo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80. Jumla ya shilingi milioni 210.2 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(n) Mradi Na. 6350: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la Shule Kuu ya Uchumi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70 na maabara kuu ya kemikali kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma za upimaji sampuli za viwandani (asilimia 30); kuendelea na upanuzi wa hosteli ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuongeza ghorofa mbili (2) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65; ujenzi wa jengo la Taasisi ya Bahari Buyu – Zanzibar (asilimia 75); na kuanza utekelezaji wa mradi wa ubunifu wa utengenezaji wa vifaa vya maabara vya mashuleni (asilimia 60). Jumla ya shilingi bilioni 17.44 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 87.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(o) Mradi Na. 4385: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa miundombinu ya maabara za sayansi katika shule ya sekondari ya mazoezi ya Chang'ombe ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60; na kuendelea na ujenzi wa Jengo la Kitivo cha Insia na Sayansi za Jamii na Maabara za Sayansi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi bilioni 7.4 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(p) Mradi Na. 6353: Upanuzi wa Chuo Kikuu Mzumbe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uwekaji wa samani katika madarasa Kampasi ya

Dar es Salaam na maabara za kompyuta kwa Ndaki ya Mbeya, ukarabati wa madarasa sita (6) katika Kampasi Kuu, bwalo la chakula Kampasi ya Mbeya na uwekaji wa taa za barabara Kampasi Kuu; kuendelea na ukarabati wa barabara za Tegeta Kampasi ya Dar es Salaam (asilimia 69), eneo la mahafali (asilimia 70), viwanja vya michezo (asilimia 44) na hosteli ya Mama Maria Nyerere (asilimia 48) katika Kampasi Kuu na hosteli Ndaki ya Mbeya (asilimia 10); na kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala (asilimia 74) na jengo la madarasa sita (6) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,129 katika Kampasi Kuu (asilimia 5). Jumla ya shilingi bilioni 2.1 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(q) Mradi Na. 6354: Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa vyumba vya madarasa 30, mabweni 2, maabara, ofisi saba (7), nyumba 10, na miundombinu ya TEHAMA; na kuendelea na ujenzi wa jengo la Ardhi - *Land Building wing "A"* ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50. Jumla ya shilingi bilioni 1.7 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(r) Mradi Na. 6365: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la stoo na choo, jengo la Kurugenzi ya Mafunzo ya Awali, utawala na mabweni matatu (3) ya wanafunzi; kuendelea na ujenzi wa jengo la Maktaba lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ambapo utekelezaji umefikia asilimia 9.42; na ujenzi wa jengo la kumbi za mihadhara lenye uwezo kuhudumia jumla ya wanafunzi 1,800 kwa wakati mmoja umefikia asilimia 50. Jumla ya shilingi milioni 906.1 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(s) Mradi Na. 6364: Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili - Kampasi ya Mloganzila**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa mabweni sita (6) ya Chole, maabara 2 za kufundishia (Multi User Simulation Lab), maabara ya mafunzo kwa vitendo na maabara ya shule ya meno (wet labs), maabara ya meno na maktaba; kuendelea na ununuzi wa vifaa vinavyotumia umeme wa jua ili kukuza matumizi ya teknolojia ya kijani kibichi na kupunguza matumizi makubwa ya umeme ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85; ujenzi wa tanki la maji katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (asilimia 95); kuendele na ujenzi wa kumbi za mihadhara 4, madarasa 3, Jengo la Utawala katika Kampasi Kuu ya Muhimbili ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50); kuendelea na ukarabati wa Hosteli nne (4) za wanafunzi, nyumba moja (1) ya utafiti na mifumo ya maji na umeme ya kituo cha kufundishia cha Bagamoyo kampasi ya Muhimbili ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80.6. Jumla ya shilingi bilioni 3.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(t) Mradi Na. 4384: Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaaam – DIT**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanzishwa kwa kiwanda cha kuzalisha vipuri vya magari

kutokana na taka za plastiki katika Kampasi Kuu; kuendelea na ukarabati wa mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 kila moja Kampasi kuu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 5; kuendelea na ujenzi wa madarasa matano (5) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 200 na mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 160 katika Kampasi ya Myunga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Ubora katika TEHAMA na Ngozi (asilimia 10); na kuendelea na tafiti nne (4) katika kilimo kuhusu hali ya hewa, ufanisi wa nishati, mkono bandia na kifaa cha kuwasaidia watoto wachanga wenye matatizo ya upumuaji. Jumla ya shilingi bilioni 8.0 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 700.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(u) Mradi Na. 6352: Tume ya Nguvu za Atomiki - TAEC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa Ujenzi wa maabara za Arusha na Dodoma; kuendelea na ujenzi wa ofisi na maabara za Dar es Salaam (asilimia 37), Mwanza (asilimia 89) na Zanzibar (asilimia 78); na jengo maalumu la kuhifadhi mazao ya kilimo kwa kutumia teknolojia ya mionzi (asilimia 37). Jumla ya shilingi bilioni 2.1 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(v) Mradi Na. 6333: Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya maabara na karakana ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99; na kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 800 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 225.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(w) Mradi Na. 6361: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine – SUA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa usimikaji wa mtambo wa kutotoleshea vifaranga vya samaki aina ya kambale; kuboresha mafunzo ya vitendo kwa kununua vifaa vya maabara; kuratibu mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu za kilimo, ikolojia ya kilimo katika uzalishaji wa mazao ya mbogamboga, ufugaji bora wa samaki, kuandaa miche ya miti ya matunda na kuiuza kwa wadau mbalimbali na kuboresha shamba la mafunzo; kuendeleza uzalishaji na utotoleshaji wa vifaranga vya samaki; ukarabati wa mifumo miwili (2) ya ufugaji wa samaki ya mzunguko (Recirculating Aquaculture systems); na ukarabati wa Hosteli katika Kampasi ya Edward Moringe (asilimia 70). Jumla ya shilingi bilioni 7.9 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(x) Mradi Na. 6229: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa majiko na gesi kwa ajili ya vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi (asilimia 96); na kuendelea na ununuzi wa vifaa vya karakana katika vyuo 34 vya maendeleo ya wananchi (asilimia 90). Jumla ya shilingi bilioni 3.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(y) Mradi Na. 4381: Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) awamu ya pili yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 768 katika kampasi ya Karume – Zanzibar ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 47 na Jengo la Maktaba na ukumbi wa mihadhara (asilimia 36), ujenzi wa madarasa 10 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja, na ofisi za walimu wanne (asilimia 60) Kampasi ya Pemba Zanzibar. Jumla ya shilingi bilioni 4.7 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(z) Mradi Na. 4306: Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa moja (1) lenye ofisi kumi (10) na kumbi nne (4) za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 katika Kampasi ya Mbeya ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70, kumbi za mihadhara katika kampasi ya Bagamoyo (asilimia 5); na kufanyika kwa tafiti mbili (2) ambazo zimesababisha kuchapishwa kwa vitabu viwili (2) vya Kiongozi cha Mwalimu Mkuu (School Management Manual) pamoja na kitabu cha Utawala Bora katika Elimu (LGA Good Governance Manual) vitakavyotumiwa na watendaji kutatua changamoto za elimu katika ngazi ya Halmashauri na mwongozo kwa walimu Wakuu ili kuboresha usimamizi wa shule. Jumla ya shilingi bilioni 5.9 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(aa) Mradi Na. 6345: Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ugharamiaji wa miradi 174 (ubunifu 133, utafiti 30 na miundombinu ya utafiti 11); kutoa vibali vya miradi 1,162 ya utafiti katika maeneo ya Sayansi, Afya, Kilimo, Mifugo, Sayansi ya Jamii, utalii, Uhandisi, Sanaa, utamaduni, lugha na fasihi; kutolewa kwa mafunzo kwa viongozi 21 kutoka taasisi za utafiti na vyuo vikuu, Wizara ya Fedha Zanzibar, Tume ya Mipango - Zanzibar na Sekta Binafsi kuhusu uendelezaji na utekelezaji wa kigoda cha Utafiti ili kubaini na kuimarisha tafiti katika maeneo ya uchumi wa buluu (sekta ya uvuvi), uchumi wa kidijitali (Data-driven economy), Kilimo, Chakula, Lishe na sekta ya Afya na mabadiliko ya miundo; na kutolewa kwa mafunzo ya usimamizi wa tafiti na utawala kwa wasimamizi wa tafiti kutoka Taasisi nane (8) za Utafiti. Jumla ya shilingi bilioni 4.9 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(bb) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa maboma 1,704 ya vyumba vya madarasa ya shule za msingi, maboma 286 ya vyumba vya maabara za sayansi katika shule za sekondari, mabwalo ya chakula 70 na mabweni 390 katika shule za msingi na sekondari zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa nyumba 216 za walimu, vyumba 1,374 vya madarasa katika shule kongwe, uzio wa mabweni 70 ya watoto wenye mahitaji maalumu, matundu 5,320 ya vyoo katika shule shikizi, madarasa

8,000 ya shule za sekondari *(Pochi la Mama)* na kukamilika kwa shule mpya 13 za Msingi. Jumla ya shilingi bilioni 263.83 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 56.84 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/34.

**(cc) Mradi Na. 4322 na 4393: Elimumsingi na Sekondari Bila Ada**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kutoa elimumsingi na Sekondari bila ada ikijumuisha ruzuku ya uendeshaji wa shule, posho ya madaraka kwa walimu wakuu 21,335 na maafisa elimu kata 3,921; fidia ya ada kwa wanafunzi wa shule za bweni 204,439 na kutwa 2,341,438; na kugharamia chakula cha wanafunzi 226,723 wa shule za bweni na wanafunzi 45,366 wenye mahitaji maalum wa shule za msingi za kutwa. Jumla ya shilingi bilioni 355.06 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 99.9 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(dd) Mradi Na. 4309: Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki (EASTRIP)**

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT )**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa majengo nane (8) kwa ajili ya madarasa, maabara, karakana, mabweni na ofisi za watumishi ambapo majengo matano (5) yanajengwa katika Kampasi ya Mabibo – Dar es Salaam na ujenzi wake umefikia asilimia 69 na majengo matatu (3) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro yapo hatua ya usanifu wa majengo; Kukamilisha ununuzi wa *Aircraft Engineering System Trainers (runnable turbo jet engine na motorised cutway piston engine)* na *Virtual Maintenance Trainer (VMT) for Boeing 737-800* kwa ajili ya mafunzo ya Wahandisi wa Matengenezo ya Ndege na vifaa maalum (Fixed Cabin Crew Mock – Ups) vya mafunzo ya wahudumu wa ndani ya ndege; Kuendela na ununuzi wa Vifaa vya mafunzo ya Urubani, *Flight Simulators* mbili, *Workshop*, *Multimedia and Computer Based equipment* umefikia asilimia 50. Jumla ya shilingi bilioni 7.44 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 2.53 katika robo ya kwanza ya 2023/24.

**(ee) Mradi Na. 6321: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala Kampasi ya Babati ambapo utekelezaji umefikia asilimia 78 na kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi kampasi ya Arusha ambapo utekelezaji umefikia asilimia 35. Jumla ya shilingi bilioni 5.0 zimetumika mwaka 2022/23.

**(ff) Mradi Na. 6322: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa madarasa, jengo la utawala, bwalo la chakula pamoja na ukumbi wa mihadhara (multipurpose hall) Geita ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99. Aidha, ujenzi wa bweni, nyumba za wafanyakazi, maktaba na maabara ya kompyuta umefikia asilimia 57. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 zimetumika mwaka 2022/23.

**(gg) Mradi Na. 6323: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, madarasa na maktaba katika Kampasi ya Nyang'homango, Misungwi - Mwanza ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80. Jumla ya shilingi bilioni 2.55 zimetumika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 1.66 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(hh) Mradi Na. 6206: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa bweni la wanafunzi awamu I na II na kuanza ujenzi awamu III katika Kampasi Kuu Miyuji (Dodoma); ujenzi wa ukumbi wa mihadhara awamau I na II na kuanza kazi ya kuweka thamani Kampasi Kuu Miyuji (Dodoma); na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara awamu III na bweni la wanafunzi katika kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa Magu (Mwanza). Jumla ya shilingi bilioni 5.26 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 2.11 zimetumikakatika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(ii) Mradi Na. 6389: Chuo cha Takwimu Mashariki Mwa Afrika (EASTC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa a jengo la utawala ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70. Jumla ya shilingi bilioni 1.11 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 380.46 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**2.3.5.4. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**(a) Mradi Na. 2326: Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa skimu za uendelezaji maeneo ya mijini kwa majiji ya Mbeya, Mwanza na Arusha; kupimwa na kuidhinishwa kwa viwanja 118,045 kwenye Halmashauri 55; kupangwa na kupimwa kwa maeneo yanazonguka miradi wa kimkakati wa Bomba la Mafuta (EACOP); kuandaliwa kwa mipangokina mitano (5) ya uendelezaji upya wa maeneo ya fukwe; na kutatuliwa kwa migogoro ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 975. Jumla ya shilingi bilioni 17.2 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Mradi Na. 2324: Mradi wa Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuimarisha mpaka kati ya Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilomita 110 kwa kupima, kuongeza alama, kuboresha zilizoharibika na kuandaa ramani za mipaka. Jumla ya shilingi bilioni 1.75 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kujenga madarasa mawili (Lecture Theater Rooms), maktaba na kukarabati Ofisi za Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA); na kujenga madarasa mawili ya Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO). Jumla ya shilingi milioni 444.08 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Halmashauri za Wilaya tatu (3) za Nsimbo (Katavi), Ngorongoro (Arusha) na Kigoma; Vijiji 316 vilivyopo kando ya miradi ya kimkakati ya SGR, EACOP na JNHPP; kukagua na kufanya tathimini ya vijiji 100 vyenye mipango ya matumizi ya ardhi; kuandaa hati za haki ya hatimiliki ya Kimila) 7,438 katika Halmashauri ya Wilaya za Makete (6,594) na Iramba Hati (844). Jumla ya shilingi bilioni 3.97 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 4953: Uboreshaji wa Milki za Ardhi**

Hatua zilizofikiwa ni: Kuidhinishwa kwa viwanja 3,640 katika Jiji la Dodoma na viwanja 5,600 katika Manispaa ya Kigoma Ujiji; kusimika alama za msingi za upimaji 67; kupimwa kwa mipaka ya vijiji 80; na kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya tano (5) za Maswa, Mbinga, Mafinga, Songwe na Chamwino. Jumla ya shilingi bilioni 6.96 zimetumika katika Mwaka 2022/23.

### 2.3.5.5. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira

**(a) Mradi Na. 3280: Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 630 yenye vituo 6,553 vya kuchotea maji vinavyonufaisha wananchi wapatao 4,393,274 kwenye vijiji 1,390; na kuundwa kwa Vyombo 129 vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii - CBWSOs. Hatua hii imechangia kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa asilimia 74.5 mwaka 2021 hadi kufikia wastani wa asilimia 77 mwaka 2022. Jumla ya shilingi bilioni 219.88 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 72.98 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(b) Mradi Na. 3306: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uchimbaji wa visima vitano (5) katika jiji la Dodoma na ununuzi na ufungaji wa pampu; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira Arusha ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99.5; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kutoa maji mto Kiwira kupeleka Jiji la Mbeya ambapo utekelezaji umefikia asilimia 5; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za maji katika jiji la Mwanza ambao ukikamilika utawezesha wananchi wapatao 440,000 ambapo umefikia asilimia 96; na kuendelea na mradi wa kuboresha huduma ya maji wa Dareda - Singu - Sigino – Baraga katika mji wa Babati ambao umefikia asilimia 90.

Aidha kwa upande majitaka shughuli zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa mradi wa Upanuzi wa Mfumo wa Uondoshaji Majitaka katika Maeneo ya Korongoni na Longuo “A” Manispaa ya Moshi; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya uondoshaji

majitaka katika mji wa Musoma umefikia asilimia 15; na kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya uondoshaji majitaka kwenye maeneo ya Area C katika Jiji la Dodoma (asilimia 91). Jumla ya shilingi bilioni 79.93 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 36.79 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(c) Mradi Na. 3307: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Mugango – Kiabakari - Butiama ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 90; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa miji 28 ambapo utekelezaji wa *Package I* inayohusisha HTM na miji ya Korogwe, Muheza na Pangani umefikia wastani wa asilimia 10.35; *Package II* inayohusisha miji ya Kilwa masoko na Nanyumbu asilimia 5; *Package III* inayohusisha miji ya Ifakara, Chunya, Rujewa, Wanging'ombe, Makambako na Njombe asilimia 5.5; *Package IV* inayohusisha miji ya Kiomboi, Singida, Manyoni, Chamwino, Chemba na Mugumu asilimia 5.25; *Package V* inayohusisha miji ya Kasulu, Mpanda, Urambo/Kaliua na Sikonge asilimia 9.6; *Package VI* inayohusisha miji ya Kayanga, Chato na Geita asilimia 5.1; ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Mafinga asilimia 15.1; mradi wa maji wa Tarime/Rorya asilimia 9 na mradi wa maji wa Mkinga – Horohoro asilimia 12; na ujenzi na ukarabati wa mradi wa maji wa Makonde asilimia 15.

Shughuli zingine ni: kukamilika kwa miradi ya uondoshaji majitaka katika mji wa Nzega; na kuendelea na ujenzi wa mifumo ya uondoshaji majitaka katika miji ya Igunga, Pangani, Chato, Kyaka na Muheza. Jumla ya shilingi bilioni 63.70 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 33.06 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(d) Mradi Na. 3341: Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mradi ambapo utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 79; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika miji ya Same na Mwanga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98. Jumla ya shilingi bilioni 8.65 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(e) Mradi Na. 3403: Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga na Miji Mingine**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa mradi wa upanuzi wa mtandao wa majisafi katika Wilaya Busega (kata za Nyashimo, Lamadi na Mhula); Kukamilika kwa zoezi la kulipa fidia, usanifu wa bomba kuu na kuhamisha makaburi 78 kwenye eneo la mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika mkoa wa Simiyu; kukamilika kwa usanifu wa miundombinu ya kusambaza maji katika miji na vijiji 147 kandokando ya bomba kuu; na kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya ulazaji wa bomba kuu umbali wa km 131.13, ujenzi wa matanki sita (6), ujenzi wa kituo cha kusukuma maji na mtandao wa mabomba wenye urefu wa km 328.42. Jumla ya

shilingi bilioni 28.72 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 1.84 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(f) Mradi Na. 3435: Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufuatilia, kukusanya na kuhakiki ubora wa maji kwenye jumla vyanzo vya maji 1,534 ya skimu 2,432 za usambazaji maji vijijini na mitandao 201 ya usambazaji maji mijini ambapo matokeo ya uchunguzi wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji yalionesha hali ya ubora wa maji inaridhisha na inaendelea kulinda afya ya ikolojia. Shughuli nyingine ni: kuendelea kuimarisha maabara za ubora wa maji kwa kuzipatia vitendea kazi. Jumla ya shilingi bilioni 5.07 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(g) Mradi Na. 3437: Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji eneo la DAWASA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa usambazaji wa maji katika maeneo ya Mshikamano, zegereni na Chalinze III; na kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi wa kutoa maji kutoka kwenye tanki la Chuo Kikuu Ardhi na kupeleka Bagamoyo. Jumla ya shilingi bilioni 45.46 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 11.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(h) Mradi Na. 3438: Mradi wa Bwawa la Kidunda**

Hatua iliyofikiwa ni: kupatikana kwa Mkandarasi wa ujenzi na Mtaalam Mshauri atakayesimamia ujenzi wa bwawa ambapo shughuli zinazoendelea ni utafiti wa hali ya udongo, ununuzi wa vifaa na kusafisha eneo la kazi. Kwa ujumla utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 5. Jumla ya shilingi bilioni 59.22 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(i) Mradi Na. 3439: Mradi wa Maji wa Mpera na Kimbiji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji ujazo wa lita milioni 15 katika eneo la Kisarawe II; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika maeneo ya Kigamboni ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95. Jumla ya shilingi bilioni 6.86 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 1.98 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(j) Mradi Na. 6545: Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati vituo 136 na ujenzi wa vituo sita (6) vya kufuatilia rasimali za maji nchini; kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa mabwawa 10 ya ukubwa wa kati; Kutoa vibali vipya 1,554 vya matumizi ya maji katika Bodi za Maji za Mabonde; kutolewa kwa vibali 36 kwa ajili ya kutupa majitaka kwenye mazingira; kuanzishwa kwa jumuiya 22 za watumiaji wa maji; na kukamilika kwa upimaji na uwekaji mipaka katika vyanzo 63 kama hatua ya awali ya kuvilinda na kuvitangaza pamoja na kutangaza vyanzo 41 kwenye Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu. Jumla ya shilingi bilioni 29.87 zimetumika katika mwaka 2022/23.

#### 2.3.5.6. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

**(a) Programu Na. 5301: Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

**(i) Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa uchimbaji wa visima virefu 14 vyenye urefu wa mita kati ya 100 hadi 150; kukamilika kwa ujenzi wa majosho sita (6) na malambo saba (7); kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda kimoja (1) cha kuchakata mafuta ya Alizeti na viwanda vidogo viwili (2) vya bidhaa za ngozi na kuhuishwa kwa taarifa za utekelezaji wa shughuli za mradi kwenye Mfumo wa Kielekroniki wa Elimu kwa Umma kuhusu mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Jumla ya shilingi bilioni 3.7 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 422 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(ii) Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutoa mafunzo kwa wakulima 335 kuhusu Kilimo hifadhi na mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya Tabianchi; kukamilika kwa ujenzi wa majiko banifu 257 kwa kaya 250 na taasisi 7; kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya majiko banifu kwa wanufaika 317 katika Wilaya za Micheweni (72), Kondoa (47), Mkalama (84), Magu (63) na Nzega (51); kupandwa kwa miche 59,020 ya miti ya matunda na misitu na mikoko 2,057,225 ili kuendeleza kilimo himilivu na mazingira; Kufanyika kwa tathimini ya Hewa ya Ukaa ambapo tathmini imeonesha mradi umeweza kuepuka tani 30,963 za uzalishaji wa hewa ya kaboni katika halmashauri tano (5) na kufyonza tani 579,475 za hewa ya kaboni; kuchimba visima virefu na vifupi 22 katika Halmashauri tano (5) kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa tuta lenye urefu wa mita 850, kutengenezwa na kutundikwa kwa mizinga ya Nyuki 3,665 na kutoa mafunzo ya masoko na ubora wa bidhaa kwa wanufaika 659 Tanzania bara na Zanzibar. Jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iii) Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu – REDD+**

Hatua iliyofikiwa ni: kuandaliwa kwa Kanuni na Mwongozo wa biashara ya kaboni; kujenga uelewa kwa wadau takribani 300 Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu Kanuni na Mwongozo wa biashara ya kaboni na masuala ya mabadiliko ya tabianchi; kuwezesha ushiriki wa Tanzania Katika Mkutano wa 27 (COP 27) wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Misri; kuendelea na maandalizi ya maandalizi ya mkutano wa 28 wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) utakaofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu. Jumla ya shilingi milioni 348.00 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(iv) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na Urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bioanuai**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa uanzishwaji wa mashamba darasa 15 ya malisho katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (2), Mbeya (8) na Sumbawanga (5); kutengwa na kuhifadhiwa kwa misitu yenye ukubwa wa hekta 22,971.3 katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Wanging'ombe, Mbarali, Mbeya, Sumbawanga, Mpimbwe na Tanganyika; Kupandwa kwa miche 1,006,836 katika Halmashauri ya Wilaya za Mbeya, Sumbawanga, Mpimbwe Mbarali, Wanging'ombe, Iringa na Tanganyika; Kukamilika kwa uanzishwaji wa mashamba darasa 31 ya kilimo cha mazao himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi katika Halmashauri zinazotekeleza mradi; na kupandwa kwa miti 304,780 kwenye maeneo ya mradi yaliyoharibika katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Mbarali, Sumbawanga na Tanganyika. Jumla ya shilingi bilioni 7.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(b) Programu Na. 6571: Programu ya Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004**

**(i) Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Nyasa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi wa misitu katika halmashauri tano (5) za Wilaya za Mbinga, Nyasa, Kyela, Ludewa na Makete; na kutoa mafunzo kwa wanakijiji 300 kuhusu kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi. Jumla ya shilingi milioni 620 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(ii) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa Kanuni tano (5) na miongozo mitano (5) ya utekelezaji wa Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira; kuendelea na maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa na Mpango kazi wa usimamizi wa taka; na kuendelea na maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa vibali vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (SEA). Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(c) Mradi Na. 5305: Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa rasimu ya kanuni za udhibiti na usimamizi wa kemikali zinazodumu kwenye Mazingira kwa muda Mrefu; Kuandaa michoro ya kina, rasimu za Mipango ya usimamizi wa taka na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kukusanya na kuchambua taka zinazorejelezwa katika Manispaa za Kigamboni na Ubungo. Jumla ya shilingi milioni 226.8 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(d) Mradi Na. 5304: Kudhibiti Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

Hatua iliyofikiwa ni: kutolewa kwa mafunzo kwa maafisa 90 kuhusu usimamizi na udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; kutolewa kwa mafunzo kwa mafundi mchundo 60 wa viyoyozi na majokofu kuhusu namna ya kuhudumia

vifaa hivyo pasipo kuharibu mazingira; na kuandaliwa kwa Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni za mwaka 2022. Jumla ya shilingi milioni 197.7 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi milioni 28 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(e) Mradi Na. 6309: Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ukarabati wa Makazi ya Makamu wa Rais, Kilimani Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98 na jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II - Dar es Salaam (asilimia 53). Jumla ya shilingi bilioni 1.45 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**(f) Mradi wa Ujenzi wa miundombinu ya kuzuia maji ya bahari kujaa na kuathiri maeneo ya makazi na kilimo katika fukwe za Swipwese- Pemba na Mikindani- Mtwara**

Hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi wa miundombinu ya kuzuia maji ya bahari kujaa na kuathiri maeneo ya makazi na kilimo katika Fukwe za Swipwese umefikia asilimia 70 na ujenzi wa fukwe za Mikindani Mtwara umefikia asilimia 55. Jumla ya shilingi milioni 582.45 zimetumika katika mwaka 2022/23.

**2.3.5.7. Usimamizi wa Maafa Nchini**

**(i) Mradi Na. 6575: Kuimarisha Uwezo wa Kujiandaa na Kukabili Maafa**

Hatua iliyofikiwa ni: kutoa huduma za kibinadamu kwa watu walioathirika na maafa zikiwemo makazi ya muda, matibabu na chakula kwa maafa yaliyotokea katika Halmashauri 25; kuandaliwa kwa mipango ya kujiandaa na kukabiliana na maafa na mikakati ya kupunguza madhara katika halmashauri 14; kutolewa kwa mafunzo kwa Kamati za Usimamizi wa Maafa na waratibu wa maafa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara; kutolewa kwa mafunzo ya kuimarisha uwezo wa vikundi vya uokoaji vya wavuvi 344 katika ukanda wa Ziwa Victoria; kuhuisha Mpango wa Dharura wa Taifa wa Kukabiliana na Ukame; na kufanya tathmini ya kina ya hali ya usalama wa chakula na lishe katika Halmashauri 30 za mikoa mitano (5); kutolewa kwa misaada ya kibinadamu kwa watu walioathirika na maafa yaliyotokana na Kimbunga *Freddy* - Malawi. Jumla ya shilingi bilioni 4.3 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shillingi milioni 332 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(ii) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

**Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Usimamizi wa Maafa Nchini**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa maghala mawili (2) ya kuhifadhi vifaa vya misaada ya kibinadamu wakati wa maafa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96; na kuanza ufungaji wa fascia na eave boards katika maghala na ujenzi wa jengo la utawala. Jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika katika mwaka 2022/23 na shilingi millioni 243.35 katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

### 2.3.6. Kuendeleza Rasilimali Watu

#### 2.3.6.1. Ujuzi na Uwezeshaji

**(a) Mradi Na. 6581: Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwezesha vijana 11,973 kupata mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi (Apprenticeship) katika fani mbalimbali za ufundi stadi; kuwezesha wahitimu 1,704 wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi (Internship) katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi; kufadhili vijana 200 kupata mafunzo ya uzoefu katika fani ya ufugaji samaki na mazao ya bahari; kufadhili vijana 308 kupata mafunzo ya kunenepesha mifugo kupitia vituo vya LITA na TALIRI vilivyopo Tanga, Mwanza na Kagera; kuwezesha vijana 74 kushiriki mafunzo ya uzoefu wa kazi (Internship) katika kilimo cha vizimba (Block Farms) kupitia mradi wa Building Better Tomorrow (BBT) katika kituo cha Bihawana - Dodoma; kutolewa mafunzo ya kukuza ujuzi (upskilling) kwa waongoza watalii na wafanyakazi wa hotelini 1,333; kuratibu na kuwezesha ushiriki wa wajasiriamali wadogo na wa kati wa sekta isiyo rasmi 250 katika maonesho ya 22 ya nguvu kazi/juakali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Jijini Kampala, Uganda; kuendelea na jitihada za kukuza ujuzi kwa vijana kwenye sekta ya kilimo ambapo vijana 260 wamepelekwa nchini Israeli kwa ajili ya mafunzo ya kilimo; na Kuwezesha vifaa mtaji Seti za Vyerehani, vifaa vya uchomeleaji na mashine za kutengeneza bidhaa za *alumunium* kwa ajili ya vikundi vya vijana vilivyohitimu mafunzo katika Halmashauri. Jumla ya shilingi bilioni 7.5 zimetumika katika mwaka 2022/23 na kiasi cha shilingi bilioni 5.75 zimetumika katika kipindi cha robo ya kwanza kwanza ya Mwaka 2023/24.

**(b) Mradi Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana**

Hatua iliyofikiwa ni: kukusanywa kwa fedha za marejesho kiasi cha shilingi bilioni 2.6 kutoka kwenye vikundi vya vijana; kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi billioni 3.15 kwenye miradi ya vikundi 141 yenye vijana 987; kujengea uwezo vijana wajasiriamali 1,497 walio katika sekta isiyo rasmi katika maeneo ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara, urasimishaji pamoja na kuunganishwa na huduma za kibiashara; na kuunganishwa kwa makampuni 118 ya vijana katika huduma zabuni za ununuzi wa umma. Jumla ya shilingi bilioni 2.82 zimetumika katika Mwaka 2022/23 na kiasi cha shilingi bilioni 1.27 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(c) Mradi Na. 6205: Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na mapitio ya Programu ya Kukuza Kazi za Staha; kuandaliwa kwa Rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya Kinga ya Jamii na Rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana; kuandaliwa kwa Mwongozo Sanifu na Mfumo wa Uratibu, Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa za Utekelezaji wa Programu ya Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya Shule na Mwongozo wa Stadi za Maisha

katika lugha ya Kiswahili; kuendelea na maandalizi ya Rasimu ya Pili ya Mfumo wa Uratibu, Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa za Utekelezaji wa Programu ya Stadi za Maisha; kukamilika kwa uchambuzi wa Sheria Na. 2 ya Mwaka 2015 ya Baraza la Vijana Tanzania pamoja na kanuni zake; kuanza majaribio ya Mfumo wa Kielektroniki wa Kanzi Data kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu; na kusambazwa kwa Mwongozo wa Taifa wa Utambuzi wa Mapema wa Afua Stahiki kwa Watoto Wenye Ulemavu. Jumla ya shilingi bilioni 1.48 zimetumika katika Mwaka 2022/23 na kiasi cha shilingi milioni 227. 78 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/24.

**(d) Mradi Na. 4954: Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa vyumba vya madarasa 17, mabweni ya wanafunzi 10, nyumba za watumishi 20, karakana saba (7), majengo ya utawala manne (4), majiko mawili (2), na matundu ya vyoo tisa (9) katika Vyuo vya Ufundi Stadi na Marekebisho vya Mtapika (Masasi – Mtwara), Luanzali (Tabora), Sabasaba (Singida) na Yombo (Dar es Salaam). Jumla ya shilingi bilioni 3.46 zimetumika katika mwaka 2022/23.

### 2.3.7. Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma

Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH) ilikusanya mapato yasiyo ya kodi jumla ya shilingi bilioni 1,011 kutoka Taasisi na Mashirika ya Umma, madeni ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (Ex-NBC), madeni ya ubinafsishaji na kodi ya upangishaji wa majengo yaliyopo chini ya usimamizi wa OMH. Makusanyo hayo ni sawa na ufanisi wa asilimia 108.4 ya lengo lililokusudiwa la kukusanya shilingi bilioni 932.96 kwa kipindi husika. Kuongezeka kwa mapato hayo kumetokana na kuongezeka kwa michango ya asilimia 15 kwenye mfuko mkuu, ulipaji wa madeni kwa wakati, makusanyo ya mtaji wa ziada pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na simu zinazopigwa nje nchi (TTMS) kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma.

Aidha, kuongezeka kwa mapato hayo kulichangiwa pia kwa kuongezeka kwa makusanyo ya madeni ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (Ex-NBC), madeni ya ubinafsishaji na kodi ya upangishaji wa majengo. Vile vile, Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma umeongezeka kutoka shilingi trilioni 67.79 mwaka 2020/21 hadi kufikia shilingi trilioni 70.67 mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 4.24.

### 2.3.8. Uwekezaji Kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania

Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC) imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi ambapo mwezi Juni 2023, mikataba nane (8) ya utekelezaji wa miradi mbalimbali yenye jumla ya thamani ya dola za Marekani milioni 1,805.12 inayotarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja 16,355 ilisainiwa.

### 2.3.9. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

**Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

Hatua iliyofikiwa ni:

(i) Kuendelea na ujenzi Kituo cha Tiba ya Ugonjwa wa Saratani chini ya Taasisi ya Tiba ya Ocean Road - (Mloganzila);

(ii) Kuanza kwa mapitio ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Awali wa ujenzi wa mradi wa Reli ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway);

(iii) Kuandaliwa kwa mkataba wa ubia na taratibu za kusaini mkataba kati ya Mbia Binafsi ambaye ni mtoa huduma wa kudumu na Wakala wa Serikali - DART kwa ajili ya kuendesha mradi wa mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza;

(iv) Kukamilika kwa uchambuzi ambao umebainisha kuwa mradi wa Magadi Soda – Engaruka unakidhi vigezo vya kushirikisha sekta binafsi kwa njia ya Joint venture (JV) au PPP katika utekelezaji;

(v) Kuendelea na taratibu za manunuzi ya mbia wa miradi ya ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano na Jengo la Biashara "Commercial Complex" katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na KIA;

(vi) Kuendelea na taratibu za manunuzi ya mbia wa mradi wa barabara ya tozo kutoka Kibaha - Mlandizi – Chalinze - Morogoro (km 205) sehemu ya Kibaha - Mlandizi- Chalinze (km 78.9);


(vii) Kuendelea na taratibu za manunuzi ya mbia wa mradi wa ukaguzi wa lazima wa vyombo vya moto na kufunga mfumo wa *traffic* kwenye barabara zote muhimu; na

(viii) Kuendelea na upembuzi yakinifu kwa miradi ya: ujenzi wa Hosteli za Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi za Dodoma na Dar es Salaam na Mbeya; barabara ya tozo kutoka Kibaha - Mlandizi- Chalinze- Morogoro (km 205) sehemu Chalinze - Morogoro (km 126.1); kuzalisha Umeme kwa njia ya Upepo katika wilaya za Siginda, Dodoma na Same wenye uwezo wa kuzalisha MW 210.

### 2.3.10. Ufuatiliaji wa Miradi katika kipindi cha Mwaka 2022/23

Serikali imeendelea kuimarisha utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo kwa lengo la kuongeza uwezo wa uzalishaji na kutoa huduma kwa wananchi. Katika mwaka 2022/23, jumla ya miradi 253 ilifanyiwa ufuatiliaji na tathmini. Miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini imejumuisha maeneo ya kukuza uchumi, huduma za jamii, na utawala bora, uwajibikaji na utoaji haki. Mchanganuo wa miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini ni kama inavyoonekana katika **kielelezo Na. 6.**

**Kielelezo Na. 4: Miradi iliyofanyiwa Ufuatiliaji na Tathmini**




Miradi mingine nane (8) katika kielelezo iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini ilihusisha miradi ya Utawala Bora, Uwajibikaji na Utoaji Haki (Sheria, Mambo ya Ndani, Habari na Mawasiliano).

Miradi ya kielelezo iliyofuatiliwa ni: Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (SGR); kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (MW 2,115); uboreshaji wa shirika la ndege Tanzania; ujenzi wa madaraja ya juu katika jiji la Dar es Salaam (Uhasibu, Chang'ombe na daraja la bandari); ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi; ujenzi wa Kiwanda na Uendelezaji wa Shamba la Miwa Mkulazi – Mbigiri Estate; ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (EACOP); ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa; na eneo maalum la uwekezaji Bagamoyo. Aidha, maandalizi ya Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini yanaendelea ambapo hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kwa Taarifa ya Kizio (Baseline Report) itakayotumika kama msingi wa maandalizi wa sera hiyo.

### 2.3.11. Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23

Katika zoezi la ufuatiliaji na tathmini changamoto mbalimbali zilijitokeza katika utekelezaji wa Mpango. Changamoto hizo zimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni changamoto za jumla na changamoto mahsusi za miradi.

**Changamoto za Jumla**

(i) Kupungua kwa nishati ya umeme ukilinganisha na mahitaji ya kiuchumi;

(ii) Ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia kutokana na kasi ya shughuli za kiuchumi kurejea katika hali ya kawaida baada ya kudhibitiwa kwa UVIKO-19 na mgogoro wa kivita baina ya Urusi na Ukraine. Ongezeko la bei ya mafuta limesababisha kuongezeka kwa gharama na kuchelewa kwa

utekelezaji wa miradi;

(iii) Ongezeko la bei ya bidhaa muhimu kwa ajili ya uzalishaji pamoja na usalama wa chakula nchini ikiwemo bidhaa za ujenzi, mbolea, ngano na kemikali muhimu zinazotumika viwandani kutokana na mgogoro wa kivita baina ya Urusi na Ukraine;

(iv) Kupungua kwa fedha za kigeni kwenye uchumi hususan dola za Marekani;

(v) Kuchelewa kukamilika kwa miradi kutokana na tatizo la upatikanaji wa vifaa na bidhaa muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, kutokana na UVIKO-19 na mgogoro wa kivita baina ya Urusi na Ukraine kuathiri mnyororo wa ugavi duniani (global supply chain disruptions);

(vi) Kukosekana kwa wabia wa miradi iliyoandaliwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi;

(vii) Wigo mdogo wa kodi unaotokana na baadhi ya biashara kutokuwa rasmi na hivyo kupunguza mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango; na

(viii) Baadhi ya wafanyabiashara kukwepa kodi, hususan kupitia njia za magendo na kutotoa stakabadhi za kielektroniki (EFD receipt) wakati wa mauzo.

**Changamoto Mahsusi**

(i) Upungufu wa rasilimali watu hususan wahandisi wa kusimamia utekelezaji wa miradi pamoja na wataalamu wa uendeshaji wa mitambo na vifaa vinavyotumia teknolojia ya kisasa;

(ii) Baadhi ya watekelezaji wa miradi kuchelewa kukamilisha taratibu za utoaji wa cheti cha msamaha wa kodi hali inayosababisha ongezeko la gharama (madai ya riba na adhabu) na ucheleweshaji wa miradi;

(iii) Usanifu duni wa mradi hali inayosababisha ongezeko la mawanda, gharama na muda wa utekelezaji wa miradi;

(iv) Usimamizi usioridhisha katika utekelezaji wa baadhi ya miradi kwa mujibu wa mikataba na mipango kazi kwa baadhi ya watekelezaji wa miradi;

(v) Ucheleweshaji wa nyaraka muhimu za malipo ya wakandarasi hali inayosababisha malimbikizo ya riba na ucheleweshaji wa mradi;

(vi) Usimamizi na uratibu wa miradi kwa baadhi ya taasisi kufanyika katika ngazi ya makao makuu bila kushirikisha wasimamizi waliopo katika eneo la mradi hali inayosababisha miradi kuchelewa, kuongeza gharama na kupunguza ufanisi katika kufikia malengo ya mradi;

(vii) Ushirikishwaji mdogo wa wadau muhimu wa mradi katika kipindi cha maandalizi hali inayosababisha kubadilika kwa mawanda ya kazi wakati wa utekelezaji; na

(viii) Kuchelewa kwa malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi.

### 2.3.12. Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto

(i) Kuimarisha utunzaji wa vyanzo vya maji vinavyotumika kuzalisha umeme, kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji – Julius Nyerere (JNHPP) MW 2,115, kuongeza upatikanaji wa gesi asilia na

kuendelea kushirikisha sekta binafsi katika uzalishaji wa umeme.

(ii) Kuboresha mifumo ya uagizaji na usambazaji wa mafuta nchini na kuanza kutumia nishati mbadala ya gesi (CNG) kwa ajili ya magari;

(iii) Kuendelea kuhamasisha na kuweka mikakati ya kuanzisha na kuendeleza viwanda mama (basic industries) ndani ya nchi hususani katika maeneo yanayoongoza katika kuagiza bidhaa nje ya nchi hususani malighafi za viwandani, bidhaa za chuma ikiwa pamoja na mashine na mitambo, mafuta, magadi soda pamoja na kuweka mikakati ya kuboresha mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi;

(iv) Kuendelea na hatua za kukabiliana na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kutoa ruzuku, kupunguza viwango na idadi ya tozo na kuongeza jitihada za kuongeza uwezo wa Akiba ya Kimkakati ya Hifadhi ya Mafuta (National Strategic Petroleum Reserves)

(v) Kutekeleza mikakati ya kuongeza uzalishaji wa ndani na mauzo nje ili kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni;

(vi) Kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kuongeza mapato ya ndani;

(vii) Kuendelea na hatua za kukabiliana na ongezeko la bei za bidhaa muhimu kwa ajili ya uzalishaji pamoja na usalama wa chakula nchini ikiwemo kupitia sera za kibajeti mfano; kupunguza tozo na kodi, utoaji ruzuku (mbolea na mafuta) kwa bidhaa muhimu na kuchukua hatua za kuongeza uzalishaji wa bidhaa husika nchini (mfano ngano na mbolea);

(viii) Kuendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuongeza mapato ya ndani na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia Mpango;

(ix) Kuendelea kudhibiti maeneo ya kipaumbele ili kuendana na rasilimali fedha zilizopo;

(x) Kuendelea kuhakikisha kuwa malipo ya hati za madai yanafanyika kwa mujibu wa mikataba;

(xi) Kuchukua hatua za kisera na kiutawala ili kuendelea kupambana na athari za mgogoro katika mnyororo wa ugavi duniani ikiwemo kutumia zaidi malighafi, vifaa na wataalamu wa ndani kwa maeneo yote ambayo hakuna ulazima wa huduma hizo kutoka nje ya nchi na usimamizi madhubuti wa uagizaji na uhifadhi wa malighafi na vifaa vinavyoagizwa kutoka nje (appropriate investory management);

(xii) Kuendelea kujenga uwezo wa kuandaa miradi inayokidhi vigezo na utaratibu wa PPP na njia mbadala za ugharamiaji ili kupunguza mzigo kwa Serikali;

(xiii) Kuendelea kuajiri wahandisi na wataalamu watakaosimamia utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo;


(xiv) Kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya ndani, kubuni vyanzo vipya vya mapato na kutafuta masoko ya bidhaa nje ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia Mpango na Bajeti. Aidha, Serikali inaendelea na kufuatilia mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa Taasisi mbalimbali ili kuweza kutekeleza miradi ya kipaumbele;

(xv) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuendelea kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki; na

(xvi) Kuhamasisha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji wa vifaa vya ujenzi ili kukidhi mahitaji ya soko yaliyoongezeka.

# 3.

# MAENEO YA KIPAUMBELE, 2024/25



# SURA YA TATU

# MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2024/25

## 3.1. Utangulizi

Sura hii inabainisha maeneo mahsusi ambayo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitapaswa kuzingatia wakati wa kuibua miradi ya kipaumbele itakayojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Utekelezaji wa Mpango huu ni nyenzo muhimu katika kutimiza malengo ya Dira 2025 kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 na huhakikisha kuwa shabaha za Mpango zinafuatiliwa na kusimamiwa kila mwaka ili kuhamasisha matumizi bora ya rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi hivyo kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini.

Katika mwaka 2022/23 na 2023/24, Serikali ililenga kukamilisha utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo pamoja na kuimarisha viashiria vya uchumi jumla na viashiria vya maendeleo ya watu. Kutokana na changamoto mbalimbali zilizoainishwa katika sehemu ya 2.4.2 ya Mapendekezo haya, utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo haukukamilika na matokeo tarajiwa hayakufikiwa katika kipindi husika. Kadhalika, baadhi ya shabaha za viashiria vya uchumi jumla hazikufikiwa. Hivyo, Mpango unaotarajiwa kutekelezwa katika mwaka 2024/25 utatambua muendelezo wa hatua za Mipango iliyopita ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuhakikisha kuwa malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 yanafikiwa.

Kwa kuzingatia rasilimali chache zilizopo, msukumo mkubwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25 ni kukamilisha miradi na programu za maendeleo zinazoendelea hususan ambazo ziko nyuma katika ratiba ya utekelezaji. Aidha, miradi mipya itakayosajiliwa italenga kuleta matokeo ya haraka (quick wins) ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi (accelerate growth) ambao ni jumuishi na shiriki (inclusive and participatory growth) yenye lengo la kuongeza mapato ya Serikali; kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni pamoja na kukuza ustawi na maendeleo ya watu. Vilevile, katika lengo la kupunguza utegemezi wa Bajeti ya Serikali katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa 2024/25 na mingine ijayo, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zitapaswa kuonyesha namna zitakavyotumia mitaji na ujuzi kutoka sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi katika utekelezaji wa miradi inayovutia sekta binafsi.

Kadhalika, kwa kuwa Mpango wa Mwaka 2024/25 ni wa nne katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Wizara, Idara

Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuainisha shabaha za utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zitakazotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2024/25 ili kuwezesha kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Tatu katika mwaka husika.

## 3.2. Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

### 3.2.1. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

Malengo na shabaha kuu katika kipindi cha mwaka 2024/25 na kipindi cha muda wa kati ni:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa ili kuiwezesha nchi kufikia malengo ya Dira ya Taifa Maendeleo ya 2025. Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2024;

(ii) Kuwa na mfumuko wa bei himilivu na tulivu ili kuwezesha uendeshaji wenye tija wa shughuli za kiuchumi. Mfumuko wa Bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi 7.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 12.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2024/25 kutoka uwiano halisi wa asilimia 11.9 uliofikiwa mwaka 2022/23 ili kuiwezesha Serikali kuwa na vyanzo vya uhakika vya rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo;

(iv) Kudhibiti ukuaji wa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.2 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 2.7 ya mwaka 2023/24 ili kuipa Serikali uwezo wa kibajeti (fiscal space) wa kutekeleza miradi na programu za maendeleo;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

(vi) Kupunguza nakisi kwenye urari wa biashara na huduma kwa kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

### 3.2.2. Misingi *(Assumptions)* ya Mpango kwa Mwaka 2024/25

Misingi itakayozingatiwa kufikia shabaha ya uchumi jumla ni pamoja na:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za kiuchumi;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko, mafuriko);

(iii) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; na

(iv) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; na

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani.

(vi) Kupanuka kwa mtandao wa mkongo wa mawasiliano wa Taifa na miundombinu ya mawasiliano ili kuwezesha ustawi wa Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy) na ufanisi katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4th Industrial Revolution) yanayoongozwa na mandeleo ya kasi ya teknolojia ya habari.

## 3.3. Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2024/25

### 3.3.1. Miradi ya Kielelezo

(i) Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway)
(ii) Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115
(iii) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL);
(iv) Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)
(v) Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania);
(vi) Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi;
(vii) Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika Vitalu vya Kimkakati vya Mnazi Bay Kaskazini na Eyasi Wembere;
(viii) Makaa ya Mawe (Mchuchuma - Njombe) na Chuma (Liganga - Njombe);
(ix) Kuendeleza miundombinu ya msingi katika Kanda Maalumu za Kiuchumi – Eneo maalumu la Uwekezaji Bagamoyo; na
(x) Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) – Njombe.

### 3.3.2. Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

#### 3.3.2.1. Kuimarisha Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji

**Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma**

**A. Reli**

(i) Kuboresha miundombinu ya reli iliyopo (Metre Gauge Railway - MGR) na reli ya TAZARA – (Cape gauge Railway - CGR);
(ii) Ununuzi na ukarabati wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vichwa vya treni, injini, mabehewa (rolling stock) na mitambo ya ukaguzi wa reli; na
(iii) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu na utoaji wa mafunzo ya reli na teknolojia ya usafiri.

**B. Barabara, Madaraja na Vivuko**

(i) Kuboresha miundombinu ya mtandao wa barabara ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu hiyo; na
(ii) Kujenga na kukarabati vivuko na miundombinu yake.

**C. Usafiri Majini**

**Meli**

(i) Kuendelea na Ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli za kubeba abiria na mizigo katika Maziwa Makuu na Bahari;

(ii) Kuimarisha usafiri, usalama na mawasiliano katika Maziwa Makuu nchini;

(iii) Kuendelea na utoaji wa mafunzo kuhusu ujenzi wa meli na teknolojia ya usafiri wa majini;

(iv) Kujenga uwezo wa taasisi za mafunzo ya usafiri majini.

**A. Bandari**

(i) Kuboresha miundombinu na huduma katika bandari za bahari na Maziwa Makuu;

(ii) Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari nchini; na

(iii) Kuendelea na Ujenzi wa bandari kavu.

**D. Usafiri wa Anga**

(i) Kuendelea na uimarishaji wa miundombinu katika viwanja vya ndege vilivyopo na kujenga viwanja vipya;

(ii) Uimarishaji wa usalama wa usafiri wa anga; na

(iii) Kujenga uwezo wa taasisi za usafiri wa anga.

**E. Hali ya Hewa**

Kuimarisha miundombinu ya huduma za hali ya hewa na mafunzo ya hali ya hewa nchini.

**F. Nishati**

(i) Kuongeza uzalishaji wa umeme kutokana na vyanzo mbalimbali;

(ii) Kujenga na kukarabati miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme mijini, vijijini na kwenye vitongoji;

(iii) Kuendeleza shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia;

(iv) Kujenga miundombinu ya kuwezesha biashara ya nishati ya mafuta na gesi asilia nje ya nchi; na

(v) Kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia majumbani na viwandani.

**3.3.2.2. Mapinduzi ya Nne ya Viwanda na Mabadiliko ya Kidijitali na TEHAMA**

(i) Kuwezesha kujenga Mfumo wa Taifa wa Anwani za Makazi na Postikodi;

(ii) Kupanua na kuongeza uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu na huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa mashirikiano na watoa huduma wa sekta binafsi;

(iii) Kuanzisha Vituo vya Umahiri vya TEHAMA ili kuwezesha Tafiti za Maendeleo, ubunifu, kuhimiza uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa mpya za TEHAMA na

kuwezesha kupatikana kwa Hati miliki za bunifu;
(iv) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi vya sekta ya Habari;
(v) Kuboresha miundombinu kwa ajili ya matumizi ya teknolojia ikiwemo mageuzi ya kidigitali au mapinduzi ya nne ya viwanda; na
(vi) Kuboresha na kuimarisha mawasiliano mijini na vijijini.

#### 3.3.2.3. Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi

**A. Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge**
(i) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya Bunge; na
(ii) Kuendelea kulijengea Bunge uwezo kwa kutoa mafunzo kwa waheshimiwa wabunge na watumishi.

**B. Maboresho ya Mahakama**
(i) Kuimarisha utawala wa Sheria na utoaji wa haki;
(ii) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Utoaji Haki nchini; na
(iii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma kwa umma.

**C. Utawala Bora na Utawala wa Sheria**

**(a) Utawala wa Sheria**
(i) Kuimarisha utawala wa sheria na uzingatiwaji wa masuala ya kikatiba;
(ii) Kuboresha mazingira na miundombinu ya utoaji haki;
(iii) Kuimarisha utoaji wa elimu ya Katiba na uraia kwa umma;
(iv) Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria ikiwemo kutekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia;
(v) Kuimarisha usajili wa matukio muhimu ya kibinadamu (vital statistics) nchini;
(vi) Kuboresha mfumo wa haki jinai; na
(vii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za sheria nchini.

**(b) Ikulu**
(i) Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya Ikulu na Ikulu ndogo; na
(ii) Kuendelea na jitihada za kupunguza kiwango cha umaskini pamoja na kuongeza ajira nchini.

**(c) Uratibu wa Shughuli za Serikali**
(i) Kuendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba – Dodoma; na
(ii) Kufanya maboresho ya mifumo ya uratibu wa shughuli za Serikali.

**(d) Uhamiaji, Magereza na Huduma za Zimamoto na Uokoaji**
(i) Kuendelea kuimarisha usalama wa raia na mali zao;

(ii) Kuboresha utendaji kazi wa vyombo vya ulinzi na usalama;
(iii) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyombo vya ulinzi na usalama;
(iv) Kuendelea kuimarisha shughuli za uzalishaji mali katika mashamba na Viwanda vya Magereza; na
(v) Kuendelea kusajili na kutambua watu wote waishio nchini wakiwemo raia, wageni wakaazi na wakimbizi.

**(e) Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

(i) Kuendelea kuimarisha uwepo wa amani, usalama na umoja.

**D. Utumishi wa Umma**

(i) Kuratibu uboreshaji wa miundombinu ya huduma katika maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, na Halmashauri;
(ii) Kuendelea kuboresha mifumo na miundo ya uendeshaji wa Serikali na menejimenti ya utumishi wa umma ili kutoa huduma bora kwa watumishi wa Umma na wananchi;
(iii) Kuimarisha miundombinu na mifumo ya matumizi ya Serikali Mtandao katika utoaji wa huduma kwa umma; na
(iv) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa makazi ya viongozi wastaafu na Klabu ya Viongozi.

### 3.3.3. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma

#### 3.3.3.1. Uzalishaji Viwandani

(i) Kuhawilisha teknolojia na kuendeleza uzalishaji wa vipuri vitakavyotumika katika sekta zikiwemo za uchukuzi, nishati, kilimo na viwanda;
(ii) Kuwezesha na kuimarisha maabara za utafiti katika maeneo ya uzalishaji na kufanya tafiti za uundaji wa magari na vipuri mbalimbali;
(iii) Kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za viwandani kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini na vifaa vya kisasa;
(iv) Kuboresha na kuongeza ustawi na tija ya viwanda nchini;
(v) Kufanya tafiti na kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora;
(vi) Kuimarisha vituo vya uendelezaji teknolojia na vituo vya uzalishaji na mafunzo kwa wajasiriamali.

#### 3.3.3.2. Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**A. Kilimo**

(i) Kuongeza tija na uzalishaji kwa kufanya utafiti wa mbegu bora; kuzalisha na kusambaza mbegu na miche bora kwa mfumo wa ruzuku; uwekezaji kwenye huduma za ugani; kupima afya ya udongo; kutoa ruzuku ya mbolea na

viuatilifu; na kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji.

(ii) Kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo ikiwemo kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja kupitia programu ya Jenga Kesho iliyo Bora-BBT;

(iii) Kuimarisha usalama wa chakula na lishe ikiwemo uwekezaji kwenye miundombinu ya uhifadhi na kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima.

(iv) Kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi kwa kujenga miundombinu ya masoko na kuimarisha uongezaji thamani kwenye mazao ya kilimo kwa kushirikiana na sekta binafsi.

(v) Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika.

**B. Mifugo**

(i) Kuongeza uzalishaji, uhifadhi wa malisho na vyakula vya mifugo pamoja na kuimarisha upatikanaji wa maji kwa mifugo;

(ii) Kuongeza fursa ya mafunzo ya ufugaji kwa vitendo na ajira kwa vijana na wanawake kupitia programu ya BBT-LIFE;

(iii) Kuimarisha miundombinu, uzalishaji na uwekezaji katika sekta ya mifugo nchini;

(iv) Kuimarisha afya ya mifugo hususan kupitia kuhamasisha wafugaji kuchanja na kuogesha mifugo kwa wakati, pamoja na ujenzi wa maabara ya kuzalisha chanjo zinazoagizwa nje ya nchi kwa ajili ya magonjwa ya vipaumbele; na

(v) Kuimarisha mafunzo na tafiti za mbegu, mifugo na masoko na kuboresha mifumo na taarifa za masoko ya mazao ya mifugo ili kuongeza tija na kupunguza upotevu wa mazao hayo (reducing post-harvest losses).

**C. Uvuvi**

(i) Kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari kuu;

(ii) Kuimarisha taasisi za uvuvi ili kuongeza ushiriki katika uchumi wa buluu (Blue Economy);

(iii) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi;

(iv) Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji;

(v) Kuimarisha uthibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji;

(vi) Kuimarisha huduma za ugani wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji; na

(vii) Kuongeza ajira kwa vijana na wanawake kwa uvuvi na ukuzaji viumbe maji kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyobora BBT – LIFE.

**3.3.3.3. Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia**

(i) Kuendelea kufanya utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege (High-resolution Airborne Geophysical Survey);

(ii) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji maduhuli na utoaji wa leseni;

(iii) Kuimarisha uwekezaji na teknolojia katika Sekta ya Madini ili kuendeleza

madini muhimu na madini mkakati ; na

(iv) Kuhamasisha uwekezaji, biashara na uongezaji thamani katika Sekta ya Madini.

#### 3.3.3.4. Huduma

##### 3.3.3.4.1. Maliasili na Utalii

(i) Kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ya Fukwe na mazao mengine ya utalii;

(ii) Kuimarisha na kuboresha miundombinu ya kitalii katika maeneo ya malikale na makumbusho;

(iii) Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali za wanyamapori, Misitu na Ufugaji nyuki na Malikale;na

(iv) Kuendelea kutekeleza mipango na mikakati ya uhifadhi na uongezaji wa kiwango cha uzalishaji pamoja na thamani ya mazao ya misitu na nyuki;

##### 3.3.3.4.2. Tasnia ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

(i) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya msingi ya michezo na kazi za sanaa na ubunifu;

(ii) Kutambua, kukusanya, kuendeleza, kulinda na kuhifadhi kumbukumbu na taarifa za Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika unaoshikika na usioshikika ndani na nje ya nchi;

(iii) Kuratibu utoaji wa mikopo na mafunzo kwa wadau wa sekta ya utamaduni na Sanaa;

(iv) Kuimarisha, kukuza na kubidhaisha Kiswahili Kitaifa, Kikanda na Kimataifa; na

(v) Kuimarisha mifumo ya kisera na kisheria ya usimamizi wa Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo.

### 3.3.4. Kukuza Biashara na Uwekezaji

#### 3.3.4.1. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji

(i) Kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kutunga Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo ili kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia Uwekezaji nchini;

(ii) Uendelezaji wa Miundombinu kwa ajili ya uwekezaji ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi; na

(iii) Kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wawekezaji katika ngazi zote.

#### 3.3.4.2. Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Kuimarisha Mifuko na Programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

#### 3.3.4.3. Kukuza Sekta Binafsi

(i) Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo nchini; na
(ii) Kuimarisha utendaji wa mabaraza ya biashara katika ngazi za mikoa na wilaya.

#### 3.3.4.4. Huduma za Biashara na Masoko

(i) Kuimarisha masoko ya ndani na nje kwa kuratibu matukio ya ukuzaji biashara ikiwemo maonesho;
(ii) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu upatikanaji wa masoko ya mazao na bidhaa;
(iii) Kuimarisha na kuboresha huduma na mifumo ya upatikanaji wa Taarifa za Biashara na Masoko;
(iv) Kuendelea kutoa elimu kwa wadau namna Soko la Bidhaa linavyofanya kazi
(v) Kuongeza bidhaa zaidi ziuzwe kupitia Soko la Bidhaa (TMX) ikiwepo madini ya vito, mifugo hai na kupanua mauzo ya kahawa katika mikoa mingine inayozalisha kahawa; na
(vi) Kuendelea kuboresha mfumo wa mauzo wa Soko la Bidhaa kulingana na matakwa ya bidhaa husika.

#### 3.3.4.5. Ushirikiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia

(i) Kuimarisha utekelezaji wa diplomasia ya uchumi;
(ii) Kuendelea na ujenzi na uboreshaji wa majengo ya vitega uchumi, ofisi na makazi ya watumishi kwenye Balozi za Tanzania Nje;
(iii) Kuimarisha ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; na
(iv) Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika shughuli za kikanda na kimataifa ikiwemo Taasisi za Kimataifa ambazo Tanzania ni mwanachama.

### 3.3.5. Kuchochea Maendeleo ya Watu

#### 3.3.5.1. Afya

(i) Kuratibu na kusimamia shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, lishe na ustawi wa jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(ii) Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ya msingi kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri;
(iii) Kuimarisha ubora wa huduma za afya katika vituo vya umma na kuongeza utolewaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi;
(iv) Kuimarisha miundombinu na Mifumo ya TEHAMA;
(v) Kuimarisha mafunzo katika fani za ubingwa na bingwa bobezi; na
(vi) Kusimamia tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za Afya pamoja kuendeleza tiba asili na tiba mbadala nchini.

#### 3.3.5.2. Ustawi na Maendeleo ya Jamii

(i) Kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi (Generation Equality Forum - GEF);
(ii) Kuhamasisha utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto;
(iii) Kuwezesha wafanyabiashara ndogondogo (machinga) kiuchumi; na
(iv) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi za Ustawi wa Jamii na vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

#### 3.3.5.3. Elimu

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimumsingi na sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(ii) Kuratibu utolewaji wa elimumsingi na sekondari bila ada;
(iii) Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za elimumsingi na sekondari;
(iv) Kuhuisha sera, mitaala, sheria na miongozo ya utoaji wa elimu na mafunzo nchini;
(v) Kuongeza fursa za elimu kwa wote hususan Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Mafunzo ya Amali) na elimu ya juu;
(vi) Kuimarisha ubora wa elimu ya awali, elimu ya msingi, sekondari na elimu ya ualimu, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (mafunzo ya amali) na elimu ya juu;
(vii) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu nchini; na
(viii) Kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya Taifa.

#### 3.3.5.4. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

(i) Kuendelea na upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini;
(ii) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi;
(iii) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi;
(iv) Kuendelea na miradi ya kuendeleza makazi ili kukabiliana na upungufu wa nyumba bora nchini;
(v) Kuimarisha mipaka ya kimataifa.

#### 3.3.5.5. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira

(i) Kuendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini;
(ii) Kuendelea kuimarisha usimamizi, uendelezaji, uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji;
(iii) Kuendelea kuimarisha huduma ya usimamizi wa ubora wa maji nchini; na
(iv) Kuendelea na ujenzi wa mabwawa ya kimkakati, ukubwa wa kati na madogo kwa ajili ya kuongeza uhifadhi wa rasilimali za maji ili kukabiliana na athari za

mabadiliko ya tabianchi.

**3.3.5.6. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

(i) Kuratibu utekelezaji wa Sera, mipango na sheria za usimamizi wa mazingira;
(ii) Kuendelea kujenga uwezo na kutoa elimu kwa jamii kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi;
(iii) Kuendelea kuboresha miundombinu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira;
(iv) Kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira; na
(v) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu (Blue Economy) nchini.

**3.3.6. Kuendeleza Rasilimali Watu**

(i) Kutekeleza Programu ya kukuza ujuzi na kuchochea ukuzaji wa fursa za ajira kwa nguvukazi iliyopo nchini ili kuongeza ajira kwa vijana na watu wenye ulemavu;
(ii) Kuimarisha mafunzo ya utarajai (internship training) na mafunzo ya uanagenzi (apprenticeship) ili kuwajengea uwezo wa kushindana katika soko la ajira kwa kushirikiana na sekta binafsi;
(iii) Kukuza kazi za staha Nchini;
(iv) Kutoa Mikopo kwa vijana kupitia miradi yao ya Biashara; na
(v) Kuimarisha vituo vya ufundi Stadi vya Watu wenye ulemevu.

**3.3.7. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

(i) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uendelezaji wa miundombinu ya reli na utoaji wa huduma kwenye viwanja vya ndege;
(ii) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji na utoaji huduma kwenye miradi ya mafuta na gesi asilia;
(iii) Kuratibu uanzishwaji wa kituo cha ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP Centre);
(iv) Kuimarisha uendeshaji na utafutaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya mfuko wa Taifa wa uwezeshaji wa ubia (National PPP Facilitation Fund);
(v) Kuendelea kujenga uelewa kwa watalaamu wa Mamlaka za Serikali kuhusu PPP ikiwemo maandalizi ya nyaraka za mradi na kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika miradi ya PPP;
(vi) Kuratibu maandalizi na utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; na
(vii) Kuendelea na mashirikiano na Sekta Binafsi katika kuibua miradi ya PPP ambayo haijaibuliwa na mamlaka za serikali.

# 4.

# UGHARAMIAJI WA MPANGO, 2024/25



# SURA YA NNE

# UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2024/25

## 4.1. Utangulizi

Sura hii inaainisha mahitaji ya Serikali katika kugharamia Mpango wa Maendelo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Aidha, sura hii inaainisha mikakati ambayo Serikali itakayoitekeleza ili kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali vinafikiwa katika ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25, Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kutekeleza vipaumbele vilivyowekwa ikiwa ni pamoja na kutenga rasilimali fedha za kutosha kwa ajili ya ugharamiaji wa Mpango huu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## 4.2. Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2024/25

Katika mwaka 2024/25, Serikali inatarajia kutumia kiasi cha shilingi bilioni 15,325.1 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo. Fedha hizi zitakusanywa kutoka katika mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, misaada na mikopo nafuu, mikopo ya ndani na mikopo ya nje yenye masharti ya biashara. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo kupitia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) na kwa kutumia njia Mbadala (Alternative Project Financing-APF) ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

## 4.3. Vyanzo vya Mapato ya Kugharamia Mpango kwa Mwaka 2024/25

Katika kugharamia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25, vyanzo vya mapato vitakavyotumika ni mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, mikopo na misaada pamoja na vyanzo mbadala vya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo.

## 4.4. Mapato ya Ndani

### 4.4.1. Mapato ya Kodi na Yasiyo ya Kodi

Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ndani ili kuwezesha kufikia malengo yaliyowekwa kwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya kodi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti za kielektroniki wanapouza bidhaa na wateja wanadai risiti wanaponunua bidhaa;

(ii) Kuendelea kutoa elimu ya kodi kwa mlipakodi kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, semina na warsha;

(iii) Kupanua wigo wa kodi kwa kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara

katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi kupitia kampeni ya Mlango kwa Mlango;

(iv) Kuendelea kutumia Mpango wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (Compliance Risk Management Plan) ili kubaini wakwepaji wa kodi;

(v) Kuimarisha ushirikiano baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na vyombo vya ulinzi na usalama nchini ili kudhibiti bidhaa za magendo na tatizo la ukwepaji wa kodi katika mipaka yote ya Tanzania;

(vi) Kuimarisha mazingira rafiki ya ulipaji kodi kwa hiari kwa kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo itakayosaidia kurahisisha ulipaji kodi;

(vii) Kuhamasisha ulipaji kodi katika sekta isiyo rasmi kwa kuijumuisha kwenye mfumo rasmi wa ulipaji kodi;

(viii) Kurasimisha shughuli zisizo rasmi zikiwemo shughuli za wajasiriamali wadogo kwa kuwatambua na kuwatengea maeneo maalum;

(ix) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wapya, kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi utakaowezesha kuongeza wigo wa kodi;

(x) Kufanya tafiti katika maeneo mapya ambayo yanaweza kuwa vyanzo vya mapato;

(xi) Kuimarisha usimamizi wa tozo na ada mbalimbali ili kuhakikisha zinakusanywa na kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

(xii) Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kufuatilia Mizigo inayokwenda nchi jirani (Eletronic Cargo Tracking System) ili kuzuia uwezekano wa kuingiza bidhaa hizo katika soko la ndani na kuikosesha Serikali mapato;

(xiii) Kuendelea kusimamia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (Government Electronic Payment Gateway- GePG) ili kurahisisha ulipaji na kudhibiti upotevu wa mapato;

(xiv) Kuimarisha mfumo wa Dirisha Moja la Kielektroniki la Uondoshaji wa Mizigo Bandarini (e-Single Window System) ili kurahisisha uondoshwaji wa mizigo katika vituo vya mipakani pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini;

(xv) Kuimarisha na kufungamanisha Mfumo wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani (Integrated Domestic Revenue Administration System - IDRAS) utakaounganisha mifumo yote ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Serikali ili kuimarisha usimamizi wa mapato yatokanayo na kodi za ndani nchini;

(xvi) Kuboresha Mfumo wa mawasiliano kati ya NIDA na TRA ili kurahisisha usajili na ufuatiliaji wa walipakodi; na

(xvii) Kuimarisha usimamizi wa Mashirika, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati.

## 4.5. Mikopo na Misaada

### 4.5.1. Mikopo ya Nje

Serikali itaendelea kukopa kwa kuzingatia Mkakati wa Usimamizi wa Madeni wa Muda wa Kati 2022/23 - 2024/25 (Medium Term Debt Strategy - MTDS) ili kuhakikisha grahama za ukopaji ni nafuu na vihatarishi vinavyohimilika. Hivyo, Serikali itaipa zaidi kipaumbele mikopo yenye masharti nafuu, na mikopo yenye masharti ya kati kwa kutumia utaratibu wa udhamini kutoka taasisi za udhamini wa mikopo (Export Credit Agencies – ECAs) ambayo masharti yake yana unafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara. Aidha, mikopo yenye masharti ya kibiashara itatumika zaidi kugharamia miradi inayochochea ukuaji wa uchumi kwa kasi na kuongeza mauzo ya biashara nje. Serikali itaendelea kufanya majadiliano na wadau wa maendeleo na taasisi za fedha ili kuhakikisha kwamba kiasi kilichopangwa kukopwa ili kiziba nakisi ya bajeti ya mwaka 2024/25 kinapatikana. Serikali itatumia njia mbalimbali za ukopaji kama Partial Credit Guarantee ili kuhakikisha inapunguza gharama za mikopo ya kibiashara.

### 4.5.2. Mikopo ya Ndani

Katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea kukopa katika soko la ndani kupitia hatifungani za Serikali kwa kuzingatia Mkakati wa Usimamizi wa Madeni wa Muda wa Kati 2022/23 - 2024/25. Vilevile, katika muda wa kati, Serikali itatumia hatifungani za muda mrefu na mfupi ili kupunguza gharama na vihatarishi kwenye deni la Serikali. Serikali itaendelea na mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kiasi kilichopangwa kukopwa katika soko la ndani kinapatikana bila kuathiri ukopaji wa sekta binafsi na kuongeza ushindani. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu zaidi kwa nchi wanachama wa SADC na watanzania waishio nje ya nchi (Diaspora) ili waweze kuwekeza katika dhamana za Serikali.

### 4.5.3. Misaada ya Nje

Serikali itaendelea kuimarisha mahusiano na washirika wa maendeelo ikiwa ni pamoja na kutekeleza maazimio ya kimataifa kuhusu kanuni za ufanisi wa ushirikiano wa maendeleo kupitia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Framework- DCF) kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zinazopokea fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Katika hatua nyingine, Serikali inaendelea na mapitio ya muda wa kati ya utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) pamoja na Mpango Kazi wake (API-DCF). Mapitio hayo yatasaidia kubainisha maeneo yenye mafanikio na changamoto katika ushirikiano, kutoa mapendekezo yatakayoimarisha na kuboresha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo pamoja na kutambua fursa zinazoweza kutumika katika ushirikiano huo.

Vile vile, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zikiwemo fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mfumo wa D-Fund Management

Information System (DMIS) ili kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo na kupata matokeo yaliyokusudiwa.

### 4.6. Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Kugharamia Miradi ya Maendeleo

Katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilianza kutekeleza Mkakati wa Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo kupitia njia Mbadala (APF) ambapo mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupitia Hatifungani za Manispaa – Municipal Bonds; Hatifungani ya Miundombinu, Hatifungani ya Buluu, Hatifungani za Makampuni, Dhamana za Muda wa Kati, Hatifungani ya Mazingira, Hatifungani ya Kiislam, *Micro-Saving Bond na Lease Financing*, mitaji ya muda mrefu kupitia utaratibu wa *syndication* na bima na ugharamiaji hatarishi kwa lengo la kupata fedha kugharamia miradi ya kimkakati katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Umoja wa Mataifa – *United Nation Capital Development Fund* (UNCDF) inaendelea kufanyia kazi maandiko ya miradi kutoka katika Mamlaka za Maji nchini ambazo zimeonesha muelekeo mzuri wa kutekeleza miradi ya maji kupitia Mkakati wa APF. Mamlaka hizo ziko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wa Maandiko hayo zikiongozwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (TANGA UWASA) ambayo ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha andiko lao la mradi linalolenga kuboresha na kuongeza utoaji wa huduma za maji katika Mji wa Tanga. Mamlaka hii inatarajia kuorodhesha Hatifungani ya Kijani kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ifikapo Desemba, 2023 ambayo itawawezesha kupata fedha za kugharamia Mradi. Utoaji wa Hatifunganii hii ya kwanza ya Kijani, kwa Mamlaka ya Maji Nchini, unategemewa kutoa mwamko mkubwa na msukumo kwa Taasisi nyingine za Umma kutumia njia Mbadala za Ugharamiaji wa Miradi (APF) katika kugharamia Miradi ya Maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa mikoa na Halmashauri mbalimbali pamoja na ukamilishaji wa miongozo ya *sustainable finance bond na sustainable taxonomy framework.*



# 5. UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

# SURA YA TANO

# UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

## 5.1. Utangulizi

Ufuatiliaji na Tathmini (U&T) ni nyenzo muhimu ya kuiwezesha Serikali katika kuhakikisha kuwa programu na miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa ufanisi, inafikia malengo yaliyowekwa na inatoa matokeo yanayotarajiwa kulingana na vipaumbele vilivyowekwa. Hii inasaidia kufanya maamuzi yanayoongozwa na uwepo wa taarifa na takwimu zilizosahihi kwa wakati. U&T pia husaidia kupima mwelekeo wa kufikia malengo na matokeo tarajiwa yaliyowekwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22- 2025/26). Kwa msingi huo, Serikali itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 kupitia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo wa Mwaka 2022; Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25; Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma; Sheria ya Bajeti, Sura 439; Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha; Waraka Na. 5 wa Hazina wa Mwaka 2020/21 Kuhusu Matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS); na Waraka Na. 1 wa Hazina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti.

Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa utafanyika katika ngazi mbalimbali ambapo katika kila ngazi itaandaliwa taarifa ambayo itawasilishwa kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo baina ya watekelezaji na waratibu wa miradi na programu za maendeleo. Taarifa hizo zitajumuisha: taarifa za utekelezaji wa miradi za kila robo mwaka; na taarifa za ufuatiliaji na tathmini. Taarifa za ufuatiliaji na Tathmini zitaandaliwa kwa kuzingatia viashiria vilivyowekwa katika mfumo madhubuti au bangokitita la mradi (Logframe) na kuziwasilisha kila mwezi kupitia NPMIS. Aidha, watekelezaji wote wa miradi ya maendeleo wanatakiwa kuzingatia maelekezo ya Waraka Na. 5 wa Hazina wa mwaka 2020/21 kuhusu matumizi ya NPMIS.

## 5.2. Misingi na Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina wajibu wa kuzingatia maelekezo kuhusu misingi na mbinu kama zilivyoainishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo wa Mwaka 2022. Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini umeainisha mfumo utawezesha kupatikana kwa taarifa za utekelezaji kwa lengo la kuwezesha watunga sera, wafanya maamuzi na wadau muhimu kufahamu mwenendo wa utekelezaji wa mipango, miradi na programu za maendeleo kwa kuzingatia hatua iliyofikia pamoja na mafanikio na changamoto ya utekelezaji wa malengo.

### 5.3. Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo yanawezesha kubaini hatua iliyofikiwa kwenye utekelezaji, mafanikio, changamoto na ushauri wa namna bora ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo. Aidha, taasisi zote zinazofanya ufuatiliaji na tathmini zinaelekezwa kutoa mrejesho wa ufuatiliaji kwa wadau wote wanaohusika na utekelezaji wa programu na miradi kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyobainishwa.

### 5.4. Muundo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ikiwa ni pamoja na: mawanda na malengo ya mradi, hali ya utekelezaji, taarifa za ugharamiaji, taarifa za mikataba, changamoto na mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, muundo wa Taarifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Miaka Mitano utatolewa na Ofisi ya Rais Tume ya Mipango na kujadiliwa na wadau kila mwaka ambao utawezesha uchambuzi wa matokeo tarajiwa yaliyoainishwa katika maeneo ya kipaumbele.

### 5.5. Mgawanyo wa Majukumu

Ufuatiliaji na Tathmini ni suala mtambuka kwa sababu linahusisha wadau mbalimballi katika ngazi tofauti. Ushirikishwaji wa wadau muhimu katika kufanikisha ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango ni suala la msingi na la kipaumbele kwa Serikali. Aidha, mgawanyo wa majukumu umefafanuliwa vyema katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo ambao umeainisha wadau mbalimbali na majukumu yao mahsusi katika ufuatiliaji na tathmini. Ufuatiliaji huo utafanyika kwa kutumia uchambuzi wa kina juu ya matokeo tarajiwa kupitia tafiti na takwimu zilizozalishwa na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

# 6. VIHATARISHI NA MIKAKATI YAKE



# SURA YA SITA

# VIHATARISHI NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO

## 6.1. Utangulizi

Katika kuhakikisha malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 yanafikiwa kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya, Mpango huu umezingatia Mwongozo wa Kuandaa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma wa Mwaka 2012, ambapo Serikali itahakikisha utekelezaji wa Mpango unaenda sambamba na utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza. Vihatarishi hivyo ni vya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ambavyo vinaweza kusababisha mradi kutotekelezwa, kutekelezwa chini ya kiwango, kuongezeka gharama au kutokamilika kwa wakati. Aidha, vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo vimegawanyika katika makundi mawili (2) ambayo ni vihatarishi vya ndani vitakavyotokana na utendaji au mifumo ya Serikali na vihatarishi vya nje vitakavyotokana na masuala yaliyoko nje ya udhibiti wa Serikali.

## 6.2. Vihatarishi vya Ndani na Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo

**Vihatarishi vya Ndani:** Hivi ni vihatarishi ambavyo Serikali ina uwezo wa kuvizuia kutokea. Vihatarishi hivyo ni pamoja na: Ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo; ushiriki usioridhisha wa sekta binafsi katika kutekeleza mipango ya maendeleo; upotevu wa mapato ya Serikali unaotokana na biashara mtandao; mabadiliko ya viwango vya riba katika soko la fedha la ndani; uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za binadamu; na vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa rasilimali. Serikali ina uwezo wa kudhibiti kutokea au kukabili athari za vihatarishi hivi kupitia utekelezaji wa mikakati iliyowekwa.

**Vihatarishi vya Nje:** Hivi ni vihatarishi ambavyo Serikali haina uwezo wa kuvizuia visitokee lakini inaweza kuweka mikakati ya kupunguza madhara endapo vitatokea. Vihatarishi hivyo ni pamoja na: mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko; mdororo na mitikisiko ya kiuchumi duniani; kuongezeka kwa kiwango cha riba katika masoko ya kimataifa; migogoro na hali ya siasa inayojitokeza kwa nchi jirani, kikanda na kimataifa; na kuongozeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

Uchambuzi wa vihatarishi vya ndani na nje pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo umeainishwa katika **Jedwali Na. 6 na 7.**

**Jedwali Na. 5: Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo**

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| 1. | Ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. | (i) Kutotekelezwa kwa miradi au kasi ndogo ya utekelezaji na hivyo kutokamilika kwa wakati;<br>(ii) Miradi kutekelezwa chini ya kiwango;<br>(iii) Kuongezeka kwa gharama za mradi; na<br>(iv) Kuchelewa kwa upatikanaji wa huduma zilizotarajiwa. | (i) Kusimamia utekelezaji wa sera za ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuhakikisha kila mfanyabiashara anatoa risiti ya kielektroniki anapouza bidhaa au huduma;<br>(ii) Kuongeza upatikanaji na matumizi ya huduma rasmi za benki na malipo;<br>(iii) Kuongeza wigo wa walipa kodi kwa kuhakikisha sekta isiyo rasmi inajumuishwa katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi;<br>(iv) Kudhibiti upotevu wa mapato kwa kusimamia ipasavyo mifumo ya ukusanyaji, ikiwemo Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (Government Electronic Payment Gateway - GePG);<br>(v) Kutekeleza miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa PPP;<br>(vi) Kuimarisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye kuongeza mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;<br>(vii) Kuimarisha na kuendeleza soko la fedha la ndani *(domestic debt market)* |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | | | ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo;<br>(viii) Kutafuta fedha kutoka kwenye mikopo yenye masharti nafuu; na<br>(ix) Kuhamasisha matumizi ya vyanzo mbadala na bunifu vya utekelezaji wa mradi. |
| 2. | Ushiriki usioridhisha wa Sekta binafsi katika kutekeleza mipango ya maendeleo | (i) Tija na ukuaji mdogo wa sekta za uzalishaji; na<br>(ii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi kutokana na uhaba wa mitaji, teknolojia na mazingira duni ya kufanya biashara. | (i) Kufanya majadiliano na Sekta binafsi ili kuweka mikakati ya kutatua changamoto zinazowakabili;<br>(ii) Kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya biashara ili kuvutia uwekezaji katika maeneo yanayofaa kwa Sekta binafsi; na<br>(iii) Kuziwezesha kifedha taasisi za Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kufanya upembuzi yakinifu kwa miradi ya PPP na kuiuza kwa Sekta Binafsi kwa ajili ya uwekezaji. |
| 3. | Upotevu wa mapato ya Serikali unaotokana na biashara ya mtandaoni | (i) Kupungua kwa mapato ya Serikali; na<br>(ii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. | (i) Kuongeza matumizi ya kidigitali katika ukusanyaji wa kodi kwa kutumia mifumo ya Serikali; na<br>(ii) Kudhibiti upotevu wa mapato kwa kuboresha usimamizi wa mifumo ya kisheria iliyopo. |
| 4. | Mabadiliko ya viwango vya riba | (i) Kuongezeka kwa matumizi ya malipo ya | (i) Kuendelea kutekeleza Sera za fedha |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | katika soko la fedha la ndani na nje. | riba na nakisi ya bajeti; na<br>(ii) Sekta binafsi kutofikia malengo ya mikopo na hivyo kupungua kwa shughuli za kiuchumi na kusababisha Serikali kukosa mapato. | zitakazowezesha viwango vya riba kuwa himilivu;<br>(ii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ili kupunguza utegemezi katika misaada na mikopo kutoka nje; na<br>(iii) Kuimarisha soko la fedha la ndani. |
| 5. | Uharibifu wa Mazingira kutokana na shughuli za binadamu. | (i) Kubadilika kwa hali ya hewa na kusababisha uharibifu wa miundombinu kutokana na mvua nyingi;<br>(ii) Kutoweka kwa bioanuai;<br>(iii) Kuongezeka kwa gharama za utoaji wa huduma za afya kutokana na kuongezeka kwa magonjwa yanayotokana na uharibifu wa mazingira;<br>(iv) Kuongezeka kwa gharama za kurejesha mazingira katika hali ya awali na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa; na<br>(v) Kupungua kwa uzalishaji wa mazao na bidhaa viwandani. | (i) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza mazingira ili kuzuia uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu;<br>(ii) Kuhamasisha matumizi ya majiko banifu na mkaa mbadala (briquettes);<br>(iii) Kudhibiti uharibifu wa uoto wa asili na bioanuai;<br>(iv) Kuimarisha usimamizi wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya maji na misitu; na<br>(v) Kutekeleza ipasavyo miongozo na kanuni za usimamizi wa mazingira. |
| 6. | Vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa rasilimali | (i) Upotevu wa fedha za umma;<br>(ii) Miradi kutekelezwa chini ya kiwango;<br>(iii) Kuongezeka kwa muda na gharama za utekelezaji wa miradi; na | (i) Kuimarisha utekelezaji wa sheria ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wanaobainika kuhusika na vitendo vya rushwa;<br>(ii) Kuimarisha shughuli za |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | | (iv) Kasi ndogo ya ukuaji wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya Maendeleo. | ufuatiliaji na tathmini ya miradi;<br>(iii) Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara yaliyoboreshwa na yenye uwazi ili kuruhusu sekta binafsi kushamiri na kurasimisha sekta isiyo rasmi; na<br>(iv) Kuimarisha mfumo wa utoaji motisha kwa watoaji taarifa zinazohusiana na rushwa. |
| 7. | Uhalifu wa kimtandao wa mifumo ya Serikali | (i) Kuharibiwa kwa mifumo ya kielektroniki ya Serikali; na<br>(ii) Upotevu wa mapato na taarifa. | (i) Kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Udhibiti wa Mifumo ya Kielektroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma;<br>(ii) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mifumo ya taarifa ya kielektroniki ya Serikali; na<br>(iii) Kuimarisha usalama wa maeneo ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali (Data recovery sites). |

**Jedwali Na. 6: Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo**

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko | (i) Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi;<br>(ii) Kupungua kwa uzalishaji;<br>(iii) Kuathiri mapato ikiwemo mapato ya kodi yatokanayo na kipato;<br>(iv) Rasilimali fedha kuelekezwa kukabiliana na | (i) Kuboresha mifumo ya kuzuia na kukabiliana na majanga;<br>(ii) Kuimarisha mifuko ya maafa;<br>(iii) Kutekeleza na kuendelea kuridhia itifaki za kimataifa |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | | majanga badala ya kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa; na<br>(v) Kuathiri ikolojia | kuhusu utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi; na<br>(iv) Kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021. |
| 2. | Mtikisiko na Mdororo wa uchumi duniani | (i) Kutopatikana kwa mikopo na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;<br>(ii) Kukosekana kwa masoko ya uhakika ya bidhaa nje ya nchi;<br>(iii) Kupungua kwa uwekezaji kutoka nje ya nchi; na<br>(iv) Kuongezeka kwa bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia zikiwemo bidhaa za mafuta, malighafi na bidhaa za viwandani. | (i) Kuimarisha mikakati ya kisera ili kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi duniani;<br>(ii) Kuendelea kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na kuzalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi nchini; na<br>(iii) Kuimarisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuhimili ushindani katika masoko ya kimataifa. |
| 3. | Migogoro na hali ya siasa isiyo imara ya nchi jirani, kikanda na kimataifa. | (i) Kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu katika soko la dunia kama bidhaa za petroli, mafuta ya kula, vyakula, mashine na mitambo;<br>(ii) Kupungua kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;<br>(iii) Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi hususan inayotumia vifaa kutoka nje;<br>(iv) Kupungua kwa uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja;<br>(v) Kupungua kwa mikopo na | (i) Kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa kutumia teknolojia na malighafi za ndani ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje; na<br>(ii) Kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi Jirani, kikanda na kimataifa ili kukuza masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa viwandani. |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| | | misaada kutoka nje; na<br>(vi) Kukosekana kwa masoko nje ya nchi kwa ajili ya kuuza bidhaa zinazozalishwa nchini. | |
| 4. | Kuongozeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia | (i) Mifumo ya kisheria, kisera, na kitaasisi iliyopo kutoendana na mabadiliko ya teknolojia hivyo kuongezeka kwa gharama za uwekezaji katika mifumo ya teknolojia mpya; na<br>(ii) Kupungua kwa uwezo wa kiushindani katika soko la kikanda na kimataifa. | (i) Kuendelea kuboresha mifumo ya kisheria, kisera na kitaasisi ili iendane na mabadiliko ya teknolojia duniani; na<br>(ii) Kuendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza ujuzi, uhawilishaji wa teknolojia na kuhamasisha ubunifu wa teknolojia kwa wataalam wa ndani. |

**Orodha ya Miradi Iliyofuatiliwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023**

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | Elimu | Ujenzi wa Chuo cha Ualimu Ngorongoro | Arusha |
| 2. | Ujenzi | Ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta - Mugumu/Loliondo - Mto Wa Mbu (km 338) | Arusha |
| 3. | Utawala Bora | Ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Jiji la Arusha | Arusha |
| 4. | Uchukuzi | Uboreshaji kiwanja cha Ndege Arusha | Arusha |
| 5. | Uchukuzi | Ukarabati wa Njia Kuu za Reli (Dar es salaam – Tanga – Arusha) | Arusha |
| 6. | Elimu | Ujenzi wa bweni la wasichana katika Chuo cha Ufundi Arusha – ATC | Arusha |
| 7. | Maji | Ujenzi wa Maji Mageri (Vijiji 8) | Arusha |
| 8. | Uchukuzi | Ujenzi wa Reli ya Kati kwa *Standard Gauge* | Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza |
| 9. | Uchukuzi | Kufufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) | Dar es Salaam |
| 10. | Ujenzi | Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo Haraka (BRT) - Awamu ya II | Dar es Salaam |
| 11. | Viwanda | Maeneo Maalum ya Uwekezaji Kwa Mauzo ya Nje (EPZ) | Dar es Salaam |
| 12. | Ujenzi | Barabara za Kupunguza Msongamano jijini Dar es Salaam (Km 138.5): Ujenzi wa barabara ya Goba – Matosa - Temboni (Km 7), sehemu ya kwanza (km 1) | Dar es Salaam |
| 13. | Ujenzi | Ujenzi wa daraja la Tanzanite (Km 1.03) na barabara unganishi (km 5.5) | Dar es Salaam |
| 14. | Utawala Bora | Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Magereza – Ukonga, dar es salaam | Dar es Salaam |
| 15. | Elimu | Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA | Dar es Salaam |
| 16. | Elimu | Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam – DUCE | Dar es Salaam |
| 17. | Miundombinu | Mradi wa Uendelezaji wa jiji la Dar es Salaam- DMDP | Dar es Salaam |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 18. | Uchukuzi | Mradi wa Uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam – DMGP | Dar es Salaam |
| 19. | Biashara | Ujenzi wa soko la kisasa Kibada (Kigamboni) | Dar es Salaam |
| 20. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi na Makazi Tanzania Bara – Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Kigamboni | Dar es Salaam |
| 21. | Utawala Bora | Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Serikali – Nyumba za Viongozi | Dar es Salaam |
| 22. | Ujenzi | Ujenzi na Ukarabati wa Maegesho ya Vivuko (Magogoni na Kigamboni) jijini Dar es Salaam | Dar es Salaam |
| 23. | Afya | Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Mwananyamala | Dar es Salaam |
| 24. | Afya | Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wodi binafsi - Hospitali ya Taifa ya Muhimbili | Dar es Salaam |
| 25. | Nishati | Mradi wa Usambazaji wa Gesi asilia katika mkoa wa Dar es Salaam | Dar es Salaam |
| 26. | Utawala Bora | Upanuzi wa huduma za zimamoto na uokoaji | Dodoma |
| 27. | Mawasiliano | Upanuzi wa usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) – Dodoma | Dodoma |
| 28. | Utawala Bora | Ujenzi wa jengo la ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Dodoma | Dodoma |
| 29. | Afya | Ujenzi wa Hospitali za wilaya – Halmashauri ya wilaya ya Kondoa | Dodoma |
| 30. | Utawala Bora | Ujenzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya Kondoa | Dodoma |
| 31. | Maji | Ujenzi wa bwawa la Farkwa na mfumo wa kutibu maji | Dodoma |
| 32. | Uchukuzi | Ununuzi wa rada, vifaa vya hali ya hewa na ujenzi wa miundombinu ya hali ya hewa | Dodoma |
| 33. | Kilimo | Kuongeza uhifadhi wa nafaka | Dodoma |
| 34. | Uvuvi | Kujenga Kituo cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji Rubambagwe – Chato | Geita |
| 35. | Ujenzi | Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita – Chato | Geita |
| 36. | Elimu | Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) – Chato | Geita |
| 37. | Viwanda | Uendelezaji wa Miundombinu ya SIDO – Geita | Geita |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 38. | Utawala Bora | Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa – Geita | Geita |
| 39. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi ya Mkoa ya Uhamiaji – Geita | Geita |
| 40. | Afya | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita | Geita |
| 41. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Askari Tanzania | Geita |
| 42. | Madini | Kituo cha Mfano cha Uchenjuaji Madini ya Dhahabu kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo – Lwamgasa. | Geita |
| 43. | Elimu | Upanuzi na ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa – MUCE | Iringa |
| 44. | Uchukuzi | Upanuzi na Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege – Iringa | Iringa |
| 45. | Afya | Uboreshaji wa Hospitali za rufaa za Mikoa - Hospitali ya rufaa ya mkoa wa Iringa | Iringa |
| 46. | Elimu | Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma – Kagera | Kagera |
| 47. | Viwanda | Uendelezaji wa Miundombinu ya SIDO – Bukoba | Kagera |
| 48. | Afya | Ujenzi wa Jengo la Mionzi Katika Kituo cha Afya cha Zamzam | Kagera |
| 49. | Ujenzi | Ujenzi wa Daraja la Kitengule | Kagera |
| 50. | Afya | Ukarabati wa Chuo cha Afya Kagemu | Kagera |
| 51. | Elimu | Ukarabati wa Maktaba Kuu ya Mkoa Wa Kagera | Kagera |
| 52. | Afya | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Wa Katavi | Katavi |
| 53. | Elimu | Mradi wa Ujenzi wa Bweni la Wasichana Shule ya Sitalike | Katavi |
| 54. | Madini | Mradi wa Usimamizi Rasilimali Madini | Katavi |
| 55. | Maji | Ujenzi wa Bwawa la Maji Kijiji cha Nsenkwa | Katavi |
| 56. | Maji | Mradi wa Maji Shankala | Katavi |
| 57. | Maji | Mradi wa Maji Kijiji cha Vikonge | Katavi |
| 58. | Uchukuzi | Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi Wa Miundombinu ya Hali ya Hewa Mkoa wa Katavi | Katavi |
| 59. | Utawala Bora | Mahakama ya Wilaya Tanganyika | Katavi |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 60. | Maji | Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Mkoa Wa Kigoma | Kigoma |
| 61. | Uchukuzi | Uboreshaji wa Bandari-Ziwa Tanganyika (Kigoma) | Kigoma |
| 62. | Afya | Ujenzi wa Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Wa Kigoma | Kigoma |
| 63. | Utawala Bora | Uimarishaji wa Mashamba ya Magereza | Kigoma |
| 64. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Kabingo - Kasulu - Manyovu (Km 260.6) | Kigoma |
| 65. | Ujenzi | Ukarabati na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kigoma | Kigoma |
| 66. | Nishati | Kuzalisha Nishati Jadidifu Kigoma | Kigoma |
| 67. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza -Kaliua – Tabora (km 389.7) | Kigoma |
| 68. | Viwanda | Mradi wa Kufufua Kiwanda cha KMTC | Kilimanjaro |
| 69. | Viwanda | Kiwanda cha Ngozi cha Himo – Kilimanjaro | Kilimanjaro |
| 70. | Viwanda | Kiwanda cha Sukari - TPC Moshi Limited | Kilimanjaro |
| 71. | Viwanda | Kiwanda cha Kilimanjaro Industrial Development Trust (KIDT) - Tawi la Same | Kilimanjaro |
| 72. | Viwanda | Kiwanda cha Kilimanjaro Biochem Co. Ltd | Kilimanjaro |
| 73. | Viwanda | Mradi wa Uendeshaji wa Kiwanda cha Imara Furniture | Kilimanjaro |
| 74. | Elimu | Ukarabati wa Maktaba ya Mkoa | Kilimanjaro |
| 75. | Afya | Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto – Kilimanjaro | Kilimanjaro |
| 76. | Afya | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kaskazini – KCMC | Kilimanjaro |
| 77. | Viwanda | Kiwanda cha Uzalishaji wa Saruji Moshi Cement Ltd- Kilimanjaro | Kilimanjaro |
| 78. | Uchukuzi | Mradi wa Rada ya Kuongozea Ndege Za Kiraia – KIA | Kilimanjaro |
| 79. | Viwanda | Kiwanda cha Kutengeneza Magunia ya Mkonge- Moshi | Kilimanjaro |
| 80. | Viwanda | Kiwanda cha Ngozi Moshi (Moshi Leather Industrial Ltd) | Kilimanjaro |
| 81. | Afya | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kilimanjaro – Mawenzi | Kilimanjaro |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 82. | Viwanda | Kiwanda Cha Bia Cha Serengeti – Kilimanjaro | Kilimanjaro |
| 83. | Uvuvi | Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa | Lindi |
| 84. | Maji | Mradi Wa Maji Mkutano | Lindi |
| 85. | Maji | Ujenzi wa Mradi wa Maji Mchangani | Lindi |
| 86. | Maji | Mradi wa Maji Makanjiro - Ruangwa | Lindi |
| 87. | Maji | Mradi wa Maji Kiwawa | Lindi |
| 88. | Maji | Mradi wa Maji Marendego | Lindi |
| 89. | Nishati | Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia Mikoa ya Dar Es Salaam, Mtwara, Lindi Na Pwani (Lindi) | Lindi |
| 90. | Ujenzi | Barabara ya Nachingwea - Ruangwa - Nanganga (km 106): LOT 2 Ruangwa - Nanganga (km 53.2) | Lindi |
| 91. | Utawala Bora | Mradi wa Ujenzi wa Ofisi Za Uhamiaji Mkoa wa Lindi | Lindi |
| 92. | Ujenzi | Ujenzi wa Daraja la Magara (Mita 84) na barabara Unganishi (Km 5.2) | Manyara |
| 93. | Afya | Uboreshaji wa Hospitali za Rufaa za Mikoa - Hospitali ya Mkoa wa Manyara | Manyara |
| 94. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji ya Mkoa wa Manyara | Manyara |
| 95. | Madini | Ujenzi wa Soko la Madini – Mirerani | Manyara |
| 96. | Maji | Uendelezaji wa Miundombinu ya Maji Darakuta – Magugu – Mwada | Manyara |
| 97. | Utawala Bora | Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Bunda | Mara |
| 98. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya – Nansio (km 121.9) | Mara |
| 99. | Afya | Mradi wa kuboresha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara – Kwangwa | Mara |
| 100. | Elimu | Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu (EP4R) | Mara |
| 101. | Elimu | Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) cha Wilaya ya Butiama kupitia programu ya ESPJ | Mara |
| 102. | Ustawi wa Jamii | Ujenzi na upanuzi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) | Mara |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 103. | Maji | Usambazaji maji katika Manispaa ya Musoma na vijiji 21 vya Wilaya ya Butiama | Mara |
| 104. | Maji | Usambazaji maji wa Mugango - Kiabakari – Butiama | Mara |
| 105. | Utawala Bora | Ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa tatu kwa ajili ya makazi ya askari polisi Manispaa ya Musoma | Mara |
| 106. | Viwanda | Kiwanda cha kuchakata kahawa cha Northern Highlands Coffee Company Limited – Tarime | Mara |
| 107. | Viwanda | Kiwanda cha Kusindika Alizeti – Rorya | Mara |
| 108. | Viwanda | Kiwanda cha Kuchakata Samaki Manispaa ya Musoma | Mara |
| 109. | Biashara | Ujenzi wa Soko la Kisasa Tarime | Mara |
| 110. | Maji | Mradi wa Maji Suguti/Kisenyi/Kwikonero | Mara |
| 111. | Maji | Mradi wa Maji – Iramba | Mara |
| 112. | Maji | Ukarabati wa Mradi wa Maji Kenyana – Nyamititа | Mara |
| 113. | Maji | Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji Bunda | Mara |
| 114. | Maji | Ujenzi wa Jengo la Utawala Tarime Mji | Mara |
| 115. | Utawala Bora | Ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja A – Tarime Rorya, Mara | Mara |
| 116. | Utawala Bora | Mradi wa Ujenzi wa Ofisi Ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara | Mara |
| 117. | Utawala Bora | Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Butiama | Mara |
| 118. | Afya | Uboreshaji wa Hospitali za Rufaa za Mikoa - Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya | Mbeya |
| 119. | Afya | Uboreshaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya | Mbeya |
| 120. | Elimu | Uboreshaji wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya – MUST | Mbeya |
| 121. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Igawa – Songwe - Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (Uyole – Songwe) | Mbeya |
| 122. | Utawala Bora | Ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo | Mbeya |
| 123. | Maendeleo ya | Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya | Mbeya |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| | Jamii | Wananchi – Nzovwe FDC | |
| 124. | Elimu | Ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Chunya | Mbeya |
| 125. | Mawasiliano | Anuani za Makazi na Postikodi | Mbeya |
| 126. | Ujenzi | Ujenzi wa barabara ya Mbeya – Makongolosi - Manyoni (Km 528) – Kipande cha Mbeya | Mbeya |
| 127. | Elimu | Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 (Tanzania Covid Relief Plan - TCRP) - Vyumba vya madarasa | Mikoa yote Tanzania Bara |
| 128. | Ujenzi | Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 142) Sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 24) | Morogoro |
| 129. | Ujenzi | Barabara ya Kidatu – Ifakara (km 66.9 | Morogoro |
| 130. | Viwanda | Kiwanda Sukari Mkulazi - Mbigiri Estate | Morogoro |
| 131. | Kilimo | Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ya Ikolojia- Lukenge Irrigation Scheme | Morogoro |
| 132. | Kilimo | Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania - Gairo, Morogoro | Morogoro |
| 133. | Maendeleo ya Jamii | Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo Wananchi - Bigwa FDC, Morogoro | Morogoro |
| 134. | Sheria | Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo - Mang’ula, Morogoro | Morogoro |
| 135. | Habari | Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania – TBC | Morogoro |
| 136. | Viwanda | Ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Maziwa - Kingolwira | Morogoro |
| 137. | Sheria | Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki - IJC Morogoro | Morogoro |
| 138. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Gairo | Morogoro |
| 139. | Afya | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mkunwa | Mtwara |
| 140. | Afya | Mradi wa Ujenzi wa Jengo La Wagonjwa Mahututi (ICU) | Mtwara |
| 141. | Afya | Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara | Mtwara |
| 142. | Elimu | Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mfano Likombe | Mtwara |
| 143. | Kilimo | Ujenzi wa Ghala na Miundombinu Nanyumbu | Mtwara |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 144. | Maji | Mradi wa Maji - Chemchem | Mtwara |
| 145. | Maji | Mradi wa Maji Namanjele - Njumbuli | Mtwara |
| 146. | Maji | Mradi wa Maji Mkululu | Mtwara |
| 147. | Maji | Mradi wa Maji Namatunu | Mtwara |
| 148. | Maji | Mradi wa Maji Kilombero | Mtwara |
| 149. | Maji | Mradi wa Chujio La Maji | Mtwara |
| 150. | Nishati | Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia Katika Mikoa ya Dar Es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani (Mtwara) | Mtwara |
| 151. | Ujenzi | Ujenzi na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Mtwara | Mtwara |
| 152. | Ujenzi | Ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi (M 3,200) na Barabara Unganishi (Km 1.66) | Mwanza |
| 153. | Kilimo | Mradi wa Kudhibiti Sumu Kuvu - Ujenzi wa Ghala na Miundombinu Wezeshi Katika Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa | Mwanza |
| 154. | Afya | Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Wa Mwanza - Sekou Toure | Mwanza |
| 155. | Elimu | Upanuzi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP Expansion Program) – Kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa Mwanza | Mwanza |
| 156. | Uchukuzi | Mradi wa Rada ya Kuongozea Ndege za Kiraia – Mwanza | Mwanza |
| 157. | Uchukuzi | Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Meli | Mwanza |
| 158. | Utawala Bora | Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Kamanda wa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza | Mwanza |
| 159. | Viwanda | Uendelezaji wa Maeneo ya Viwanda vya Shirika La Maendeleo la Taifa – Mwanza | Mwanza |
| 160. | Uchukuzi | Ujenzi wa Jengo la Abiria Katika Uwanja wa Ndege Mwanza | Mwanza |
| 161. | Afya | Mradi wa Ujenzi Wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe Awamu ya Pili | Njombe |
| 162. | Elimu | Mradi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Njombe | Njombe |
| 163. | Maji | Mradi wa Maji Kijiji cha Nyombo | Njombe |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 164. | Maji | Mradi wa Maji Kibena Howard | Njombe |
| 165. | Maji | Mradi wa Maji Igula | Njombe |
| 166. | Ujenzi | Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje (Km 157.4): Kipande Moronga – Makete (Km 53.5) | Njombe |
| 167. | Utawala Bora | Mradi wa Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Njombe | Njombe |
| 168. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Njombe | Njombe |
| 169. | Maji | Mradi wa Maji Idende - Unenamwa | Njombe |
| 170. | Nishati | Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115: | Pwani |
| 171. | Viwanda | Mradi wa Uendelezaji wa Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo | Pwani |
| 172. | Nishati | Ujenzi wa daraja jipya la Wami na barabara unganishi | Pwani |
| 173. | Maji | Mradi wa bomba la kusafirisha maji kutoka Mlandizi (Ruvu juu) hadi Chalinze (kijiji cha Mboga) | Pwani |
| 174. | Viwanda | Uwekezaji katika Kiwanda cha Kutengeneza chumvi neel kanth salt- Pwani | Pwani |
| 175. | Viwanda | Kiwanda cha uzalishaji cha marumaru – Goodwill (t) Ceramic co. Ltd | Pwani |
| 176. | Viwanda | Kiwanda cha kuchakata kahawa cha Rafiki Coffee Limited | Pwani |
| 177. | Viwanda | Kiwanda cha kuzalisha Saruji cha Fortune Cement (t) Company Limited | Pwani |
| 178. | Viwanda | Mradi wa kiwanda cha uzalishaji wa nyaya za mawasiliano (Fiber Optic Cables) cha Raddy Fiber Manufacturing Tanzania Ltd | Pwani |
| 179. | Viwanda | Kiwanda cha uzalishaji wa Plasta bodi na poda ya gypsum –Kauf Gypsum Tanzania Limited | Pwani |
| 180. | Viwanda | Eneo la Kongane ya Viwanda – TAMCO. | Pwani |
| 181. | Afya | Uboreshaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Wa Sumbawanga | Rukwa |
| 182. | Maji | Mradi wa Maji Kanoge Ii | Rukwa |
| 183. | Maji | Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Maji Ikozi | Rukwa |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 184. | Maji | Mradi wa Maji Msandamuungano | Rukwa |
| 185. | Maji | Ujenzi wa Bwawa la Maji Kijiji cha Kalepula | Rukwa |
| 186. | Maji | Ujenzi wa Bwawa la Maji Kilewani | Rukwa |
| 187. | Maji | Mradi wa Maji Matai | Rukwa |
| 188. | Maji | Mradi wa Maji Isale | Rukwa |
| 189. | Maji | Mradi wa Maji Matala | Rukwa |
| 190. | Maji | Mradi wa Maji Kasu | Rukwa |
| 191. | Maji | Hospitali ya Wilaya ya Sumbawanga - MTOWISA | Rukwa |
| 192. | Maji | Mradi wa Maji Muze Group | Rukwa |
| 193. | Nishati | Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (Awamu ya Pili ya Mradi wa Rea III) Katika Mkoa wa Rukwa | Rukwa |
| 194. | Ujenzi | Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga (Km 112) | Rukwa |
| 195. | Elimu | Mradi wa Chuo cha Maendeleo Ya Wananchi Mputa | Ruvuma |
| 196. | Elimu | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi - Mbinga | Ruvuma |
| 197. | Kilimo | Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini – SMMRP: Kituo cha Umahiri Songea | Ruvuma |
| 198. | Kilimo | Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kudhibiti Sumukuvu | Ruvuma |
| 199. | Kilimo | Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu – FORVAC (Ruvuma) | Ruvuma |
| 200. | Maji | Mradi wa Maji Ruvumachini | Ruvuma |
| 201. | Maji | Mradi wa Maji Mangamao | Ruvuma |
| 202. | Maji | Mradi wa Maji Liuli Group | Ruvuma |
| 203. | Maji | Mradi wa Maji Mabuni | Ruvuma |
| 204. | Uchukuzi | Mradi wa Ukarabati na Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Songea | Ruvuma |
| 205. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara Mbinga - Mbamba Bay kwa Kiwango cha Lami (Km 66) | Ruvuma |
| 206. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Kitai - Lituhi Km 84.5 | Ruvuma |
| 207. | Elimu | Ujenzi na Ukarabati wa Chuo Cha Ualimu | Shinyanga |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| | | Shinyanga | |
| 208. | Afya | Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa - Hospitali ya Rufaa Shinyanga | Shinyanga |
| 209. | Maendeleo ya Jamii | Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo Wananchi - FDC | Shinyanga |
| 210. | Elimu | Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi Kampasi ya Kizumbi – Shinyanga | Shinyanga |
| 211. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Uhamiaji – Ofisi ya Kamanda wa Uhamiaji Mkoa wa Shinyanga | Shinyanga |
| 212. | Kilimo | Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi – Shinyanga | Shinyanga |
| 213. | Nishati | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa KV 400 Iringa – Singida – Shinyanga (BTIP II) | Shinyanga |
| 214. | Uchukuzi | Mradi wa Kiwanja cha Ndege Shinyanga | Shinyanga |
| 215. | Viwanda | Kiwanda cha *Jambo Food Products Limited*. | Shinyanga |
| 216. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu | Simiyu |
| 217. | Kilimo | Mradi wa kudhibiti Sumukuvu - Itilima | Simiyu |
| 218. | Utawala Bora | Ujenzi wa nyumba mbili za makazi ya askari polisi Wilaya ya Meatu | Simiyu |
| 219. | Ujenzi | Ujenzi wa barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 121.9) | Simiyu |
| 220. | Viwanda | Ujenzi wa viwanda vya chaki na vifungashio katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa. | Simiyu |
| 221. | Elimu | Ujenzi wa Vyumba Vya Madarasa Biashara Sekondari (EP4R) | Simiyu |
| 222. | Elimu | Ujenzi Wa Vyumba vya Madarasa Bariadi Sekondari ((EP4R) | Simiyu |
| 223. | Kilimo | Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu | Simiyu |
| 224. | Maji | Mradi wa Maji Nyamalapa | Simiyu |
| 225. | Maji | Mradi wa Maji Lamadi – Mkula | Simiyu |
| 226. | Maji | Mradi wa Maji Ngulyati – Nyamswa | Simiyu |
| 227. | Maji | Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Maji – Maswa | Simiyu |
| 228. | Ujenzi | Barabara ya Maswa Bypass (Km 11.3) | Simiyu |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 229. | Utawala Bora | Ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B – Bariadi - Simiyu | Simiyu |
| 230. | Maendeleo ya Jamii | Ukarabati wa vyuo vya Maendeleo ya Wananchi – FDC | Singida |
| 231. | Ujenzi | Ujenzi wa barabara ya Mbeya – Makongolosi - Manyoni (KM 528) – Kipande cha Manyoni | Singida |
| 232. | Nishati | Ujenzi wa njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida - Arusha - Namanga (KTPIP) – kituo cha kupoza umeme wa kV 400 | Singida |
| 233. | Uchukuzi | Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Songwe | Songwe |
| 234. | Ujenzi | Ujenzi wa barabara ya Mpemba - Isongole (Km 51.2) | Songwe |
| 235. | Afya | Uboreshaji wa Hospitali za Rufaa za Mikoa - Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe | Songwe |
| 236. | Nishati | Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (EACOP) | Tabora |
| 237. | Kilimo | Kudhibiti Sumukuvu – Halmashauri ya Wilaya ya Nzega | Tabora |
| 238. | Elimu | Ukarabati wa Jengo la Maktaba ya Mkoa wa Tabora | Tabora |
| 239. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 365.98) | Tabora |
| 240. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Nyahua – Chaya (km 170), Kipande cha Nyahua - Chaya (km 85.4) | Tabora |
| 241. | Uchukuzi | Ukarabati Wa Majengo ya Mamlaka ya Hali ya Hewa, Tabora | Tabora |
| 242. | Viwanda | Ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata na Kufungasha Mazao ya Nyuki – Sikonge | Tabora |
| 243. | Ujenzi | Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Tabora | Tabora |
| 244. | Ujenzi | Ujenzi Wa Barabara ya Tanga – Pangani - Makurunge (km 256) | Tanga |
| 245. | Uchukuzi | Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Tanga | Tanga |
| 246. | Uchukuzi | Mradi wa Ufufuaji wa Njia ya Reli ya Tanga - Arusha (km 437) | Tanga |
| 247. | Viwanda | Kiwanda cha Kusindika Chai - Mponde | Tanga |
| 248. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Muheza - Amani (km 40) kwa Kiwango Cha Lami | Tanga |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 249. | Afya | Uboreshaji wa Hospitali ya Rufaa – Tanga | Tanga |
| 250. | Viwanda | Kiwanda cha Kuchakata Maziwa cha Tanga Fresh Limited | Tanga |
| 251. | Viwanda | Kiwanda cha Kuchakata Maganda ya Miwati | Tanga |
| 252. | Viwanda | Kiwanda cha Kuzalisha Saruji cha Kilimanjaro Cement Company Limited | Tanga |
| 253. | Utalii | Jengo la Kuhifadhi Kumbukumbu – Makumbusho Urithi Tanga | Tanga |



Tume ya Mipango,
Mji wa Serikali-Mtumba,
Mtaa wa Makamu wa Rais,
S.L.P 1324, 40477 Dodoma.